# ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA RIWAYA ZA *NYONGO MKALIA INI* NA *MAFAMBA*

**BEATRICE WANJIKU NDUNG'U**

**C50/CE/25704/2014**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**APRILI, 2022**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi:…………………………………..… Tarehe: 04/04/2022……………………………

**Beatrice Wanjiku Ndung'u**

**C50/CE/25704/2014**

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:…………………………………..… Tarehe: 9/4/2022……………………………

**Dkt. Richard Wafula**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

Sahihi:…………………………………..… Tarehe: 04/04/2022……………………………

**Dkt. Jessee Murithi**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mume wangu mpendwa, Samson Ndung'u kwa kunionyesha upendo na kunitia moyo wakati wa utafiti wa kazi hii. Pia, nawatunikia tabaruku wanangu Lincoln, Lynn, Tiffany na Tinah.

# SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kunipa nguvu na kunijalia baraka zake hadi kutimia kwa kazi hii. Ni kwa neema zake ambapo kazi hii imekamilika.

Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Dkt. Jessee Murithi kutokana na mwongozo wenu na ushauri wa mara kwa mara ulioniwezesha kutimiza ndoto yangu ya kufuzu katika shahada ya uzamili. Ninawashukuru pia Dkt. Pamela, Dkt. Osore na Dkt. Beth kwa ushauri na walionipa mwanzoni mwa kazi hii.

Ningependa aidha kuwashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa kunipa mwongozo wakati wa kutetea pendekezo langu la utafiti. Walinifaa sana.

Aidha, natoa shukrani kwa wanafunzi wenzangu Dan, Steve, Dorcas, Pauline, Kioko, Carol, Hawa, Mercy, Kerre na wengine wengi ambao sijataja. Kila mara walinitia moyo na kunipa ushauri.

Nashukuru mume wangu mpendwa Samson Ndung’u na watoto wangu Lincoln, Lynn, Tiffany na Tinah kwa mapenzi yao ya dhati na kunihimiza nijitahidi kumaliza kazi hii.

Ninatoa shukrani zangu kwa wazazi wangu Bwana Patrick Njoroge na mama Jane Wangui. Mliniwekea msingi wa masomo yangu. Aidha, wacheja wangu Bwana Peter Nyinge na mama Teresia Waithira kwa nasaha yao ya kila mara. Mungu aendelee kuwaongoza na kuwabariki.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza athari za matukio ya kihistoria katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* Chimerah, (1995) na *Mafamba* Olali, (2008). Athari za matukio ya kihistoria ambazo hujumuisha maswala ya siasa, uongozi, uchumi na maswala ya kijamii kwa jumla na jinsi yanavyoathiri usawiri wa maudhui, wahusika na mtindo na lugha ni swala ambalo halikuwa limeshughulikiwa kama mada mahususi ya utafiti katika riwaya. Malengo ya utafiti huu yamekuwa ni kuchunguza iwapo matukio ya kihistoria huathiri jinsi waandishi wanavyowasilisha maudhui yao, kuchunguza ikiwa matukio ya kihistoria huathiri usawiri wa wahusika na kuchunguza iwapo matukio ya kihistoria huathiri mtindo na lugha ambayo waandishi hutumia katika kuwasilisha kazi ya fasihi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhistoria mpya iliyoasisiwa na Greenblatt (1980). Nadharia hii huangazia umuhimu wa muktadha katika utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi. Aidha, huonyesha kuwa, jinsi jamii zinavyozidi kukua, utamaduni hubadilika kiwakati na jambo hili huathiri utunzi, uwasilishaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Utafiti huu umefanyika maktabani. Udurusu wa kina wa vitabu vilivyoteuliwa, makala mbalimbali na tasnifu za watangulizi umefanywa. Matokeo yametolewa kwa njia ya kimaelezo. Ripoti ya utafiti huu imepangwa katika sura tano. Utafiti huu umetoa mchango kwa wasomi na watafiti katika kuonyesha kuwa matukio ya kihistoria yamewaathiri waandishi katika usawiri wa maudhui, wahusika na mtindo na lugha kwenye riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* mtawalia.

# ABSTRACT

This research study investigated the effect of historical events on the selected two novels *Nyongo Mkalia Ini (*Chimerah, 1995) and *Mafamba* (Olali, 2008). The effects of historical events that include political, administrative, economic and social issues in general and how they affect the presentation of themes, characters and style and language is an issue that has not been addressed as a specific research research topic in the novel. The aim of this research has been to investigate whether historical events affect how novelists portrays themes in their literary works, investigate how historical events affect characterization and investigate how historical events affect the linguistic styles in swahili novel. The research has employed new historicism theory which was founded by Greenblatt (1980). New historicism theory puts into consideration contextual importance in composing and analyzing literary work. The theory also stipulates that, as the society develops; cultural changes occur that consequently affects composition, depiction and analysis of literary works. The topic on effect of historical events to the development of Swahili novel is important for various reasons. This research has been done in the library through reading the selected novels, journals and prior literary works relevant to the research. Research findings have be presented through analysis and explanations. The research has been presented in five chapters. The research has shown the effects of historical events on *Nyongo Mkalia Ini* and *Mafamba.* The research has shown that historical events have affected writers in depicting their themes, characters and linguistic styles in *Nyongo Mkalia Ini* and *Mafamba* respectively.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

**Matukio** - Mambo ambayo yalifanyika.

**Historia** - Ni masimulizi ya matukio na mambo yaliyopita.

**Maudhui** - Ni jambo kuu linaloshughulikiwa katika kazi ya fasihi.

**Wahusika** - Ni vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa.

**Mtindo** - Ni upekee wa mwandishi katika kuwasilisha kazi ya sanaa.

**Mandhari** **-** Ni mazingira ya utunzi ya kazi za kifasihi.

## VIFUPISHO

TY: Tafsiri yetu

**YALIYOMO**


IKIRARI ........................................................................................................ ii

TABARUKU .................................................................................................. ii

SHUKRANI.....................................................................................................iv

IKISIRI ............................................................................................................v

ABSTRACT ...................................................................................................vi

MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU ............................................................ vii

VIFUPISHO .................................................................................................. viii

YALIYOMO....................................................................................................ix

**SURA YA KWANZA** ......................................................................................1

**UTANGULIZI** .................................................................................................1

1.0 Utangulizi ......................................................................................................1

1.1 Usuli wa Mada............................................................................................. 1

1.2 Suala la Utafiti ............................................................................................. 5

1.3 Malengo ya Utafiti........................................................................................ 7

1.4 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 7

1.5 Sababu za Kuchagua Mada........................................................................... 8

1.6 Upeo na Mipaka............................................................................................ 9

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..................................................................... 11

1.8 Misingi ya Nadharia .................................................................................... 20

1.8.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhistoria Mpya.................................................... 22

1.9 Mbinu za Utafiti........................................................................................... 24

1.9.1 Muundo wa Utafiti ........ 25
1.9.2 Mahali pa Utafiti ........ 25
1.9.3 Sampuli na Usampulishaji ........ 26
1.9.4 Ukusanyaji wa Data ........ 27
1.9.5 Uchanganuzi wa Data ........ 27
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ........ 27
1.9.7 Uzingatifu wa Maadili ........ 28
1.10 Hitimisho ........ 28
**SURA YA PILI** ........ 30
**ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA KUWASILISHA MAUDHUI KATIKA RIWAYA TEULE** ........ 30
2.0 Utangulizi ........ 30
2.1 Dhana ya Vipindi vya Kihistoria ........ 30
2.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Maudhui katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ........ 31
2.2.1 Maudhui ya Vita vya Uhuru ........ 32
2.2.2 Maudhui ya Mizozo ya Ardhi ........ 35
2.2.3 Maudhui ya Siasa ........ 37
2.2.4 Maudhui ya Elimu ........ 41
2.2.5 Maudhui ya Utabaka ........ 44
2.3 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Maudhui kwenye Riwaya ya *Mafamba* (2008) ........ 46

2.3.1 Maudhui ya Ufisadi ........................................................................ 46

2.3.2 Maudhui ya Siasa.......................................................................... 49

2.3.3 Maudhui ya Elimu ........................................................................ 51

2.3.4 Maudhui ya Usaliti ........................................................................ 53

2.3.5 Maudhui ya Vita vya baada ya Uchaguzi ........................................ 55

2.3.6 Maudhui ya Ukombozi .................................................................. 56

2.4 Hitimisho ....................................................................................... 58

**SURA YA TATU** .............................................................................61

**ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KWA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA TEULE**..............................................................................61

3.0 Utangulizi ...................................................................................... 61

3.1 Dhana ya Wahusika ........................................................................ 61

3.1.1 Uhusika na Wahusika katika Fasihi.............................................. 62

3.1.2 Wahusika wa Kihistoria................................................................. 63

3.1.3 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Wahusika katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia ini* (1995)........................................................ 63

3.1.4 Omari ............................................................................................ 65

3.1.5 Mumanyi........................................................................................ 66

3.1.6 Munga............................................................................................ 67

3.1.7 Bwana Khalifa ............................................................................... 70

3.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Wahusika katika Riwaya ya *Mafamba* (2008)......................................................................... 72

3.2.1 Maotad ........................................................................................................ 74

3.2.2 Amrao ......................................................................................................... 75

3.2.3 Limioe......................................................................................................... 77

3.2.4 Manstanji .................................................................................................... 79

3.3 Hitimisho ...................................................................................................... 80

**SURA YA NNE** .................................................................................................82

**ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA KUWASILISHA MTINDO NA LUGHA KATIKA RIWAYA TEULE** .....................................82

4.0 Utangulizi ..................................................................................................... 82

4.1 Dhana ya Mtindo ........................................................................................... 82

4.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Mtindo na Lugha katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ..................................................................... 83

4.2.1 Matumizi ya Taashira ..................................................................................... 83

4.2.1.1 Matumizi ya Taashira ya Jipu..................................................................... 84

4.2.1.2 Matumizi ya Taashira ya Damu................................................................... 87

4.2.1.3 Taashira ya Pembe za Ndovu ...................................................................... 89

4.2.1.4 Taashira ya Sanamu na Picha ..................................................................... 92

4.3 Matumizi ya Jazanda ........................................................................................ 93

4.3.1 Matumizi ya Jazanda katika *Nyongo na Ini*................................................... 94

4.4 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Uwasilishaji wa Mtindo na Lugha katika Riwaya ya *Mafamba* (2008) ........................................................................ 97

4.4.1 Matumizi ya Maelezo ..................................................................................... 97

4.4.2 Matumizi ya Mjadala ........ 99
4.4.3 Matumizi ya Utambaji ........ 100
4.4.4 Matumizi ya Nyimbo ........ 102
4.4.5 Matumizi ya Anagramu ........ 106
4.4.6 Matumizi ya Mdokezo ........ 107
4.5 Hitimisho ........ 108
**SURA YA TANO** ........ 110
**MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO** ........ 110
5.0 Utangulizi ........ 110
5.1 Muhtasari ........ 110
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 112
5.3 Changamoto za Utafiti ........ 120
5.4 Mchango wa Matokeo ya Utafiti ........ 120
5.5 Mapendekezo ........ 121
**MAREJELEO** ........ 122

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Aidha, sababu za kuchagua mada na umuhimu wake, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia na mbinu zilizotumiwa katika utafiti; muundo wa utafiti, njia za kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

## 1.1 Usuli wa Mada

Chanzo cha fasihi ni katika maisha ya binadamu. Madumulla (1988) anaeleza kuwa katika kipindi cha maisha kuna matukio fulani ambayo hujitokeza zaidi kuliko mengine. Baadhi ya matukio haya yanaweza kuiathiri jamii kwa njia chanya au kwa njia hasi kulingana na kipindi maalum cha kihistoria. Matukio haya huwa na athari kwa jamii husika na huwa katika kumbukumbu za jamii hiyo miaka mingi halafu. Maswala ya kihistoria huathiri utunzi wa msanii kimaudhui, kifani na kidhamira.

Mlacha (1984) anahoji kuwa historia ya kipindi fulani cha utunzi ina umuhimu katika utunzi wa kazi za kifasihi ikiwemo riwaya. Waandishi wa kazi za fasihi wana nafasi mbalimbali za kukashifu uovu na kuyamulika maswala mbalimbali yanayowaathiri wanajamii. Lengo la mwandishi ni kuiumba jamii mpya kwa kuwa

fasihi ni kioo cha jamii. Aidha riwaya ni utanzu ambao humulika ule urazini wa jamii husika katika kipindi husika.

Wellek na Warren (1949) wanailezea fasihi kama sanaa inayotumia lugha kiubunifu. Njogu na Chimerah (1999) wanaielezea fasihi kuwa aina ya sanaa inayotumia lugha ili kusimulia tajriba za binadamu. Wamitila (2008) anahoji kuwa fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Wamitila (2003), anaeleza fasihi andishi kuwa ni fasihi ambayo kimsingi huhifadhiwa kwa njia ya maandishi

Kwa mujibu wa King'ei (1999), maendeleo ya riwaya ya Kiswahili nchini Kenya yanaweza kuainishwa katika vipindi vinne. Kipindi cha kwanza kilikuwa kati ya mwaka (1850-1890) kabla ya kupata uhuru. Kipindi hiki kilishuhudia mwanzo wa mfumo wa kijamii wa Waswahili kuvunjiliwa mbali huku mahali pake pakichukuliwa na mfumo wa kibwanyenye. Kipindi hiki kilishughulikia zaidi maudhui yaliyoegemea sana upande wa dini. Kazi za kinathari ingawa hazikuwa nyingi, zilijikita katika maswala ya kidini. Kipindi kilichofuata kati ya mwaka (1890–1930) kilikuwa chenye uhaba wa kazi za kinathari huku kipindi cha tatu kati ya mwaka (1963-1992) kikiwa kile cha mapambano ya uhuru. Kwa mujibu wa uainishaji huu, kipindi kilichopo katika utunzi wa riwaya kilianza mwaka wa 1992 hadi wakati huu. Kipindi hiki kimeshuhudia utanzu wa riwaya ukianza kupokea

mielekeo tofauti na mipya ya kimuundo na kimaudhui iliyoambatana na mabadiliko na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiitikadi na kisiasa. Kutokana na yale yaliyokuwa yakifanyika katika nchi nyingi za Afrika, mambo haya ni bayana kuwa yalijitokeza. Kwa mujibu wa Kapiyo na wenzake (2011), historia ni maelezo ya matukio ya wakati uliopita. Aidha, ni tawi la elimu linaloshughulikia maswala ya wakati uliopita ya wanadamu na jinsi wanvyoathirika na mazingira yao kwa miaka kadhaa (TY).

Mbatiah (2016) anasema kuwa, historia ya riwaya haiwezi ikalinganishwa na historia ya fasihi simulizi. Anadai kuwa, fasihi andishi ilikuja baada ya uvumbuzi wa kimaandishi ambapo kazi kama *Don Quixote* (1605). Wataalamu wengi wa fasihi wanahusisha kuzaliwa kwa riwaya na kazi hii. Kwa mujibu wa Mbatiah (2016), Barani Afrika, uandishi wa riwaya tangu mwanzo ulikuwa tofauti na ule wa Ulaya kwa kuwa mazingira ya Kiafrika yalikuwa tofauti kabisa. Hii ni kwa sababu Afrika haikuwa na tabaka la matajiri waliokuwa na wakati wa kusoma majuzuu ya riwaya. Pia, hadhira ya wasomaji wa Kiafrika ilikuwa makundi madogo ya watu waliopata elimu ya kimishonari kwa kuwa idadi ya watu wengi haikuwa na ujuzi wa kusoma na kuandika.

Riwaya nyingi za Kiswahili zinadhihirisha dhana ya historia. Waandishi kama Said A. Mohamed, Adam Shafi na wengine wameandika kazi za kihistoria kama njia moja ya kuonyesha maendeleo ya kijamii kuanzia miaka ya wakoloni hadi

sasa (Wafula na Njogu, 2007). Mbatiah (1999) alitafiti kuhusu Chimbuko na maendeleo ya riwaya ya Kiswahili nchini Tanzania. Alisema kuwa hatua muhimu katika maendeleo ya riwaya ya Kiswahili yalikuwa tokeo la matukio ya kihistoria na jamii nchini Tanzania.

Mbatiah (1999) anahoji kuwa kabla ya kuja kwa wakoloni, mfumo wa fasihi ulijikita sana katika fasihi simulizi. Anazidi kudokeza kuwa kazi za kibunilizi za awali za Shaban Robert ziliandikwa katika miaka ya arobaini na hamsini, kwa mfano *Adili na Nduguze* (1952) *Kufikirika* (1946) na *Kusadikika* (1951) kazi hizi zilizoandikwa wakati wa ukoloni ziliendeleza fasihi simulizi. Anaendelea kusema kuwa fasihi andishi ilizaliwa katika karne ya ishirini. Huu ulikuwa wakati wa ukoloni ambapo mapambano ya uhuru yalikuwa yakiendelea. Kwa hivyo, kazi nyingi za riwaya ya Kiswahili zilijikita katika maswala ya ukombozi na uhuru wa nchi.

Mbatiah (1999) anaendelea kuonyesha kuwa chanzo cha riwaya ya Kiswahili na maendeleo yake yanahusiana kwa karibu na ukuaji wa Kiswahili nchini Tanzania. Maendeleo haya ya Kiswahili yaliweka msingi dhabiti katika chimbuko na ukuaji wa riwaya pevu. Kwa mfano, waandishi kama vile Kezilahabi na M. S. Mohamed waliibuka kama waandishi mashuhuri walioshughulikia maswala ya uozo wa jamii na uongozi mbaya. Kwa mujibu wa Mbatiah (1999), mfumo wa elimu wa kikoloni nchini Tanzania ulijaribu kutatua tatizo la ukosefu wa vifaa vya kufundisha

Kiswahili kwa kuhimiza tafsiri ya kazi za fasihi ya kiingereza kwa lugha ya Kiswahili.

Katika msingi huu mtafiti ananuia kushughulikia athari za historia katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (Chimerah, 1995) na *Mafamba* (Olali, 2008). Riwaya hizi zina tofauti ya zaidi ya mwongo mmoja. Tofauti ya kipindi hiki cha wakati ni katika tawala mbili tofauti. Kipindi cha utawala wa miaka ya tisini katika utawala wa Rais Moi, kipindi ambacho demokrasia nchini Kenya haikuwepo hivyo basi, waandishi katika kipindi hiki, walitumia lugha fiche katika kuyashughulikia maswala mbalimbali yaliyowaathiri wanajamii.

Kipindi cha pili cha kiwakati ni kipindi cha miaka ya elfu mbili kuendelea. Hiki ni kipindi cha kiwakati ambacho kulikuwa na demokrasia nchini Kenya na waandishi wa fasihi walikuwa na uhuru wa kuangazia maswala mbalimbali kwa uwazi zaidi. Katika kipindi hiki, kulikuwa na milengo mingi ya vyama vya kisiasa kila mlengo ukiahidi kupigana na uozo unaoangaziwa na mwandishi kama mafamba.

## 1.2 Suala la Utafiti

Sababu iliyomchochea mtafiti ni kuwa, asili ya utungo wa fasihi ipo katika maisha ya mwanadamu na mazingira yake maalum ya kihistoria, kijamii na kiuchumi. Malighafi kubwa ya msanii yanapatikana katika mazingira yake ya kijamii na ya kihistoria. Aidha, tajriba ya msanii hutokana na anayoyaona, anayoyasikia, na yale

anayokumbana nayo katika shughuli za kila siku. Nchi ya Kenya imepitia mabadiliko mbalimbali kijamii, kisiasa, kiteknolojia na kiuchumi. Mabadiliko haya yanakisiwa kuwa yaliathiri utunzi wa riwaya kidhamira kimaudhui, mtindo, lugha na usawiri wa wahusika. Mabadiliko haya yanakisiwa kuwa yamesababishwa na mpwito wa wakati. Misingi hii ndiyo imechangia kufanywa kwa utafiti huu. Mtafiti anaamini kuwa utafiti unaofuata mkabala huu haujafanywa kwa kina.

Utafiti huu umeshughulikia athari za matukio ya kihistoria katika riwaya. Riwaya ambazo zimeshughulikiwa ni *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008). Kulingana na mtafiti, athari za matukio ya kihistoria dhidi ya maudhui, wahusika na mtindo katika riwaya ya Kiswahili hazijashughulikiwa kwa kina katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* (Chimerah, 1995) na *Mafamba* (Olali, 2008). Hili ndilo pengo ambalo utafiti umelenga kuziba. Suala la historia linahusisha masuala mengi katika jamii na lina athari za moja kwa moja katika jamii husika. Masuala ambayo yameangaziwa katika riwaya hizi ni ya kijamii, kiuchumi, kisaikolojia, kiteknolojia na kisiasa. Riwaya hizi zina tofauti ya zaidi ya mwongo mmoja. Hivyo, zinakisiwa kuwa zitaweza kuibua tofauti za kimaudhui, mtindo na lugha na usawiri wa wahusika. Huenda tofauti hizi katika kusawiri maudhui, wahusika na mtindo na lugha, zimetokana na riwaya hizi kuandikwa vipindi tofauti vya kiutawala nchini Kenya. Utafiti huu umelenga kuchunguza namna matukio ya

kihistoria yalivyowaathiri waandishi Rocha Chimerah katika riwaya yake ya *Nyongo Mkalia Ini (*1995) na Tom Olali katika riwaya yake ya *Mafamba* (2008).

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

i) Kubaini athari za matukio ya kihistoria katika kuwasilisha maudhui kwenye riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

ii) Kuchunguza athari za matukio ya kihistoria katika usawiri wa wahusika kwenye riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

iii) Kuchunguza athari za matukio ya kihistoria katika uwasilishaji wa mtindo na lugha kwenye riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni kwa jinsi gani matukio ya kihistoria yameathiri namna waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* walivyowasilisha maudhui yao?

ii) Ni kwa jinsi gani matukio ya kihistoria yameathiri namna waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* walivyowasawiri wahusika?

iii) Ni kwa jinsi gani matukio ya historia yameathiri namna waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* walivyowasilisha mtindo na lugha?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Historia katika fasihi andishi hasa utanzu wa riwaya ni muhimu kwani ni katika historia hii ndipo masuala ya maudhui, wahusika na mtindo hupatikana. Riwaya ambazo zimeshughulikiwa zilikisiwa kuwa zitakuwa na maswala mengi ya kihistoria. Mtafiti alinuia kuyaweka bayana mambo yawapatayo watu walio katika jamii ya kisasa.

Waandishi Chimerah na Olali wameshughulikia vipengele mbalimbali katika riwaya teule. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti ili kufahamu namna ambavyo matukio ya kihistoria katika vipindi hivi vya kiwakati yalivyoathiri uwasilishaji wa kazi zao. Mtafiti ameshawishiwa kufanya utafiti na sababu zifuatazo: Kwanza, riwaya hizi *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* husomwa na wanajamii na kila tabaka. Pia, hufunzwa vyuoni hivyo vinapaswa kuhakikiwa ili kuwezesha wasomaji wa riwaya hizi kufahamu zaidi na kuwa na uelewa unaofaa. Isitoshe, utanzu wa riwaya ni utanzu muhimu katika fasihi na unakua kila uchao. Hivyo, utafiti umefanywa ili kutathmini jinsi mabadiliko ya kiwakati yamechangia katika kuleta tofauti katika uwasilishaji wa dhamira, maudhui, mbinu za lugha na usawiri wa wahusika. Vilevile, mitindo iliyotumiwa na waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* ni ya kipekee. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* Rocha Chimerah ametumia mbinu ya taashira iliyofumbika kwa wingi. Pia, ametumia jazanda kwa wingi. Uteuzi wa mbinu hizi ambazo huficha yanavyozungumziwa huenda ulichochewa na jinsi hali ilivyokuwa nchini Kenya

wakati huo. Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ametumia mbinu zilizo wazi zaidi katika kuwasilisha kazi yake. Tofauti hii ya vipindi vya wakati kifasihi imeibua tofauti katika uwasilishaji wa kazi ya riwaya hizi mbili. Hivyo, msomaji yeyote lazima aielewe kwanza ili aelewe kazi hizi.

Aidha, mtafiti ameshawishiwa na haja ya kuchangia taaluma ya uhakiki kwa kuwa riwaya hizi za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* hazijafanyiwa uhakiki wa kutosha kwa kuzingatia vipengele vya maudhui, wahusika na mtindo na lugha. Mbali na hayo, athari za matukio ya kihistoria katika riwaya ni swala ambalo halijazingatiwa kwa kina katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Isitoshe, riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* ni riwaya zinazoakisi hali yakinifu ya mambo yaliyojiri katika jamii. Hivyo, riwaya hizi zinatumika kama kumbukumbu ya matukio muhimu yaliyofanyika nchini Kenya ambayo yaliathiri maisha ya wananchi na jinsi yao ya utendakazi. Hali hii pia, huenda ilimwathiri mwandishi katika uteuzi wake wa maudhui, mbinu za lugha na wahusika na hivyo, zinasaidia katika kutunza historia muhimu kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mada hii pia imesaidia katika kukuza na kuhifadhi historia kama itakavyodhihirika katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba*.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu utashughulikia riwaya mbili za Kiswahili. Riwaya hizi ni: *Nyongo Mkalia Ini* (Chimerah, 1995) na *Mafamba* (Olali, 2008). Kazi hizi ni miongoni

mwa riwaya ambazo zimeshughulikia masuala ya kihistoria nchini Kenya. Utafiti huu umebainisha jinsi matukio ya kihistoria yameathiri usawiri wa maudhui, mtindo na lugha na usawiri wa wahusika kwa mujibu wa tofauti za vipindi maalum vya kihistoria. Riwaya hizi, zilichapishwa katika vipindi tofauti vya kiwakati, hivyo utafiti umebaini kuwa tofauti hii ya kiwakati imeibua tofauti katika uwasilishaji wa maudhui, lugha na mtindo na usawiri wa wahusika.

Kwanza, kazi hizi zimechaguliwa kuwakilisha vipindi tofauti; miaka ya tisini na miaka ya elfu mbili kuendelea ili kuweza kuchunguza athari za matukio ya kihistoria katika vipindi hivi vya wakati. Aidha, waandishi hawa wamechaguliwa kwa sababu wana tajriba pana ya uandishi wa fasihi na kwa hivyo kazi zao zimefaa katika utafiti huu. Sababu ya utafiti huu kuangazia historia ni kuwa kupitia kwayo tumepata kusudio na mafunzo ya watunzi kwa hadhira na wasomaji. Vilevile, jinsi wanavyowasilisha masuala ya kihistoria ni muhimu katika utunzi wa kifasihi kwani watunzi wanatumia njia hiyo kuiathiri jamii kupitia kuzindua, kutahadharisha, kukashifu, kuelekeza na kwa jumla kuelimisha.

Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ni riwaya ambayo inayamulika masuala ya kihalisia katika jamii. Maswala haya ni pamoja na uongozi, madaraka, elimu, ufisadi, ukoloni, ukoloni mamboleo, utabaka, ukombozi, ukabila miongoni mwa mengine. Riwaya ya *Mafamba* (2008) ni riwaya ya kwanza yake Olali inayoangazia hali ya kisiasa katika jamii na harakati za kuwangoa viongozi

wadhalimu. Riwaya hii ni riwaya inayosimulia uozo katika nchi ya Bikerani-Msiige ambapo viongozi wanajihusisha na nyendo za ufisadi uliokita mizizi. Hata baada ya wananchi kuwaondoa mamlakani viongozi hawa, viongozi wapya wanaotawazwa wanaendeleza uozo huu.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Baadhi za kazi zilizoshughulikia historia zimejikita katika kuelezea namna jamii na historia zinavyoungana pamoja. Mink (1974) alifafanua mada ya historia na bunilizi kama mikakati ya ufahamu akirejelea maoni ya wanafalsafa mbalimbali kwa mfano; Aristotle, Descartes, Hegel, Collingwood, Arthur Danto, W. B. Gallie, Weigand na Barbara Hardy. Baadhi ya maoni ya Mink ni kuwa fasihi haitokani na ombwe tupu bali hutokana na mazingira halisi ya watu kama vile matamanio, maono na maisha yao. Anaendelea kusema kuwa fasihi si masuala ya kidhahania na kuwa uhalisia unatokana na historia. Isitoshe, vipindi vya kihistoria huwa na upekee. Anaeleza ya kuwa matukio ya kihistoria huwa yanakubalika na watu wengi. Mink pia anadai ya kuwa historia inahusu hifadhi ya matukio ya kweli yaliyoshuhudiwa na mambo yanayoweza kutegemewa sana. Vilevile, historia hutazamwa kama sanaa na wala si sayansi. Ufafanuzi huu wa Mink umesaidia utafiti lengwa katika kuchanganua mazingira halisi yaliyokuza uandishi wa riwaya teule. Isitoshe mtafiti amelenga kubainisha namna matukio ya kihistoria yameathiri uwasilishaji wa kazi ya fasihi. Mink alifafanua mada ya historia na

bunilizi kama mikakati ya ufahamu ilhali utafiti lengwa umechunguza athari za matukio ya kihistoria katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

Craig (1975) alichunguza sheria za kihistoria na maendeleo ya fasihi. Craig alipendekeza sheria ambazo ni za kinadharia tete na alizibuni baada ya kufanya na fasihi ya Uingereza katika karne ya kumi na sita. Alidai kuwa ukuaji wa utanzu unaenda sambamba na ukuaji wa tabaka. Craig pia alidai ya kwamba kuna uwezekano wa utanzu mpya kuchipuka kutokana na motifu, mtindo na mbinu zingine ambazo hazichukuliwi kama sanaa halisi. Vilevile, alieleza kuwa kuna uwezekano wa huo mchipuko wa utanzu kufanyika kwa ghafla na mageuzi hayo kuwa ya haraka. Craig anaendelea kusema kuwa mabadiliko katika fasihi na mabadiliko katika historia yanayolingana huenda yanahusiana sio moja kwa moja lakini kwa sababu ya kutegemea nyenzo moja katika kipindi fulani. Kwa mujibu wa Craig, fasihi hubadilika kulingana na sheria kadri miaka inavyopita. Mabadiliko haya ya kifasihi hutokea hatua kwa hatua. Utafiti wa Craig una manufaa kwa utafiti lengwa kwa kuwa, utafiti lengwa umenuia kubainisha namna mabadiliko ya kihistoria yalivyochangia katika mabadiliko ya kifasihi. Kazi ya Craig ni tofauti na utafiti lengwa kwa kuwa Craig alitafiti kuhusu sheria za kihistoria na maendeleo ya fasihi ilhali utafiti lengwa umejikita kwenye athari za matukio ya kihistoria katika riwaya.

Bennett (1978) anaeleza kuhusu historia ya zamani ya Zanzibar chini ya utawala wa Mwarabu. Vilevile anaeleza juu ya kujinyakulia uhuru kwa nchi ya Zanzibar pamoja na maendeleo yake. Bennett ameeleza kwa uwazi zaidi juu ya kupotea kwa uhuru, utawala wa Waingereza kutoka miaka ya 1890-1939. Hatimaye, kuna kuanguka kwa uongozi wa Waarabu nchini Zanzibar. Kupitia kwa kazi ya Bennett, mtafiti ameweza kuchanganua matukio ya kihistoria. Kazi ya Bennett ni tofauti na utafiti lengwa kwa kuwa utafiti wa Bennett ulishughulikia historia ya zamani ya Zanzibar, ilhali utafiti lengwa umeshughulikia athari za matukio ya kihistoria katika riwaya nchini Kenya kwa mujibu wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

Rollins (1983) anafafanua historia inayozingira maandishi ya nathari ya Kiswahili, mwanzo wake na pia aina zake tangu mwanzoni mwa miaka ya sabini. Rollins amejadili vipengee muhimu vya nathari hiyo ambavyo ni hadithi, hekaya, kioja, habari na baadaye maandishi kama vile wasifu, simo, masimulizi, neno la hekima na ngano. Aidha, anadokeza kuwa misingi ya nathari ya Kiswahili ni fasihi simulizi ya Kiswahili. Kazi ya Rollins imekuwa ya manufaa katika utafiti lengwa katika kuchanganua mtindo na lugha iliyotumiwa na waandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Kinyume na utafiti lengwa, Rollins alishughulikia historia na maendeleo ya riwaya kwa kuzingatia tanzu za fasihi simulizi ilhali utafiti lengwa umejikita katika kuchunguza athari za matukio ya kihistoria katika riwaya.

Njogu (1997) ameeleza taswira ya hali ya visiwa vya Zanzibar kwa kiasi kikubwa. Kazi hii imeshughulikia masuala ya historia kama vile mapinduzi ya kijamaa, mikinzano ya kitabaka, mfumo wa uzalishaji mali na mapinduzi ya kijamii. Alizingatia uhakiki wa riwaya za visiwani Zanzibar kama vile *Kuli* ambacho kina maswala mengi ya kihistoria. Aliegemea zaidi katika kujadili wahusika na maudhui pasi na kuyaoanisha na historia. Riwaya ya *Kuli* ni riwaya ya mapigano na mivutano kati ya watawala na watawaliwa kisiwani Zanzibar. Alitumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa lakini utafiti lengwa utatumia nadharia ya uhistoria mpya ili kuweza kubanisha kila kipengele cha utafiti lengwa kwa mujibu wa historia. Kazi hii ya Njogu itakuwa kazi mojawapo ya kimsingi katika kuyachanganua masuala mbalimbali kuhusiana na utafiti lengwa kwa kuwa aliweza kushughulikia kindani maswala ya historia ya kijamii ambayo kwa kiasi kikubwa utafiti huu umenuia kushughulikia.

Mbatiah (1998) anaonyesha namna suala la wahusika, mtindo na maudhui ya kidhanaishi yanavyojitokeza. Alibaini kuwa, wahusika hutegemeana na mazingira huwa na mchango mkubwa katika kila badiliko linalotokea kwa wahusika. Katika utafiti lengwa, mtafiti amelenga kubainisha iwapo vipindi maalum vya kihistoria huathari uwasilishaji wa maudhui, mtindo na lugha na wahusika katika kazi ya fasihi.

Kulingana na Muhammed (1988), *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* ni zao la kihistoria kuhusu visiwa vya Pemba na Unguja. Anadai kuwa, historia hiyo, hasa tukio la mapinduzi ya Januari 1964, ilizua mhemuko wa fasihi ya Kiswahili kutoka visiwani na kushutumu vitabu vilivyokosa kuangazia mapinduzi hayo. Kwa mujibu wa Mohammed, utenzi huu umesimulia chanzo cha mapinduzi ya Zanzibar. Uhakiki wa kazi hii pamoja na utenzi huu ni muhimu kwa kazi lengwa kwa sababu umelinganisha matukio ya kihistoria na kazi ya fasihi ambayo ni msingi wa utafiti lengwa.

Keesey (2003) anasema kuwa, uhakiki ambao unathaminiwa siku hizi ni uhakiki wa kihistoria. Anasema kuwa kazi yoyote ya fasihi inapaswa kuchunguzwa kwa kujikita kwenye muktadha wa mwandishi na muktadha wa utamaduni alimotungia mtunzi. Anaeleza kuwa kazi inafaa ichunguzwe kwa kurejelea mtunzi, maoni yake, itikadi yake, jamii yake, utamaduni, mambo yaliyopita na ya kisasa. Anadai ya kuwa kila kipindi cha kihistoria huzalisha fasihi ambayo huakisi uhalisia wa kipindi hicho, wakati maalum na watu maalum. Anadai ya kuwa kazi za awali zinaweza kuathiri matokeo ya kazi ya sasa na kwa hivyo kuna umuhimu wa historia katika fasihi. Utafiti wa Kessey umetufaa kujikita kwenye muktadha wa mwandishi na muktadha wa utamaduni walimotungia.

Nthenya (2007) alihakiki riwaya ya *Haini* ya Adam Shafi kama riwaya ya kihistoria. Mhakiki alitathmini vipengele vya usukaji, uhusika na wahusika. Aliitazama dhana ya usukaji kama yenye kuyamulika matukio au matendo ya historia katika jamii. Aliyaona matukio haya kuwa ndiyo hujenga historia ya jamii husika. Mtafiti alishugulikia sifa bainifu zinazoakisi uhalisia wa kihistoria wa Zanzibar. Utafiti wa Simon utakuwa wa manufaa kwa utafiti lengwa kwani utatupa mwanga zaidi katika kuchambua maudhui yanayochangiwa na mabadiliko ya kihistoria ambayo ni nguzo kuu katika utafiti huu. Kupitia utafiti wake, mtafiti amepata mwelekeo kuhusu nadharia ya uhistoria mpya, asili yake na mihimili yake. Hata hivyo, tofauti na Simon aliyetafiti kuhusu uhakiki wa *Haini* kama riwaya ya kihistoria utafiti lengwa umeangazia athari za matukio ya kihistoria katika riwaya. Utafiti lengwa pia umechanganua jinsi matukio ya kihistoria yalivyoathiri uwasilishaji wa maudhui, lugha na mtindo na jinsi wahusika wamesawiriwa katika kazi ya fasihi.

Mwirabua (2009) anaeleza kuwa bara la Afrika limepitia awamu tofauti za kihistoria katika ukuaji wake. Kulingana na Mwirabua, Bara la Afrika limepitia vipindi mbalimbali vikiwemo kipindi cha utumwa kilichotokea katika karne ya 14, kipindi cha ukoloni mkongwe cha karne ya 19, kipindi cha ukoloni mamboleo cha karne ya 20 na kipindi cha utandawazi cha karne ya 21. Utafiti wa Mwirabua uliongozwa na nadharia ya baada ya ukoloni kinyume na utafiti lengwa ulioongozwa na nadharia ya uhistoria mpya. Vilevile, kazi hii inachanganua

masuala ya kihistoria kuhusu jamii za mataifa ya ulimwengu wa tatu, utafiti huu ni tofauti na utafiti lengwa ambao umechanganua ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia, nao utafiti lengwa umetathmini athari za matukio ya kihistoria katika riwaya kwa mujibu wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008).

Nasimiyu (2013) alichunguza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Diwani ya Dhifa*. Mtafiti alibaini na kutambua kuwa siasa ya Tanzania ilichukua mkondo mpya baada ya Azimio la Arusha. Isitoshe, mazingira tofauti ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yalichangia mno katika uwasilishaji wa maudhui katika *Diwani ya Dhifa.* Utafiti wa Nasimiyu umekuwa wa manufaa kwa utafiti lengwa kwani umetoa mwanga zaidi kuhusu kuchambua maudhui kwenye riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008). Kupitia kwa utafiti wa Nasimiyu, mtafiti amepata uelewa wa nadharia ya uhistoria mpya. Mawazo ya Nasimiyu yametusaidia kupanua uelewa wa nadharia kwa kina. Utafiti wa awali unatofautiana na utafiti lengwa kwa kuwa utafiti wa awali ulihusu athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya diwani ya *Dhifa* ilhali utafiti lengwa umeangazia athari za matukio ya kihistoria katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008).

Owallah (2013) alihakiki maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa*, anasimulia kuhusu maudhui na mandhari katika *Utenzi wa Nabii Isa.* Utenzi huu ni wa

kihistoria kwa sababu mtunzi anaongelea hali halisi kuhusu dini. Mhakiki huyu ametoa mwelekeo kuhusu uhakiki wa maudhui ambayo ni kipengele teule cha uhakika lengwa wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Utafiti wa Owallah ni kinyume na utafiti lengwa kwa vile anahakiki maudhui teule huku utafiti lengwa ukiwa umechunguza athari za matukio ya kihistoria katika kukuza maudhui hayo.

Mlaga (2015), alitafiti kuhusu uhistoria katika riwaya ya Kiswahili. Katika makala yake, aliangalia kwa kina namna uhistoria unavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Makala haya yalibainisha kuwa uhistoria katika riwaya ya Kiswahili unajitokeza kwa kuegemea katika misingi mikuu ya mambo matatu; falsafa ya historia, nadharia ya uhalisia na nadharia ya uhistoria mpya. Misingi hii mitatu ndiyo inayoifanya riwaya ya Kiswahili na riwaya kwa ujumla ifae kutumika kufundisha historia. Utafiti wa Mlaga ni tofauti na utafiti lengwa kwa kuwa alijikita kwenye misingi mitatu yaani falsafa ya historia, nadharia ya uhalisi na nadharia ya uhistoria mpya ilhali utafiti lengwa umeongozwa na nadharia ya uhistoria mpya. Vilevile, utafiti wa Mlaga ulihusu riwaya za *Ndoto ya Ndaria, Gamba la Nyoka* na *Miradi Bubu ya Wazalendo* ilhali utafiti lengwa umejikita kwenye riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Utafiti wa Mlaga ametoa mwelekeo kwa utafiti lengwa kuhusu jinsi ya kubainisha maudhui yanayojitokeza katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba*.

Munyao (2017) alitafiti kuhusu mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini mwa Irara*. Alihakiki mchango wa historia katika kufumbata nia ya mwandishi wa *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini mwa Irara*, pia alizingatia kwa kina maudhui, mchango wa mandhari, na jinsi historia na fasihi zinavyoingiliana na kutegemeana. Utafiti lengwa ni tofauti na wa Munyao kwa namna mbalimbali. Kwanza utafiti huu unaangalia athari za matukio ya kihistoria katika riwaya teule ilhali utafiti wa Munyao ulizingatia mwingiliano wa fasihi na historia katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini mwa Irara*. Pili, utafiti lengwa umezingatia riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba t*ofauti na Munyao aliyetafiti kuhusu *Utenzi wa nchuu Cwavo yapo tini mwa irara*, tatu, misingi ya kinadharia ni tofauti kwani Munyao alizingatia nadharia ya uhalisia wa kijamaa huku utafiti lengwa ukiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya.

Tafiti hizi ambazo nimeziangazia, hazijazingatia kwa kina athari za matukio ya kihistoria kwa mujibu wa maudhui, mbinu za uandishi na usawiri wa wahusika katika riwaya ya Kiswahili nchini Kenya, kwa kurejelea riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Utafiti huu umechunguza athari za matukio ya kihistoria katika riwaya. Kadri mtafiti ajuavyo na kuelewa, utafiti unaofuata mkabala huu bado haujafanywa. Hii ni ithibati tosha kuwa pana pengo lililojazwa na utafiti huu.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Nadharia ya uhistoria mpya iliongoza utafiti huu. Uhistoria mpya ni aina ya nadharia ya kifasihi ambayo lengo lake ni kueleza historia kupitia fasihi na fasihi kupitia muktadha wa kitamaduni katika miaka ya 1950. Kazi za mwanzo za kihistoria zilizofahamika kama za aina ya "kitamaduni za kishairi" zilianzishwa katika miaka ya 1980 kupitia kazi za kihakiki za wanachuo wa chuo kikuu cha California. Baadaye zilipata mashiko kupitia kwa Stephen Greenblatt na zikasambaa miaka ya 1990 (TY). Nadharia ya Uhistoria Mpya ni nadharia inayochukuliwa kuwa ya kisasa na ya kimaendeleo inayofungamanishwa na kundi la wasomi walio na mwelekeo wa kilimbwende na ufufuo wa elimu na maarifa katika kazi za sanaa. Ni nadharia inayohusishwa na shule ya wahakiki wa kimarekani wanaofahamu ufaafu wa muktadha wa kazi za kifasihi. Waitifaki wa nadharia hii ni Bakhtin, Althuser, Hayden White, Roland Barthes, Jacques Derrida, Gadamer, Greenblatt na Marilyn Butler. Ni nadharia iliyokuzwa ili kuendelezwa na vilevile kuchangiwa na nadharia za hivi karibuni kama vile uchanganuzi nafsia, usomaji-mwitikio, na uana (Wamitila 2002). Ni nadharia iliyo na misingi katika mawazo ya Raymond Williams (1977) na Michel Foucault (1972). Mawazo makuu katika nadharia hii ni kuwa, matukio yote ya vielezi huegemezwa katika hali changamano ya matukio ya kikweli na kwamba matukio yote ya kufichua, kuhakiki, kukosoa na hata kupinga humalizia kuzitumia mbinu zinazozipinga. Vilevile, kuna mwingiliano wa kimzunguko kati ya kazi za kifasihi na zile zisizo za kifasihi na hamna usemi wowote wa kibunifu unaoweza

kuelekeza katika uhakika usiobadilika ama unaoelekezea hali ya kibinadamu isiyoweza kubadilishwa. Aidha, nadharia hii inafunua kwamba mtindo wa kuhakiki kwa lugha inayoakifu hutaarifu utamaduni upatikanao kwenye jamii halisi ambazo huzalisha fasihi katika mazingira na wakati maalum (Butler, 1987).

Kulingana na Greenblatt (1980), utoaji na upokezi wa kazi za fasihi huathiriwa na mahitaji ya kijamii na kisiasa. Watunzi huathiriwa na mazingira yao na athari hizi hujitokeza katika tungo zao. Utungo wa kifasihi huwa zao la ushirika fulani ambapo kipimo chake cha utamaduni, maendeleo yake ya fasihi kwa jumla kati ya mambo mengine, hushirikiana katika kuupa utungo fulani maana maalum. Wananadharia ya uhistoria wanatofautiana kwa kiasi fulani na wale wananadharia ya Ki-Maksi wanaosema kwamba fasihi na ujumisia wake huwa zao la jamii. Nao Wana–Umaksi hujishughulisha sana na suala la uchumi huku wana-uhistoria mpya wakijishughulisha zaidi na suala la usasaleo linalododadisi masuala ya utamaduni, uana na umri wa jamii, (Wamitila, 2002).

Tofauti iliyopo kati ya nadharia ya uhistoria mpya na ile ya uhistoria mkongwe ni kwenye masuala ya udumaji na utopendeleo. Wanauhistoria mpya wanajikita katika utafutaji wa mbinu mpya za kusawiri matukio ya kihistoria katika muktadha wa kisasa tofauti na kusawiri matukio kihistoria. Maelezo haya yana umuhimu katika utafiti lengwa kwani haujihusishi na kuweka maudhui yanayoibuka katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* (Chimerah, 1995) na *Mafamba* (Olali, 2008) katika

muktadha wa wakati uliopita bali ni kuyachanganua ili kuashiria ukweli tofauti kiwakati na kimaana kifasihi.

Wanauhistoria mpya wanaamini kuwa mwingiliano matini wa sasa huonekana kwa kuiangalia jamii na utamaduni wake wala hamna haja ya mhakiki wa fasihi kujikita katika kipengele fulani maalum pekee cha kazi za fasihi. Kuibuka kwa nadharia hii kulichochewa na nadharia za kiufafanuzi na za kuhakiki. Nadharia za juzi zilizoikuza, kuiendeleza na kuchangia ukuaji wa nadharia ya uhistoria mpya ni pamoja na nadharia ya mwitikio wa msomaji, uana wa upambanyaji na ile ya uchanganuzi nafsia.

### 1.8.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhistoria Mpya

1. Lengo la mwandishi wa fasihi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria, kazi ya fasihi ambayo inahakikiwa pamoja na ya jamii husika. Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* ni riwaya ambazo zimeathiriwa na maendeleo ya jamii. Maswala ya uongozi, siasa, dhuluma miongoni mwa maswala mengine yamepelekea waandishi kuandika kazi hizi za kifasihi. Mhimili huu umesaidia utafiti lengwa katika kubaini kuwa waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* wameathiriwa na maendeleo ya kihistoria yaliyokuwepo katika jamii zao hivyo walilenga kuangazia maswala mbalimbali kwenye jamii zao.
2. Kazi ya kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee yake.

Waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* wameshughulikia maswala mbalimbali ambayo si ya kubuniwa pekee ila pia ya kihalisia. Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* kwa mfano, ni riwaya iliyotungwa nyakati za siasa kali nchini Kenya na hivyo mwandishi alilazimika kutumia lugha fiche ili kufumba yale aliyokuwa ikiangazia. Aidha, riwaya ya *Mafamba* imeangazia uozo katika jamii. Uozo huo unahusu ufisadi, dhuluma, mauaji, uongozi mbaya miongoni mwa mengine. Mhimili huu umefaa utafiti lengwa kwa kuwa, bali na ubunifu, waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* wameshughulikia maswala ya kihalisia kama vile mizozo ya ardhi, vita vya uhuru, siasa, utabaka, ufisadi, elimu, na usaliti.

3. Kazi zote za kubuni huwa na muktadha wa kijamii na mahusiano yao huingiliana. Mhimili huu ni muhimu katika kuchanganua masuala ambayo waandishi walishughulikia katika riwaya teule. Maswala haya ni pamoja na uongozi mbaya, dhuluma, siasa, ufisadi, ukabila, ukoloni mkongwe, mizozo ya ardhi, usaliti na vita vya uchaguzi.
4. Kazi yoyote ya fasihi haina budi kubadilika. Mhimili huu umetusaidia kuchanganua matukio ya kihistoria na jinsi matukio hayo yalivyoathiri uwasilishaji wa maudhui, usawiri wa wahusika na mtindo na lugha katika kazi za kifasihi. Mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, kwa mfano ametumia lugha fiche ili kufanikisha kazi yake. Baada ya mwongo mmoja, riwaya ya *Mafamba* inaandikwa kwa uwazi zaidi kwa kuwa mwandishi anawasilisha

maudhui yake pasi kuyaficha sana. Huenda haya yametokana na mabadiliko kihistoria na kijamii.

5. Uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi huathiriwa na muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika. Chimbuko la riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* ni siasa, uongozi na uchumi. Mhimili huu umetufaa katika kuyachanganua maswala yaliyokuwa yakitendeka wakati wa kuandika kazi hii ya fasihi. Kwa mfano, riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* iliandikwa katika kipindi ambacho waandishi hawakuwa na uhuru wa kujieleza, hivyo mwandishi ametumia mbinu za uandishi kama vile taashira, jazanda, taswira baadhi ya mbinu nyingine ili kuweza kuwasilisha kazi yake. *Mafamba* ni riwaya ambayo iliandikwa katika kipindi kilichojawa na uozo mwingi katika jamii na misukosuko ya kiutawala. Kazi hizi *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* zinapohakikiwa, mhakiki hana budi kuhakiki kwa kurejelea yaliyokuwa yakitendeka katika jamii.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zinahusu muundo wa utafiti uliotumiwa na jinsi utafiti wote ulivyofanywa. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), mbinu ambayo hutumika ina uzito katika kuamua data itakayokusanywa na kuchanganuliwa. Sehemu hii iliangazia vipengele vifuatavyo: muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), muundo wa utafiti ni mwongozo wa utafiti. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu ni mtazamo unaodadisi sifa zinazojitokeza katika suala linalodadisiwa. Mbinu ya kimaelezo ilitumika kueleza matukio ya kihistoria nchini Kenya kwa mujibu wa vipindi vya tawala mbalimbali na athari za matukio hayo katika uwasilishaji wa maudhui, wahusika na lugha kwenye riwaya teule. Mbinu hii aidha ilitumika katika ukusanyaji, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kupitia kwa muundo huu, matukio ya kihistoria yamejadiliwa na kisha maelezo yakatolewa namna yameathiri uandishi wa riwaya teule. Kupitia kwa muundo huu matukio ya kihistoria yamezungumziwa na kisha kueleza namna yameathiri uandishi wa riwaya teule.

### 1.9.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Maktabani, mtafiti alisoma kwa kina riwaya teule za *Nyongo Mkalia Ini* (Chimerah, 1995) na *Mafamba* (Olali, 2008) na yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya uhistoria mpya na riwaya ya Kiswahili. Pia, mtafiti alidurusu makala na machapisho yaliyoandikwa kuhusu utafiiti lengwa kama vile; tasnifu, majuzuu, magazeti, vitabu na majarida. Aidha, ili kupata ufahamu zaidi wa nadharia ya uhistoria mpya, mtafiti alisoma makala na vitabu vinavyoeleza kuhusu nadharia hii. Ili kustawisha suala la utafiti na mbinu za utafiti, mtafiti pia alisoma machapisho mengine muhimu.

### 1.9.3 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli imeteuliwa kimaksudi. Mtafiti alilazimika kuteua sampuli lengwa kimaksudi ili kupata sampuli inayofaa utafiti wake. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa malengo ya sampuli lengwa hulenga sampuli maalum kwenye sampuli pana. Sababu hiyo ilimfanya mtafiti kuteua kimaksudi sampuli ambayo kwa ushahidi wake, anaamini imemfaa. Sampuli lengwa imekuwa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini (*1995) na *Mafamba* (2008). Riwaya hizi zimechaguliwa kimaksudi kwa vile zina tofauti ya zaidi ya mwongo mmoja. Katika udurusu wa mtafiti, imebainika kuwa tofauti hii ya kiwakati imeibua matukio mbalimbali katika historia ya nchi ya Kenya, na matukio haya yakaleta tofauti katika uwasilishaji kimaudhui, kidhamira, mbinu za lugha na usawiri wa wahusika. Kuna riwaya nyingi za waandishi tofauti ambazo zimeachana kiwakati lakini hazikuteuliwa kwani riwaya zilizoteuliwa zina data toshelevu ambayo imeafikiana na malengo ya utafiti huu. Data ya utafiti huu imekusanywa baada ya kusoma matini teule kwa kina ambapo mtafiti amedondoa na kunuku sehemu ambazo zina maudhui, mtindo na lugha na wahusika. Mbinu hii imemwezesha mtafiti kupata ujumbe wa kwanza ili kuonyesha namna matukio ya kihistoria yalivyoathari waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* katika kuwasilisha kazi zao.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Data ilishirikisha vifungu na sentensi ambazo zilifafanua hoja za kihistoria.

Data ilikusanywa kwa usomaji wa maktabani. Riwaya teule zilisomwa kwa kina na kisha kunukuu sehemu ambazo zina vifungu na sentensi ambazo zilifafanua hoja za kihistoria. Aidha, katika kukusanya data hii, malengo ya utafiti yalizingatiwa. Hii ni mbinu ambayo ilikidhi data ya utafiti huu.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data ilishirikisha vifungu na sentensi ambazo zilifafanua hoja za kihistoria.

Data ilipangwa kwa kuzingatia maudhui, wahusika na mtindo na lugha. Aidha, katika kuchanganua data hii, mtafiti alizingatia maudhui ya riwaya teule yaliyoibuliwa na matukio ya kihistoria, kubainisha wahusika wa kihistoria na kuonyesha mtindo na lugha uliotumiwa katika vipindi hivyo maalum vya kihistoria. Haya yalilenga kuziba pengo la utafiti ambalo ni kuonyesha athari za matukio ya kihistoria katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.* Uchanganuzi aidha ulikusudia kujibu maswali ya utafiti huu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya uhistoria mpya.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyokusanywa imewasilishwa kimaelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhistoria mpya. Njia ya kimaelezo inahusisha kutenga vifungu na kufungamanisha kimjadala. Matokeo haya yamepangwa katika sura

tano. Sura ya kwanza imehusu utangulizi wa utafiti lengwa, sura ya pili imeangazia maudhui yaliyowasilishwa katika riwaya teule, sura ya tatu imejadili wahusika katika riwaya teule, sura ya nne imeshughulikia mtindo na lugha katika riwaya teule na sura ya tano na ya mwisho imehusisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 1.9.7 Uzingatifu wa Maadili

Kabla ya mtafiti kuanza utafiti wake, aliomba kibali cha kuufanya utafiti kutoka kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta, idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kama njia moja ya kuzingatia maadili ya utafiti. Utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia maadili ya utafiti ambayo hupendekeza uwazi na uaminifu. Utafiti alijiepusha na wizi wa mawazo ya waandishi wa hapo awali. Mligo (2012) anasema kuwa upo wizi wa kitaaluma unaohusisha wizi wa mawazo, maneno au vifungu vya maneno ya watafiti wengine. Ili kujiepusha na aina yoyote ya wizi, utafiti huu umetambua mchango wa waandishi na wataalam wa awali kwa kuwanukuu.

## 1.10 Hitimisho

Masuala ambayo yalijadiliwa katika sura hii yanahusu msingi wa utafiti. Yanahusu utangulizi wa sura, usuli wa mada, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Vilevile, sura hii ilijishughulisha na yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti lengwa pamoja na msingi wa nadharia. Isitoshe, iliangazia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika kufanikisha utafiti huu.

Sura inayofuata inashughulikia athari za matukio ya kihistoria katika kuwasilisha maudhui kwenye riwaya teule. Katika sura ya pili, mtafiti alichanganua uwasilishaji wa maudhui katika riwaya ya kihistoria.

## SURA YA PILI

## ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA KUWASILISHA MAUDHUI KATIKA RIWAYA TEULE

### 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, mtafiti ameangazia suala la utafiti kwa kina. Hali kadhalika, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia na yaliyoandikwa kuhusu mada yamejadiliwa. Aidha, sehemu hiyo imeangazia mada na upeo wa utafiti. Lengo la kwanza lilikuwa ni kubainisha jinsi matukio ya kihistoria huathiri jinsi waandishi wanavyowasilisha maudhui kwenye riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

Katika sura hii, mtafiti ameangazia maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ya Rocha Chimerah na *Mafamba* (2008) ya Tom Olali. Mtafiti amefanya hivi akiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya inayoeleza kuwa kuna uhusiano baina ya kazi ya kifasihi na historia. Nadharia hii imetuwezesha kubaini ikiwa matukio ya kihistoria yamewaathiri Rocha Chimerah na Tom Olali katika uwasilishaji wa maudhui yanayojitokeza katika riwaya teule.

### 2.1 Dhana ya Vipindi vya Kihistoria

Kapiyo (2011) anasema ya kwamba, tukio la kihistoria ni jambo muhimu lililofanyika wakati uliopita. Kipindi cha kihistoria hurejelea nyakati tofauti tofauti katika historia ya nchi fulani kwa mfano, Kenya. Kwa msingi wa utafiti huu,

nyakati zinazorejelewa ni wakati wa ukoloni, wakati wa utawala wa rais wa kwanza wa nchi ya Kenya, Rais Kenyatta, wakati wa utawala wa rais wa pili wa nchi ya Kenya, Rais Moi na wakati wa utawala wa rais wa tatu wa nchi ya Kenya, Rais Kibaki. Katika vipindi vya Rais Kenyatta na Rais Moi, waandishi wengi hawangeandika maudhui yao moja kwa moja kwa kuhofia kutiwa ndani kwa visingizio vya kuchochea raia dhidi ya serikali. Ni hali hii ndiyo iliyowaelekeza waandishi wengi kutumia mitindo ya kijazanda ili wasitiwe ndani. Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ni riwaya inayoangazia maswala ya kihalisia. Maswala haya yanahusisha uhusiano baina ya vijana na wazee, viongozi na watawaliwa, wasomi na wasiokuwa wasomi na matajiri na wachochole. Kupitia kwa mahusiano yao, maudhui ya mizozo ya ardhi, ukombozi, siasa, elimu na utabaka yanajitokeza.

## 2.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Maudhui katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995)

Sehemu hii imeangazia maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini.* Mtafiti amefanya hivi ili kubaini ni kwa kiasi kipi mtunzi wa riwaya hii alivyoathiriwa na matukio ya kihistoria katika uwasilishaji wake wa maudhui. Maudhui yaliyoangaziwa ni kama vile: mizozo ya ardhi, siasa, elimu, vita vya uhuru na utabaka.

### 2.2.1 Maudhui ya Vita vya Uhuru

Vita ni makabiliano baina ya nchi, vikundi vya watu au hata mataifa kwa kutumia silaha. Kupitia mhusika Mumanyi, mwandishi wa *Nyongo Mkalia Ini* anatusawiria maudhui ya vita. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Mimi hupenda kusema ukweli; na sasa nasema kweli… Wallahi nilikuwa nikidhani ni sanamu za wapiganiaji uhuru wa Maji Maji! Kumbe ni watu waliojitoa mhanga kuulinda utawala wa Mwingereza… Aah, nishafahamu sasa.’' (Uk. 36).

Maneno haya ya Mumanyi yanoonyesha jinsi ambavyo sanamu za wakoloni ziliondolewa baada ya Waafrika kujinyakulia uhuru. Anajiuliza ni kwa nini sanamu za waliopigania uhuru hazijachongwa baada ya kuondolewa kwa sanamu za mkoloni.

Aidha, kupitia kwa maelezo ya mama Mumbe tunapata maelezo kuhusu vita vya Maji Maji (Uk. 58-63). Mapigano haya yalipiganwa msituni. Katika mapigano hayo, Mama Mumbe anaeleza kuwa alikuwa akimpelekea bwanake chakula msituni. Aidha, anaeleza kuwa waja waliotuhumiwa kushirikiana na Maji Maji waliuawa. Aidha, mashujaa wa Maji Maji waliposhuku kuwa kuna mtu alishirikiana na serikali walimuangamiza. Ni kutokana na haya, baadhi ya watu waliofanya kazi katika reli waliuawa. Hali kadhalika, anataja kuwa baadhi ya Waafrika walikula viapo.

Kwa upande mwingine, mwandishi anatueleza kuhusu maana ya Maji Maji. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Kwani maana ya Maji Maji ni nini? Munga aliuliza.
> Mzungu ajitenge, Mchovya ajitawale! Alidakia Omari.’’(Uk. 66).

Maneno haya ya Omari yanatubainishia jinsi katika eneo hilo wanajamii walidhani kuwa watu wa jamii ya Wachovya ndio waliopigania uhuru. Hata hivyo, inabainika kuwa sio tu Wachovya waliopigania uhuru bali Afrika nzima. Mwandishi anataja kuwa hata mtawala wa Misri, Abdel Gamar Nasir aliwasaidia Wachovya kupigania uhuru. Anaeleza zaidi kuwa wengi hufikiri kuwa Wachovya walipigania uhuru kwa sababu baba Mwanzilishi wa nchi alikuwa ni Mchovya. Hali kadhalika, mwandishi anataja baadhi ya watu walioshikwa pamoja na Baba Mwanzilishi ambao sio Wachovya ikiwemo Chieng’o Radingo wa Ziwakuli, Sauli Ngovi wa Ukavuni na Kwecho.

Hata hivyo, mwandishi anatumia maneno ‘vita vya Maji Maji’ kuashiria ‘vita vya Mau Mau’. Vita vya Mau Mau vilifanyika nchini Kenya. Baba Mwanzilishi anayetajwa hapa alikuwa ni Jomo Kenyatta anayetoka katika jamii ya Wakikuyu. Kutokana na Kenyatta kuwa Rais wa kwanza, watu wa jamii yake wamechukulia kuwa ni wao ndio waliopigania uhuru. Aidha, kihistoria Kenyatta alipokuwa Rais wa Kenya aliwapa watu wengi wa jamii yake nafasi za uongozi. Jambo hili liliwafanya Wakenya wengi kuhisi kuwa utawala wa Mwingereza ulibadilishwa na ukawa utawala wa jamii yake. Isitoshe, Klopp (2001) anaeleza kuwa wakoloni waliibua propaganda kuwa jamii ya Wakikuyu sio watu waaminifu. Kutokana na jambo hili, jamii mbalimbali nchini Kenya zimekosa kuwaamini Wakikuyu.

Mwandishi anatumia neno ‘Wachovya’ kijazanda kuashiria jamii ya ‘Wakikuyu’ iliyokuw imeshikilia uongozi wa takriban taasisi zote na kupewa mashamba katika sehemu nyingi nchini. Hali kadhalika, mwandishi anawataja wanajamii wengine walioshikwa na baba Mwanzilishi ambao sio wa jamii ya Wachovya ikiwemo Chieng’o Radingo wa Ziwakuli na Sauli Ngovi wa Ukavuni na Kwecho. Wahusika hawa wanasimamia watu walioshikwa pamoja na Kenyatta ambao sio wa jamii ya Kikuyu yaani Achieng Oneko kutoka jamii ya Waluo na Paul Ngei kutoka jamii ya Wakamba. Isitoshe, inabainika kuwa Abdel Gamar Nasir aliwasaidia mashujaa wa Mau Mau katika vita vyao. Aidha, stesheni ya Misri iitwayo “Voice of Afrika” iliwaunga mkono wapiganaji wa Mau Mau.

Hali kadhalika, vita vya Mau Mau vilipiganiwa msituni. Akina mama walitumiwa kuwapelekea mashujaa hao vyakula. Aidha, mashujaa hao walikula viapo na walioshukiwa kuwa wasaliti waliuawa.

Imebainika kuwa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* imejadili athari za matukio ya kihistoria kwa njia ambayo si wazi kwani ametumia majina kama vile Mumbe, Wachovya na Maji Maji ili kuficha matukio yake. Hali hii inaoana na maelezo ya Wamitila (2003) kuwa, tukiangazia nadharia ya uhistoria mpya, matukio ya kihistoria siyo lazima yaonekane wazi. Aidha, Mlaga (2015), anamuunga mkono Wamitila (2003), kwa kueleza kuwa fasihi inabeba umaizi wa juu ya uumbaji wa vipindi vya kihistoria. Kwa msingi huu, mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia*

*Ini* ana utambuzi wa kipindi ambacho vita vya Mau Mau vilipiganwa nchini Kenya. Mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi ulifaa utafiti lengwa katika kuyachanganua maudhui ya vita vya ukombozi.

### 2.2.2 Maudhui ya Mizozo ya Ardhi

Mzozo wa ardhi ni jambo ambalo limeathiri bara la Afrika. Kwa mujibu wa Ndungu (2005), katika kipindi cha utawala cha Rais Moi, kulikuwa na njia kadhaa ambazo zilitumika kunyakua ardhi. Barua na stakabadhi zisizo halali zilitumika katika kugawa ardhi na rekodi katika wizara ya ardhi na makao kuharibiwa makusudi (TY). Ni kutokana na hali hii, ndipo kazi mbalimbali zinaangazia maudhui yanayohusu mvutano baina ya watu kwa sababu ya ardhi. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, mwandishi anasawiri maudhui ya mzozo wa ardhi. Mwandishi anaeleza kuhusu namna serikali ilivyogawanya mashamba baina ya Waafrika baada ya uhuru. Kugawanya huku kuliibua migogoro baina ya makabila mbalimbali ya Kiafrika. Aidha, Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Aliamka siku moja akasema sehemu ile yote tuliyokuwa tukikaa na kulima ataizungusha waya. Ati kwa nini? Kwa kuwa amepata fununu kwamba serikali imeanzisha mpango wa ugawaji wa mashamba’’. (Uk. 21).

Mfano huu unabainisha jinsi mhusika Mumanyi alivyofukuzwa mahali walimokuwa wakiishi. Babake Mumanyi anafanya kosa la kujitengea sehemu ya ardhi. Hali hii inamfanya kuitwa kikaoni ili kujitetea mbele ya baraza. Kulingana na wakazi wa eneo hilo, ardhi ilikuwa ya jamii na sio ya mtu binafsi. Baadaye,

mzozo unaibuka kati ya babake Mumanyi na wanakijiji. Baadaye, wanafurushwa kwao. Mzozo huu unatokana kwa sababu kuwa wanakijiji hawataki kukubali njia mpya ya umiliki wa ardhi. Kupitia mhusika huyu, mwandishi anasawiri matukio ya kihistoria. Katika nchi mbalimbali za Kiafrika, mashamba yalimilikiwa na jamii mbalimbali na sio mtu binafsi. Ndiposa, Boone (2011) na Okoth-Ogendo (1989) wanakubaliana kuwa baada ya Kenya kupata uhuru umiliki wa ardhi ulibadilika kutoka kwa asasi za kijamii hadi kumilikiwa na mtu binafsi. Aidha, mwandishi anatueleza kuhusu namna wahusika mbalimbali walivyopelekwa katika maeneo tofauti ili kupewa mashamba na serikali, Jambo hili liliibua migogoro baina yao na wenyeji wa maeneo hayo. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Sasa serikali ilifanya makosa kutupeleka huko, sio? Haikufanya makosa, lakini iliwabidi mfahamu ya kuwa pale pana wenyeji. Ada ya mgeni akienda ugenini hushikana na wale wenyeji akawaomba wampe pahali pale akae.’’ (Uk. 20).

Kutokana na haya, inabainika jinsi mhusika huyu kwa jina Omari alivyohamishwa hadi eneo lingine. Omari anawalaumu wenyeji wa Uziwani kwa kuwafukuza baada ya kupewa shamba na serikali. Hata hivyo, jambo ambalo hafahamu ni kuwa, shamba hilo alilopewa ni la wenyeji wa Uziwani. Tukio hili la watu kupewa mashamba na serikali kwingine ni la kihistoria. Nchini Kenya ugawaji wa mashamba ulifanywa na serikali kuu (Boone, 2012).

Ugawaji huu uliibua migogoro baina ya wanakijiji. Aidha, Griener (2013) na Onoma (2010) wanakubaliana kuwa wakati utawala wa Rais Kenyatta na Rais Moi mashamba yalipeanwa ili kuendeleza uhusiano wa kisiasa. Aidha, Klopp (2001)

anaeleza kuwa ugawaji wa mashamba wakati wa utawala wa Kenyatta ulifaidi tu jamaa zake. Hali hii inaweza kumuafiki mhusika Omari ambaye pengine kabila lao lilipewa mashamba katika eneo la Uziwani bila hata kuwazia wenyeji wa eneo hilo ili kuendeleza uhusiano wa kisiasa na kiongozi wa nchi hiyo.

Aidha, Rocha Chimerah mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, anataja eneo la Gongwa katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Katika mashairi ya Muyaka (*1870)* yaliyomo katika kitabu cha Abdulaziz (1979), Muyaka anatumia neno 'Gongwa' kurejelea Mombasa. Inawezekana kuwa matukio yanayoelezewa na Chimerah yalitokea Mombasa. Aidha, katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* wageni waliitwa 'Wanyika' na wenyeji wa eneo hilo ambao ni Waarabu na Waswahili (Uk. 25). Kutokana na haya, inabainika kuwa mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa mwandishi wa fasihi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria una mashiko. Kwani Rocha Chimerah ameathiriwa na matukio ya kihistoria nchini Kenya.

### 2.2.3 Maudhui ya Siasa

Kwa mujibu wa Omary (2011), siasa ni sanaa ya kuongoza na kutawala nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali. Aidha, Adero (2005) anaelezea kuwa siasa hujihusisha na mitafaruku ya kijumla na njia ya kusuluhisha mizozo hiyo. Kyle (1999) anasema kuwa siasa ya kipindi cha kabla ya uhuru ziliwapa wakoloni wakati mugumu wa kuchagua kiongozi ambaye angelinda maslahi ya baada ya kuondoka

nchini. Aidha, Orwa (1992) anasema ya kuwa nchi ya Kenya ilirithi kutoka uingereza mfumo wa kisiasa, kiuchumi miongoni mwa mengine. (TY).Vilevile, Mahoney (2010) anaendelea kusema kuwa, baada ya kifo cha Rais Kenyatta, aliyekuwa naibu wake alirithi mfumo wa utawala uliokuwepo. Kijumla, siasa ni mbinu ambayo watawala na watawaliwa hutumia ili kusuluhisha matatizo yao. Mbinu ya kusuluhisha matatizo yao huweza kutegemea utawala uliopo. Ikiwa utawala ni wa kidikteta basi mbinu huwa tofauti na mbinu inayotimiwa katika utawala wa kidemokrasia.

Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, maudhui ya kisiasa yamesawiriwa. Mwandishi anatueleza kuhusu mauaji ya kisiasa, mikataba mbalimbali ya kisiasa na watu mbalimbali kushikwa kwa sababu ya kutofautiana kimaoni na viongozi. Mifano ni Abdallah, Muyaka bin Hajji na Socrates waliodhulumiwa kwa sababu ya kutofautiana na viongozi. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Baada ya karne mbili hivi, kijana Abdallah Mkilindi akakariri swala hilo hilo la wavyele wake. Wenye uwezo hawakusita kumfungia chumba cha giza…. Huko akatueleza maoni yake kuhusu kule tuendako, na vile tutakavyoishia mambo yasiposhika mkondo mwongofu. Alitueleza katika mashairi kadhaa aliyoyakusanya na kuyachapisha katika kitabu kizuri sana kilichompendeza kila msomaji. Muhimu sana kilishinda tuzo la Rais la uandishi bora.’’ (Uk. 89).

Mfano huu unaonyesha jinsi Abdallah alivyoshikwa na kuwekwa gerezani kwa sababu ya kutofautiana kimawazo na watawala wa nchi. Baadaye, anaandika mashairi. Mashairi haya yanamfanya kushinda tuzo.

Mwandishi anasawiria matukio halisi ya kihistoria. Kihistoria mwandishi Abdilatif Abdalla (aliyezaliwa mwaka wa 1946) alishikwa na kuwekwa gerezani kutoka mwaka wa 1969 hadi mwaka wa 1972. Aliwekwa gereza la Kamiti na baadaye kupelekwa katika gereza la Shimo la Tewa. Isitoshe, Abdalla alishikwa kwa sababu ya kuunga mkono chama cha KPU na kuandika makala iitwayo *Kenya Twenda Wapi*. Chama cha KPU kilikuwa kinapinga utawala wa Kenyatta. Aidha, makala ya *Kenya Twenda Wapi* ilipigania usawa na haki na kupinga utawala wa kidikteta wa rais Jomo Kenyatta. Hata hivyo, akiwa gerezani aliandika Diwani ya *Sauti ya Dhiki* iliyochapishwa mwaka 1973. Diwani yake ilishinda tuzo la "Jomo Kenyatta Prize for Literature". Isitoshe, WaKinyatti (2008) anaeleza kuwa wakati wa utawala wa Rais Kenyatta, mtu yeyote aliyepinga utawala wake alishikwa na kuwekwa gerezani bila kupewa nafasi ya kujitetea. Hali hii inaweza kubainisha sababu ya Abdilatif kuwekwa gerezani.

Kutokana na haya, inabainika kuwa matukio haya ya kihistoria ni ya wakati wa utawala wa Kenyatta. Ndiposa, fasihi hujikita katika matukio muhimu ya kihistoria kwa kuwa hujaribu kuweka uasili wa kazi za kifasihi katika kipindi fulani cha kihistoria. Kwa msingi huu basi, mwandishi ameweka matukio yake katika kipindi cha utawala wa Kenyatta.

Isitoshe, katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* mwandishi anatueleza kuhusu mkataba baina ya Sultan na viongozi wa Uingereza. Mkataba huu ulifanywa ili

kuwawezesha Waingereza kutawala vizuri. Aidha, Sultan aliweza kuwagawia Wahindi na Waarabu mashamba. Mwandishi anatueleza hivi:

> ‘‘Na Mwingereza anataka kuhifadhi heshima yake machoni mwa watu wa nje. Hataki kulaumiwa alimpindua Sultan. Kwa hivyo akaona jambo la kufanya ni kumwachia uwezo kiasi tu, apewe heshima na raia zake. Waarabu wadanganyike kuwa Sultani wao anawatawala kumbe Sultani mwenyewe ni kibaraka wa Mwingereza.’’ (Uk. 74).

Mfano huu unathibitisha jinsi Mwingereza alivyotumia akili ili kuwatawala wananchi. Kupitia mkataba wa viongozi wa Uingereza na Sultan, Waingereza wanafaulu kuwatawala wenyeji. Jambo hili analolizungumzia mwandishi ni tukio la historia. Mnamo 1895 Waingereza walikuwa na mkataba na Sultan wa Zanzibar kuhusu eneo la pwani. Mkataba huu uliwafaidi wachache tu ikiwemo Wahindi na Waarabu. Hata hivyo, wenyeji wa pwani walinyanganywa mashamba.

Isitoshe, mwandishi anataja baadhi ya watu mbalimbali waliokuwa wakati wa utawala wa Kenyatta ikiwemo Prince Philip, Duke of Edinburgh na Rowland Vidzo (Ronald Ngala). (Uk 2). Mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee yake ulifaa utafiti huu kwa kuwa mwandishi ameangazia maswala halisi kama vile mauaji ya kisiasa, watu kushikwa na kuwekwa gerezani na mkataba baina ya Sultan na viongozi wa Uingereza.

### 2.2.4 Maudhui ya Elimu

Elimu ni nyenzo ya kupitisha maarifa na ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hapo awali wanajamii waliwaelimisha wana wao. Hata hivyo, baada ya kuja kwa wakoloni mfumo wa elimu ulibadilishwa. Mfumo huu ulikumbwa upinzani kutoka kwa wenyeji. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, mwandishi anatueleza kuhusu namna wanajamii walivyokataa kuenda shuleni. Anataja sababu kuwa ni mila na dini. Anaeleza hivi:

> "Elimu hii ya kizungu ilianzia hapa uziwani; lakini watu hawakuijali hadi sasa ndio twaanza kukubali kwa wingi. Sitakwambia sababu zake. Labda ni mitafuruku wa dini na mila sijui. Hivyo ni lazima ufahamu kuwa sehemu nyingine za huku Uziwani kwetu ziko nyuma sana kielimu. Mojawapo ni Kijiji hiki … " (Uk. 5).

Maneno haya ya Mumanyi yanabainisha wazi kuwa watu wengi walikataa kusoma kwa sababu ya mila na tamaduni. Mumanyi anaeleza kuwa Omari ndiye aliyekubali kusoma. Aidha, anaongezea kuwa waja wa eneo hilo wameanza kukubali masomo. Kutokana na maelezo ya Mumanyi, inabainika kuwa anazungumzia tukio la Waingereza kwenda eneo hilo. Mwandishi anasawiri tukio la kihistoria japo hataji moja kwa moja. Kihistoria, Wamishenari walifika eneo la pwani kwanza kabla ya kuenda maeneo mengine nchini Kenya. Hata hivyo, Wapwani wengi walikuwa wa dini ya Kiislamu na hivyo walikataa kufunzwa na Waingereza kwa sababu Waingereza ni Wakristo.

Isitoshe, katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, mwandishi anatueleza kuhusu migomo na maandamano katika vyuo vikuu. Kupitia barua ya Tom Munga kwa

Mumanyi anatueleza kuwa fujo zimeanza tena katika chuo kikuu cha Zutafindukani na hii ni sababu ya ukabila. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Fujo zimeanza tena. Na hivyo pepo zivumavyo naona hatuna salama ila kufukuzwa tena hivi karibuni. Moto wa ukabila umeteketeza siasa za Zutafindakani na kudunisha maendeleo. Nafikiri siasa ya mkoloni ‘gawa-utawale’ yachunguliachungulia tena’’. (Uk. 15).

Barua hii ya Munga inathibitisha kuwa kulikuwa na ukabila chuoni Zutafindakani ambapo ukabila huu ulisababishwa na siasa ya wakati huo. Aidha, anaeleza kuwa wako tayari kumwaga damu ili kuwafyeka vibaraka, Japo mwandishi anatumia Chuo Kikuu cha Zutafindakani anatueleza matukio halisi nchini Kenya. Kenya ilishuhudia migomo mingi vyuoni mnamo mwaka wa 1970 hadi 1979 (K’okul, 2010). Migomo hii iliathiri masomo vyuo vingi ikiwemo Chuo Kikuu cha Egerton, Kenyatta na Nairobi. Nkinyangi (1981) na Standa (2000) wanakubaliana kuwa mnamo mwaka wa 1970 hadi 1979 migomo mingi ya vyuo vikuu ilisababishwa na mauaji ya kisiasa yaliyokuwa yakitendeka (mifano ni Ronald Ngala na J. M. Kariuki) na ukabila. Kwa mujibu wa Hornsby (2012), anasema kuwa mnamo Disemba mwaka wa 1972, Nchi ya Kenya ilipoteza mwanasiasa mwingine maarufu. Ronald Ngala alipata ajali mbaya ya barabarani na baada ya wiki mbili akaaga dunia. Kulikuwa na uvumi kuwa kifo chake kilikuwa kimepangwa. (T.Y). Hornsby (2012) anaendelea kusema kuwa baada ya miaka mitatu, gari la J.M Kariuki lilikuwa limepigwa bunduki kadhaa na ya kuwa kulikuwa na jaribio la kumuua. Mnamo mwaka wa 1975 mwezi wa Machi maafisa kutoka kwenye kitengo cha G.S.U walimshika nje ya hoteli ya Hilton na kumpeleka mahali

pasipojulikana. Siku iliyofuata wachungaji kutoka kwa jamii ya Kimasai waliipata maiti yake ikiwa imetupwa karibu na milima ya Ngong. Baadaye wananchi na wanafunzi wa vyuoo vikuu waligoma kufuatia kifo hiki. Kwa msingi huu, inawezekana kuwa mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ameandika kuhusu mgomo wa Chuo Kikuu kimoja nchini Kenya uliotokea wakati huo.

Aidha, mwandishi anatuthibitishia kuwa ukabila uliathiri sio tu vyuo vikuu bali pia shule za upili na msingi. Anatueleza kuhusu kisa kimoja katika shule ya upili ya St. Bwanga. Katika shule hiyo, wanafunzi waligawanywa kwa msingi wa kikabila. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Hapa kidogo haijambo, lakini Tangana- si wafahamu nilikuwa nasomea shule ya St. Bwanga? Huko kulikuwa na mgawanyiko mkubwa. Wanailo walikuwa wengi. Palikuwa na walimu kadhaa wa kinailo ambao walituhimiza tujivunie unailo wetu. Walipenda sana kuwadharau walimu wengine na aidha wanafunzi wa makabila mengine.’’ (Uk. 85).

Mfano huu unabainisha jinsi ukabila ulivyoathiri shule ya St. Bwanga. Mwandishi anaeleza kuwa walimu na wanafunzi wa kinailo waliwadharau wenzao. Hii ni kwa sababu walikuwa wakitoka katika makabila tofauti nao.Kazi ya kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee yake. Mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ameshughulikia changamoto zilizokumba elimu nchi Kenya katika kipindi cha wakati alipoiandika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Changamoto hizo zikiwa migomo, mauaji na ukabila.

### 2.2.5 Maudhui ya Utabaka

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011), tabaka ni kundi la watu katika jamii linalojitofautisha na kundi jingine kwa misingi mbalimbali kama vile; kiuchumi na kielimu. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, mwandishi anatueleza kuhusu namna jamii imejigawanya katika matabaka mbalimbali. Mwandishi anaeleza hivi:

> ''Sisi sote ni nyuki. Kama nyuki tumegawanyika matabaka matabaka. Kama nyuki, wapo wanaochuma asali na wanaokula asali…''(Uk. 46).

Maelezo haya ya mhusika Mumanyi yanabainisha jinsi utabaka ulivyoathiri jamii. Akitumia mfano wa nyuki na asali, anatuonyesha kuwa katika jamii kuna wale wanaofanya kazi kwa bidii ilhali kuna wengine ambao kazi yao ni kujifaidisha kutokana na bidii yao. Aidha, katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* watu wa tabaka la juu wanawanyanyasa watu wa tabaka la chini. Wanafanya hivi kwa kuwapokonya mashamba. Mwandishi anaeleza hivi:

> ''Wale WENYE- nchi mabwana mashamba wengi wa kigeni ambao hata hawakai mashambani mwao… hufanya kuagizia tu. Watu hawa walinyakua maeneo makubwa ya ardhi hapa Uziwani toka enzi za ukoloni. Kisha bado watu wa Uziwani wanaokaa katika ardhi yao wanachukuliwa kuwa wapangaji. Makwetu.'' (Uk. 78).

Maelezo haya kutoka barua aliyoandika Dzuya yanabainisha jinsi watu wa tabaka la juu walivyowanyanyasa watu wa tabaka la chini. Anatueleza kuwa tangu enzi za ukoloni watu wa Uziwani wamekuwa kama wapangaji. Tangu wanyang'anywe mashamba wamekuwa hohe hahe. Aidha, anataja kuwa Baba Mwanzilishi

alipigania uhuru lakini haonyeshi mfano mwema. Kila wanapopigania mashamba yao wanaambiwa watoe Hati Miliki.

Hata hivyo, jambo analolizungumzia mwandishi kuhusu kunyang'anywa mashamba na watu wa tabaka la juu ni la kihistoria. Inabainika kuwa kihistoria watu wa eneo la Pwani walinyang'anywa mashamba na wakoloni. Aidha, Baba Mwanzilishi hapa ni rais wa kwanza nchini Kenya, Rais Kenyatta. Isitoshe, wenyeji wa pwani wengi hawana hati ya hatimiliki.

Masuala haya yanathibitishwa na Kanyinga (1998) anapoeleza kuwa mkataba kati ya Sultan na viongozi wa Uingereza uliwapa waja waliohusiana na Sultan mashamba katika mwambao wa pwani huku wenyeji wakiachwa bila mashamba. Aidha, Kanyinga (1998) anaongezea kuwa miaka ya 1970-1978 serikali ya Kenya ilitambua umiliki wa kibinafsi wa ardhi bila kujali jinsi watu walivyopata mali hiyo.

Aidha, Branch (2011) anaongezea mawazo ya Kanyinga (1998) kwa kueleza kuwa, Rais Jomo Kenyatta aliwapa wakoloni haki ya kumiliki mashamba nchini Kenya na wale waliotaka kutoka nchini Kenya wangepewa fidia. Hali hii yaweza kubainisha kuwa mwandishi wa *Nyongo Mkalia Ini* ana uelewa wa historia kuhusu jinsi tabaka la juu lilivyonyakua mashamba ya wenyeji. Ndiposa, anataja masuala ya hati miliki shamba kugawanywa na serikali na Baba Mwanzilishi kutowatetea.

Kwa kufanya hivi, fasihi imetumiwa kama nyenzo ya kusawiri historia (Mlaga, 2015).

## 2.3 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Maudhui kwenye Riwaya ya *Mafamba* (2008)

Katika sehemu hii, mtafiti amejadili maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Mafamba* (2008). Mtafiti amefanya hivi ili kubaini ikiwa mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ameathiriwa na historia katika uwasilishaji wake wa maudhui. Maudhui yaliyoangaziwa ni kama vile: ufisadi, siasa, vita vya uchaguzi, ukombozi, elimu na usaliti.

Riwaya ya *Mafamba* **(**Olali, 2008), ni riwaya inayoangazia tawala mbalimbali katika sayari ya NUKA iliyoongozwa na Maotad. Wananchi wa sayari ya NUKA waliitwa wana Bikerani-Msiige. Sayari hii ilishuhudia miungano ya kisiasa. Katika hadithi, Uongozi wa Maotad uliendeleza maovu ambayo yanarejelewa kama mafamba. Viongozi mbalimbali katika riwaya wanaungana ili kuondoa mafamba.
Katika sehemu hii, mtafiti amejadili maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Mafamba* (2008).

### 2.3.1 Maudhui ya Ufisadi

Kulingana na Kimeu (2016), ufisadi hurejelea matumizi ya mamlaka ili kunufaika au kufaidi kundi fulani la watu. Aidha, Njoroge (2014) anaelezea ufisadi kama

nyendo za uovu ikiwemo kutumia madaraka ili kujifaidisha. Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa ufisadi ni maovu yanayotendwa na mtu ili kujifaidisha au kuwafaidisha makundi fulani ya watu ikiwemo kupeana rushwa na kutumia rasilimali ya serikali vibaya.

Katika riwaya ya *Mafamba*, maudhui ya ufisadi yamesheheni. Mwandishi anatueleza kuhusu sakata mbalimbali ikiwemo sakata ya mfuko wa vito na *Anglolasting.* Sakata hizi ziliwafaidisha baadhi ya viongozi huku wananchi wakiteseka. Kupitia hadithi yake Mzee Twajua, tunaelezwa kuwa Engineer alikuwa mfisadi sana. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Unamaanisha kuwa bidhaa hutanunua lakini utazinunua. Mimi nitakupa chako nawe unipe changu. Huo ndio ujenzi wa Karifa.’’ (Uk. 207).

Mfano huu unabainisha jinsi ufisadi ulivyoendelezwa na wanachama wa Bora ikiwemo Engineer. Engineer anamlipa mtu pesa aandike cheti kuonyesha vifaa kama vile tarakilishi mia saba, magari, kemikali na pasipoti za kielektroniki shilingi bilioni 666 ilhali ni bilioni 66. Aidha, hanunui vifaa hivyo bali anataka cheti pekee. Pesa hizo anazitumia kwa maslahi yake tu. Kutokana na haya, inabainika kuwa mzee mmoja aitwaye Jogi anajiuzulu na kuguria sayari nyingine akihofia maisha yake. Hii ni kwa sababu alikuwa anajua kuhusu sakata ya Anglolasting.

Isitoshe, mwandishi anatueleza kuwa ufisadi ulikuwa umesambaa kote kiasi cha kuchapishwa magazetini kila siku. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘OVER 2,000 FIRMS IN BRIBES SCAM
> Companies paid $1.8 bn to SAHU regime under the oil- food for food deal. ” (Uk. 211).

Kichwa hiki cha gazeti moja kilionyesha jinsi utawala wa BORA ulivyokuwa. Kampuni elfu mbili zilikumbwa na sakata ya ufisadi. Aidha, mwandishi anaeleza kuwa sakata hii ya *Anglolasting* inamkumbusha sakata ya mfuko wa vito iliyokuwa wakati wa utawala wa NUKA. Isitoshe, anaeleza kuwa hakuna yeyote aliyeshikwa katika sakata hizo mbili.

Imebainika kuwa mwandishi anazungumzia tukio la kihistoria kuhusu namna ufisadi ulivyoathiri Kenya. Ndonga na Carranza (2019) wanaeleza kuwa, wakati wa enzi ya utawala wa rais wa tatu nchini Kenya, Rais Mwai Kibaki viwango vya ufisadi viliongezeka ikiwemo kashfa ya *angloleasing*. Aidha, Ndonga na Carranza (2019) wanaongezea kuwa wakati huo pia kulikuwa na kashfa ya Goldenberg iliyowahusisha viongozi waliokuwa katika serikali ya Rais Daniel Arap Moi. Licha ya tume mbalimbali kubuniwa ili kuchunguza kashfa hizi hakuna aliyehukumiwa. Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* anatuelezea matukio haya lakini anatumia majina tofauti. Majina kama vile Jogi kuashiria mheshimiwa John Githongo, NUKA kuashiria chama cha KANU, mfuko wa vito kuashiria Goldenberg na Anglolasting kuashiria *angloleasing*. Aidha, anaeleza kuwa sakata ya Anglolasting ilitokea wakati serikali ilihitaji pasipoti za kielektroniki. Mhimili

wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee yake una mashiko kwa kuwa, maswala yalioangaziwa na mwandishi Tom Olali ni ya kihalisia na yalitokea katika jamii yake katika kipindi cha kiwakati alipoiandika riwaya ya *Mafamba*.

### 2.3.2 Maudhui ya Siasa

Maudhui ya siasa yanajitokeza katika riwaya ya *Mafamba*. Katika riwaya hii, mwandishi anatuonyesha mbinu mbalimbali ambazo wanasiasa hutumia kushinda uchaguzi. Mbinu hizi ni kama vile: kuwaua wapinzani, kuungana kwa vyama tofauti, propaganda, ahadi za uwongo na pia kuwapa wananchi pesa ili wawachague. Mwandishi anatueleza kuhusu muungano wa wanasiasa waliojitoa katika sayari ya NUKA na sayari nyinginezo. Anaeleza kuhusu muungano wa viongozi wa sayari za DiPieNi, PiDi, KEFO na viongozi wengine ili kushinda chama cha NUKA. Viongozi wa vyama hivi walikuwa ni: Amrao, LiMioe na Boyi. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Karatasi hii inasema hivi;
> KINARA WA SAYARI YA NUKA: LiMioe
> NAIBU WA KINARA: Boyi
> MSAIDIZI MKUU WA KINARA: Amrao
> NAIBU WA MSAIDIZI MKUU WA KINARA: Fadhila
> NAIBU WA PILI WA KINARA: Kamu.’’ (Uk. 162).

Maelezo haya yanaonyesha mkataba kati ya Boyi, Fadhila, Amrao, LiMioe na Kamu kuhusu ugavi wa nafasi za uongozi. Hata hivyo, sheria za NUKA

hazikuruhusu nyadhifa za Amrao, Fadhila na Kamu. Hata hivyo, walihakikishiwa kuwa mamlaka haya yataidhinishwa baada ya kushinda uchaguzi.

Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* anatueleza kuhusu kisa ambacho mhusika Avadi alilazimishwa kuwaunga mkono sayari ya NUKA. Katika kisa hicho, Avadi akiwa chumbani anakumbuka baadhi ya watu waliokosa kutii mwenye nguvu na hatimaye wakauawa. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Picha za wale ambao hawakutii “wenye nguvu” na hatimaye “kubadilishwa cadaver” zilimjia Avadi. Aliwaona Jimase, Alekimu, Rojo, Bwana Kachooheze na Ka-Mj.’’ (Uk. 159).

Mfano huu unatuonyesha picha aliyoiona Avadi kuhusu wale waliouawa kutokana na kutotii mwenye nguvu. Anawaona watu kama vile: Jimase, Alekimu, Rojo, Bwana Kachuoheze na Ka-Mj. Kutokana na hofu aliyokuwa nayo, Avadi anagura chama cha BORA na kujiunga na NUKA. Aidha, anaamua kugombea kiti kama makamu wa U.

Inabainika kuwa mwandishi anatueleza kuhusu masuala yaliyotendeka nchini Kenya katika kipindi cha utawala wa Rais Moi. Mwandishi anatueleza kuhusu muungano wa NARC uliyowaleta pamoja viongozi kama vile Raila Odinga (Amrao), Fadhila (Charity Ngilu), Boyi (Kijana Wamalwa), Kamu (Kalonzo Musyoka) na LiMieo (Emilio Mwai Kibaki) ili kumpiku kiongozi wa KANU (NUKA) Uhuru Kenyatta (U) na naibu wake Musalia Mudavadi (Avadi).

Aidha, mwandishi anatubainishia ni kwa nini Mudavadi (Avadi) aliunga mkono chama cha KANU (NUKA). Isitoshe, picha zinazokuja akilini mwa Avadi ni ya wanasiasa waliokufa wakati wa utawala wa Moi. Hao ni pamoja na John Robert Ouko (Rojoo), Alexander Kipsang Muge (Alekimu) na J. M. Kariuki (Ka-MJ).

Aidha, mwandishi anaeleza kuhusu watu walioshikwa kwa sababu ya kupinga utawala wa Maotad. Watu hao walikuwa Charu, Mastanji na Amrao. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya kuteswa, Mastanji alitoka akiwa nusu mtu. Kwa msingi huu, mwandishi anatueleza tukio la kihistoria ambapo Raila, Charles Rubia na Kenneth Matiba walikamatwa kwa sababu ya kupinga utawala wa Rais Moi. Hali ya mwandishi wa *Mafamba* kusawiri matukio yaliyopita ya kisiasa inaoana na kauli ya Wamitila (2002) kuwa fasihi husawiri tajriba ya maisha ya binadamu ikiwemo siasa, uchumi na kijamii. Kwa msingi huu, mwandishi amesawiri athari za matukio ya kisiasa nchini Kenya.

### 2.3.3 Maudhui ya Elimu

Katika riwaya ya *Mafamba*, maudhui ya elimu yanajitokeza. Mwandishi anatueleza kuhusu elimu ya kisiasa na pia elimu ya shuleni. Anatueleza kuhusu namna utawala wa BORA ulivyoleta elimu ya bure. Aidha, kutokana na elimu hii watoto wengi walijiunga na shule ya msingi. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Licha ya maasi, yalikuwa mambo mengi ambayo utawala wa BORA ulikuwa umetia fora. Masomo ya bure katika shule za msingi. Jambo hili liliwafanya sayari ya BORA kuwa na wanafunzi wengi. Waliokosa elimu wakati wa utawala wa

> Jokaga na Maotad waliweza kuendelea na masomo yao katika enzi ya LiMioe. Kwa mara ya kwanza, kukawa na wanafunzi ambao ni wazee kabisa katika shule za msingi.’’ (Uk. 229).

Mfano huu uliomo katika riwaya ya *Mafamba* unathibitisha kuwa kuna mambo mazuri yaliyofanywa na utawala wa BORA. Utawala wa BORA ulileta masomo ya bure kwa shule ya msingi. Jambo liliowafanya wengi kujiunga na shule mbalimbali kuliko tawala za awali ikiwemo za Maotad na Jokaga. Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* anarejelea tukio la historia nchini Kenya. Kihistoria, elimu ya bure ya shule ya msingi ilianzishwa na serikali ya NARC mnamo 2003. Jambo hili liliwafanya wengi kujiunga na shule za msingi. Kwa mujibu wa Wizara ya elimu (2004), Nchini Kenya, idadi ya wanafunzi ilikuwa 6,078,100 mwaka wa 2000, 6,081,900 mwaka wa 2001, 6,131,000 mwaka wa 2002 na ikapanda hadi 7,208,100 mwaka wa 2003 baada ya kuanzishwa kwa elimu ya bure.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Mafamba* pia inasawiri elimu ya kisiasa. Katika riwaya hii, inabainika kuwa wanasiasa wengi walifunzwa siasa na Maotad. Ndiposa, hatimaye wanajamii wa NUKA hawaoni tofauti kati ya utawala wa Maotad na BORA (Uk. 228). Tawala zote hizi zilikuwa na sera ya MAFAMBA. Mwandishi anatupa sababu ya Saigeo kunyimwa uongozi wa sayari ya NUKA. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Kinara wa NUKA simwachii Saigeo. Saigeo ni mwanafunzi.
> Ni mwanafunzi nimesema. Nimesema ni mwanafunzi.’’ (Uk. 87).

Maneno haya ya Maotad yanaonyesha kuwa Saigeo alikuwa ni mwanafunzi wa kisiasa wa Maotad. Maotad alimfunza Saigeo siasa. Kwa hivyo, anakataa kumwachia uongozi. Tukio hili linarejelea wakati Moi alivyomkataza George Saitoti (Saigeo) kurithi uongozi wake. Moi alimtaja Saitoti kama mwanafunzi wake na alihitaji kujifunza mengi. (Hornsby, 2012).

### 2.3.4 Maudhui ya Usaliti

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2006), usaliti ni hali ya kuenda kinyume na makubaliano na mtu au kundi la watu au kudanganya. Katika riwaya ya *Mafamba*, mwandishi anatusawiria usaliti wa kisiasa. Anatuonyesha kuwa katika siasa hamna marafiki wa kudumu. Aidha, anaeleza kuwa kilicho muhimu ni matakwa ya wanasiasa wenyewe. Mwandishi anatueleza kuwa Amrao, Saigeo na Kamu wanaungana na kundi la LiMioe kwa sababu wanahisi wamesalitiwa na Maotad. Hii ni kwa sababu Maotad aliwaahidi uongozi lakini hatimaye Maotad anaamua uongozi wa sayari ya NUKA utachukuliwa na U.

Isitoshe, LiMioe anaahidi kuwatengea nafasi ya kisiasa akina Fadhila, Amrao na Kamu pindi tu anapokuwa kiongozi. Hali kadhalika, wanakubaliana kuwa watafanya kazi kwa pamoja bila kuzozana na wenye kushindwa katika uchaguzi hawataungana nao tena. Hata hivyo, LiMioe anaenda kinyume na mkataba huo. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Viongozi walioteuliwa walikuwa wengi kinyume na ahadi ya nane ya Kundi la BORA. Kukatokea tetesi. Watu walijiuliza ni

> kwa nini watu kutoka eneo moja la sayari ya BORA kupata nyadhifa nzito na zilizo muhimu.'' (UK. 84).

Dondoo hili linatuonyesha jinsi LiMioe alivyoenda kinyume na ahadi ya nane ya kundi la BORA. LiMioe aliwateua watu wengi katika nyadhifa za uongozi kinyume na makubaliano. Aidha, baada ya Boyi kuaga dunia Limioe anamteua Damisi kama naibu wake. Aidha, anateua watu wa eneo moja la sayari kumsaidia kuongoza. Jambo hili liliibua mgawanyiko katika kundi la BORA. Hii ni kwa sababu Damisi hakuwa kwenye mkataba. Isitoshe, Amrao, Fadhila na Kamu walihisi wamesalitiwa kwani badala ya kupewa nyadhifa walizoahidiwa walifutwa kazi.

Hali kadhalika, mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* anatuelezea jinsi ambavyo wanasiasa wanawasaliti wananchi. Wanasiasa hawa wanawapa wananchi ahadi ambazo hawazitimizi. Kupitia hotuba ya LiMioe, anatuelezea ahadi ambazo LiMioe aliwapa wananchi. Mwandishi anaeleza hivi:

> ''Wafanyakazi wa utawala wa BORA ambao watapatikana na hatia ya kujiingiza katika mafamba wataachishwa kazi, kushtakiwa, kupelekwa na kutupwa korokoroni.'' (Uk. 183).

Mfano huu unabainisha ahadi ambayo LiMioe aliwapa wananchi. Anawaahidi wananchi kuwa atawashika viongozi ambao watajiingiza katika mafamba. Hata hivyo, hatimizi ahadi yake kwani utawala wake unageuka na kuwa utawala wa Mafamba. Utawala wa LiMioe ulikumbwa na kashfa ya Anglolasting na hakuna hata kiongozi mmoja aliyechukuliwa hatua.

Imebainika kuwa matukio anayoyarejelea mwandishi ni ya kihistoria. Mwandishi anarejelea tukio ambalo Kibaki aliwasaliti Charity Ngilu, Kalonzo Musyoka na Raila Odinga kwa kuvunja mkataba waliokuwa nao. Aliahidi kuwatengea nyadhifa za juu uongozini atakaposhinda kura ya mwaka wa 2002. Aidha, Kibaki aliahidi kutoshirikiana na wapinzani wao. (Hornsby, 2012).

Hata hivyo, wakati Kijana Wamalwa anapoaga dunia anamchagua Moody Awuori kuwa naibu wake. Jambo hili liliibua mgawanyiko baina ya wanachama wa NARC. Wanachama wengi walihisi kuwa Kibaki aliteua watu wengi kutoka jamii yake katika nyadhifa za uongozi. Aidha, licha ya Kibaki kuwaahidi wananchi kuwa utawala wake utakabiliana na ufisadi vilivyo, utawala wake unakumbwa na kashfa mbalimbali ikiwemo sakata ya angloleasing. Aidha, Steeves (2006), anaeleza kuwa Kibaki aliwateua watu wengi wa jamii yake katika nafasi za uongozi. Hali hii inaweza kuwa inasawiriwa na mwandishi wa *Mafamba*, anapoeleza kuwa LiMioe aliteua watu wa sayari moja kumsaidia kuongoza.

**2.3.5 Maudhui ya Vita vya baada ya Uchaguzi**

Katika riwaya ya *Mafamba*, mwandishi anatusawiria vita vya uchaguzi. Vita hivi vilitokea kwa sababu ya sitofahamu kati ya LiMioe na Amrao mwaka wa 2700. Kila mmoja wao alishikilia kuwa alishinda uchaguzi. Kutokana na jambo hili, vita vilitokea kati ya wafuasi wao. Nyumba zilichomwa na watu wakauawa. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Amrao alisema yeye ndiye aliyekuwa mshindi na upande mwingine, LiMioe alishikilia madai yayo hayo. Wakereketwa wa viongozi hawa wawili walikatana kwa mapanga na kuchomana-miili na mali.’’ (Uk. 251).

Dondoo hili kutoka riwaya ya *Mafamba* linaonyesha namna Amrao na LiMioe walivyotofautiana kuhusu matokeo ya uchaguzi. Kutokana na jambo hili, wafuasi wao walipigana. Mwandishi anaeleza kuwa kulikuwa na uharibifu wa mali. Inabainika kuwa mwandishi japo anataja mwaka wa 2700, anarejelea uchaguzi wa 2007. Uchaguzi wa 2007 ulikumbwa na utata. Kutokana na Raila Odinga kutokubali matokeo, wafuasi wa Raila na wafuasi wa Kibaki walipigana. Matokeo ya mapigano hayo yalikuwa ni uharibifu wa mali na vifo vya watu wengi. Hata hivyo, mwandishi wa *Mafamba* anatumia wakati ujao yaani 2700 kusawiri matukio ya historia. Hali hii inaweza kuoana na maoni ya Munyole (2017) akimnukuu Foucault (1972) kuwa fasihi inafaa kuangalia matukio ya jadi kwa muktadha wa kisasa.

### 2.3.6 Maudhui ya Ukombozi

Ukombozi ni hali ya kujitoa katika dhuluma au mateso kwa kupitia vita au njia yoyote ule. Kwa muktadha huu, ukombozi hurejelea hali ambapo wanajamii hujitoa kutoka kwa dhuluma ya viongozi. Katika riwaya ya *Mafamba*, maudhui ya ukombozi yanajitokeza. Mwandishi anaeleza kuwa wanajamii walitafuta njia ya kujiokoa kutokana na wanasiasa wanaovunja mali. Wanajamii waliamua watawangoa mamlakani wanasiasa wanaoendeleza sera ya ‘mafamba’ kupitia kupiga kura. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Asilimia tisini na tisa nukta tisa ya viongozi walitimuliwa akiwemo Damisi ambaye alikuwa naibu wa LiMioe. Ulikuwa mfano wa mwosha huoshwa.’’ (Uk. 250).

Mfano huu unabainisha jinsi wanasiasa wengi walivyotimuliwa na wananchi. Wananchi walipiga kura ya kuwatimua baadhi ya viongozi ikiwemo Damisi. Wanasiasa hawa walikuwa wamehusishwa na sera ya ‘mafamba’.

Isitoshe, mwandishi anatueleza kuwa wakati vita vilipoibuka baada ya uchaguzi kulikuwa na harakati ya ukombozi. Harakati hii ilihusu ugavi wa mamlaka kati ya LiMioe na Amrao. Mwandishi anaeleza hivi:

> ‘‘Walierevuka na kuishi tena kwa amani baada ya sayari nyingine za nje kuingilia kati ya LiMioe na Amrao. Suluhisho lilikuwa ni mkataba wa kugawana mamlaka uliotiwa sahihi na kushuhudiwa na sayari zote mnamo tarehe 2/28/2800.’’ (Uk. 252).

Dondoo hili linaonyesha namna suluhisho lilivyopatikana katika eneo la Haponaseremwige. LiMioe na Amrao walikubali kugawana mamlaka baada ya sayari nyinginezo kuingia kati.

Imebainika kuwa mwandishi anatuelezea tukio la kihistoria. Anatueleza kuhusu uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Katika uchaguzi huu, viongozi wengi walishindwa na wapinzani wao. Isitoshe, kulikuwa na ghasia baada ya matokeo ya uchaguzi. Hatimaye, ilibidi watu kama vile Koffi Anan kuingilia kati ili kutafuta suluhu ya kudumu. (Hornsby, 2012).

Kutokana na haya, inabainika kuwa mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* aliweza kushuhudia uchaguzi wa 2007. Alishuhudia jinsi viongozi wengi walivyoshindwa kupata nafasi ya uongozi mara ya pili. Ndiposa, anasawiri matukio hayo ya kihistoria katika riwaya. Mhimili kuwa kazi za kubuni zina muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana ulifaa utafiti huu kwa kuwa mwandishi alichanganua matukio ya kihistoria.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia uwasilishaji wa maudhui katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba*. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995), mtafiti ameangazia maudhui kama vile: siasa, vita vya uhuru, elimu, mizozo ya ardhi na utabaka. Mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* anasawiri jinsi ukabila ulivyoathiri elimu kiasi kwamba watu walitengwa kwa msingi wa kikabila mfano ni katika shule ya St. Bwanga. Aidha, anaeleza kuhusu utawala wa kidikteta uliowafanya wengi kushikwa ikiwemo Abdalla. Isitoshe, mzozo wa ardhi unasababishwa na ugawaji wa mashamba na serikali. Ugawaji huu wa mashamba ulifanywa kwa mapendeleo. Hali kadhalika, utabaka kwake umetumika kama mbinu ya kuwanyang'anya maskini mashamba yao. Mwishowe, mwandishi anasawiri vita vya uhuru kama kigezo cha kuwafaidi jamii ya 'Wachovya' na sio jamii nyinginezo.

Imebainika kuwa mwandishi wa *Nyongo Mkalia Ini* ameathiriwa na matukio ya historia wakati wa ukoloni na utawala wa Jomo Kenyatta nchini Kenya. Katika vipindi hivyo, suala lililowaathiri waafrika zaidi ni ukabila na masuala ya ardhi. Ndiposa, anaonyesha jinsi wanajamii mbalimbali walifikiria kuwa uhuru ni wa jamii moja Isitoshe, anaeleza namna ukabila ulivyoathiri elimu Aidha, anaonyesha jinsi ugavi wa mashamba ulivyokumbwa na mapendeleo na jinsi watu wa tabaka la juu walivyonyakua mashamba ya watu wa tabaka la chini. Mwishowe, mwandishi anaonekana kuwa ameathiriwa na mazingira ya pwani. Ndiposa, anasawiri matukio yaliyotendeka pwani. Anatumia neno 'Gongwa' kurejelea Mombasa. Aidha, anataja maeneo mengi ya pwani kama vile Kilindini na Mariakani.

Imebainika kuwa mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ameathiriwa na vipindi viwili vikuu vya historia. Vipindi hivyo viwili ni wakati wa Utawala wa Moi na Kibaki. Katika tawala za Kibaki na Moi, Kenya ziliathiriwa na ufisadi. Aidha viongozi mbalimbali Waligura kutoka chama kimoja hadi kingine ili kupigania nafasi za uongozi. Isitoshe, wanasiasa waliwasaliti wanajamii kwa kuwapa ahadi za uwongo. Kutokana na jambo hili, wananchi wengi walizinduka na kuamua kutowapigia kura viongozi ambao wanashiriki ufisadi. Kutokana na matukio haya, mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ameegemea zaidi kutueleza kuhusu ufisadi unaoendelezwa na wanasiasa katika enzi za tawala za BORA na NUKA. Aidha, anaonyesha kuzinduka kwa wananchi kwani wanakosa kuwapigia kura wanaoshiriki 'mafamba'. Isitoshe, wananchi hawa hawaangalii vyama katika

kuchagua viongozi. Sura ya tatu imeangazia namna matukio ya kihistoria yalivyoathiri uwasilishaji wa wahusika katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

## SURA YA TATU

## ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KWA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA TEULE

### 3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilishughulikia maudhui yaliyotokana na athari za matukio ya kihistoria katika riwaya teule. Aidha, lengo la pili lilikuwa kuchunguza jinsi matukio ya kihistoria huathiri usawiri wa wahusika katika kuwasilisha kazi ya fasihi. Katika sura hii, mtafiti ameangazia wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ya Rocha chimerah na *Mafamba (1999)* ya Tom Olali. Pia amechunguza jinsi wahusika hawa wametumika kuendeleza ploti. Mtafiti amefanya hivyo akiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya. Nadharia hii imetumika kuchunguza wahusika wa kihistoria wamechorwa na kuwasilishwa kwa kuhamasishwa na wahusika halisi wa kihistoria katika riwaya teule.

### 3.1 Dhana ya Wahusika

Njogu na Chimerah (1999) wanadokeza kuwa wahusika huhimili vitushi vya riwaya na husaidia kuisukuma riwaya mbele. Aidha wahusika hujadiliwa jinsi wanavyoingiliana na maudhui. Haya huonekana katika mazungumzo yao, tabia zao na matendo yao. Kwa Mujibu wa Njogu na Chimerah (2016), riwaya nyingi za awali zilikuwa na wahusika watu na wahusika wanyama. Riwaya ya kisasa ya Kiswahili ina wahusika watu kinyume na ilivyokuwa katika riwaya za awali. Fasihi ya kabla uhuru ilikuwa na wahusika watu na wahusika wanyama kwa

sababu mazingira ya wanyama yalikuwa sehemu ya maisha ya jamii zote za Kiafrika. Baada ya miaka ya sabini, riwaya ya Kiswahili ilianza kukaribia uhalisia wa kisanaa na kuwezesha taratibu za maisha kwa mfano dini na siasa kutazamwa kwa kina. Aidha wahusika katika riwaya hizi wanahusishwa sana na hisia zao na masuala ya utu na uhuru wao. Isitoshe, wengine wanapewa majina ya kimajazi ili kulenga sifa zao mahsusi. Njogu na Chimerah (2016) wanaendelea kusema kuwa, kuna juhudi za kuwatumia watu wa kawaida kama wahusika badala ya kutumia majitu, mashetani, na mazimwi. Aidha, wasanii hubuni wahusika wanaoweza kupatikana katika jamii. Wahusika hawa ni wahusika wenye udhaifu na uwezo. Tabia za mhusika hubainishwa kwa namna anavyotumia lugha. Lugha ya mhusika inaonyesha mawazo yake na huelekeza msomaji kwenye matendo yake. Hivyo, msomaji anapochunguza lugha ya mhusika hupata mwangaza kuhusu hulka za mhusika huyo. Isitoshe, saikolojia ya mhusika hueleweka kupitia mahusiano yake na jamii. Aidha, mhusika hujibainisha kutokana na matendo yake. Vilevile, mhusika hujibainisha kupitia wahusika wale wengine wengine.

### 3.1.1 Uhusika na Wahusika katika Fasihi

Wahusika ni sehemu ya fani wanaosawiriwa kutumia sifa za kitabia, kifalsafa, kimaumbile, kiitikadi na kimaadili (Njogu na Chimerah, 1999). Mink (1970) anaeleza kuwa uhusiano kati ya historia na bunilizi unaweza kudhihirika katika matukio na pia kupitia kwa wahusika. Aidha, waandishi wengi wa riwaya huchukua wahusika halisi, matukio yanayojulikana na yasiyojulikana kuwa kiini

cha hadithi. Isitoshe, wahusika hawa pamoja na matukio haya yanajulikana vizuri ama huwa yamehifadhiwa katika rekodi za kihistoria kama vile stakabadhi za nchi, magazeti na barua (Mink, 1970).

### 3.1.2 Wahusika wa Kihistoria

Wahusika wa kihistoria ni wahusika wanaopatikana katika kazi za kihistoria. Katika kazi zinazobuniwa, wahusika huumbwa ili kuwakilisha wanaohusishwa na matendo katika kazi hiyo. Mhusika wa kihistoria ni yule anayesawiriwa kama aliyeishi kipindi fulani cha hapo awali (Wamitila, 2008). Hata hivyo, waandishi katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* wamewasilishwa kihalisia hata kama waliishi kihistoria. Mwandishi Rocha Chimerah, amewabuni wahusika wake ili kuwa kiwakilishi cha jamii halisi. Kupitia kwa matendo, tabia, itikadi na mitazamo yao, wahusika hawa wa kubuni ambao ni Mumanyi, Omari, Obote, Munga, Bwana Khalifa, Amu Zaid na Warega. Mwandishi ameangazia jamii na maswala ambayo ni changamoto kwenye jamii. Aidha, mwandishi wa *Mafamba* anawasilisha wahusika wa kihistoria wengi. Mwandishi amewatumia kuangazia masuala mbalimbali ya kihistoria.

### 3.1.3 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Wahusika katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia ini* (1995)

Wahusika katika riwaya hii ni wa kihalisia. Wamitila (2008) anafafanua wahusika wa kihalisia kama wale sifa zao nyingi zinahusishwa na maisha ya binadamu ya

kila siku katika kazi za kiubunifu. Wamitila (Keshatajwa) anadokeza kuwa mhusika wa kihalisia huainishwa kwa kuzingatia taratibu za maisha halisi. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, wahusika ni watu halisi wanaotekeleza majukumu halisi katika maisha halisi ya jamii zao. Mathalani, wahusika Mumanyi na Obote ni binadamu halisi wanaotekeleza majukumu halisi. Wanatembea kwenye ofisi ya bwana Khalifa kwa minajili ya kutafuta kazi. Wanapopata nafasi ya kuingia ofisini kila mmoja anapata nafasi ya kutoa tawasifu yake kwa bwana Khalifa. Baadaye, kila mmoja anapata kazi. Wahusika hawa wamehusishwa na sifa na majukumu halisi.

Mwandishi Rocha Chimerah ameainisha wahusika wake kwa kuegemea vipengele viwili ambavyo ni utabaka na umri. Katika tabaka la juu kuna mhusika Khalifa na Amu Zaid. Aidha tabaka la kati linawakilishwa na Munga, Mumanyi, Warega, Omari, Mama Mumbe na Esta. Tabaka hili ni kiwakilishi cha watu wenye elimu kubwa ila mapato yao hayakidhi mahitaji yao. Isitoshe, kuna tabaka la wenye elimu ndogo na wasio na elimu kamwe. Tabaka hili linalazimika kuuza uhuru na utu wao kwa ukosefu wa mahitaji ya kimsingi. Tabaka la mwisho ni la watu wasiojiweza kamwe na mfano riwayani ni kaka yake Warega. Mhusika huyu ni kiwakilishi cha watu wanaoishi kwa kuombaomba na idadi yao ni nyingi katika jamii.

Aidha, Rocha Chimerah ametumia kipengele cha umri katika kuainisha wahusika wake. Kuna uhusiano baina ya wazee na vijana. Kupitia kwa mahusiano, inabainika wazi kuwa kuna mwanya kati ya vijana na wazee. Katika wodi ya wagonjwa, hapana mazungumzo kati ya vijana na wazee. Kutoingiliana huku kati ya wazee na vijana ni dhihirisho kuwa enzi ya wazee imekwisha na ni wakati wa vijana kuchukua mamlaka (Njogu na Chimerah, 2008). Aidha, wanaendelea kusema kuwa ndiyo sababu wahusika takribani wote katika riwaya wana umri mdogo wakilinganishwa na wakinzani wao ambao ni Khalifa na Amu Zaid.

Sehemu hii imeangazia wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Nyongo Mkali Ini*. Mtafiti amefanya hivi ili kuchunguza ni kwa kiasi kipi mtunzi wa riwaya hii alivyoathiriwa na matukio ya kihistoria au alivyowachora kama ni kielelezo cha mhusika wa kihistoria aliyewahi kuishi. Baadhi ya wahusika ni wa kubuni katika viwango vyote ili kuipa riwaya hii sura ya bunilizi. Wahusika walioangaziwa ni Omari, Momanyi, Munga na bwana Khalifu.

### 3.1.4 Omari

Mhusika Omari ni mhusika wa kiumri na pia mhusika wa kubuni katika viwango vyote. Ni miongoni mwa wahusika wanaoifanya kazi hii iwe bunilizi. Omari ni mwanawe mzee Swalehe. Amesawiriwa kama kijana mcheshi na mpenda raha kwelikweli. Anapenda kurusharusha maneno bila nidhamu na bila kuchunga ulimi wake. Aidha ni mfyozi kulingana na nukuu hii;

> ‘‘Omari wacha ufyozi bwana. Mstaarabu huteua la kunena. Kurusharusha maneno bila nidhamu na kubwata utakavyo sio msingi wa maendeleo, wala ishara ya ungwana.’’ (uk 11).

Isitoshe, ni mkware kupindukia. Anawapenda wanawake zaidi ya nafsi yake jambo linalosababisha kifo chake anapopatikana na mke wa mwenyewe (uk 18). Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (2016), wahusika hutumiwa na mwandishi kuweza kuwakilisha maudhui katika kazi ya fasihi. Mhusika Omari ni mwanafalsafa anayeshikilia msimamo kuwa nyuki ni wachovya asali. (uk 29).

Aidha, mhusika Omari alitumika katika kutekeleza mauaji ya wote waliopinga njia potovu za Bwana Khalifu. Mwandishi Rocha Chimerah ameathiriwa na uozo uliokuwa ukitendeka katika jamii. Viongozi na matajiri kama vile Khalifu wanawatumia vijana wachochole vibaya katika kutekeleza maovu katika jamii.

### 3.1.5 Mumanyi

Mhusika Juma Mumanyi ni msomi ambaye ana masomo ya kutosha lakini hana kazi. Mwandishi anamsawiri kama mhusika wa kihistoria kwa kuwa anahamasishwa na wasomi walioishi nyakati za miaka ya themanini. Haya yanabainika wanapotembelea ofisi ya bwana Khalifu wakiwa na Obote kwa minajili ya kutafuta kazi anaposimulia kuhusu tawasifu yake kama ifuatavyo;

> ‘‘Mimi nilizaliwa Majengo, Doria, miaka ishirini iliyopita. Nilisomea shule ya msingi ya Methodist huko huko Doria, ikiitwa Miyani. Toka huko nikaenda Ota-la-samaki kwa masomo ya juu ambayo niliyamaliza mwaka juzi. Nimetafuta kazi tangu siku hizo lakini sijafanikiwa…’’ (uk 32).

Mhusika huyu ni kiwakilishi cha vijana wengi waliosoma lakini hawajapata kazi. Aidha, anasawiriwa kama mtambuzi wa mambo ndiyo kwa sababu anapewa kazi ya kutafiti fumbo la nyuki na akaifanya vizuri.

Njogu na Chimerah (1999) wanadai kuwa, mwanafasihi hujiuliza maswali mengi kuhusu jamii yake. Ndiposa mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, Rocha chimerah anamsawiri mhusika Mumanyi kama msomi na mtambuzi wa mambo lakini hana kazi. Inabainika katika mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa kazi ya kifasihi ni matukio ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi peke yake. Mwandishi Rocha Chimerah anaisawiri hali halisi kama ilivyo nchini Kenya ambako wanafunzi wengi wamesoma lakini hawana kazi. Ni kielelezo cha wasomi wengi walioshi kati ya miaka 1980 na 1990 waliokuwa wafikirivu. Kwa mujibu wa gazeti la *Business Daily (Jumatatu 24 Februari 2020*) zaidi ya asilimia theluthi ya vijana wanaopaswa kuwa na kazi hawana kazi. Aidha, Kenya ni nchi inayoongoza kwa takwimu za juu katika jumuia ya Afrika Mashariki katika ukosefu wa kazi kwa vijana.

### 3.1.6 Munga

Munga ni kiwakilishi cha mhusika wa kihistoria. Mwandishi amemsawiri kama mhusika anayependa maendeleo na pia mwanamapinduzi. Ni kielelezo cha wasomi waliokuwepo miaka ya utawala wa chama kimoja. Ni msomi na

mwanafunzi katika chuo kikuu cha Zutafindaki mjini Gichuka kupitia kwa barua yake aliyomwandikia Mumanyi, mwandishi amemsawiri mhusika huyu kama mwanamapinduzi.

Anatetea haki za wanyonge na kupinga udhalimu unaoendeshwa na wenye mamlaka. Suala hili linathibitishwa na usemi huu;

> ‘‘Nafikiri siasa ya mkoloni ya “gawa-utawale” yachunguliachungulia… japo sisi wanamapinduzi twajitahidi kuifyeka, kimezuka kikundi cha wasaliti ambacho chaipalilia. Na mwanamapinduzi ikiwa atamruhusu msaliti kudumisha uharibifu wake, atakuwa si mwanamapindizi tena. Hivyo asilani; hatutakubali usaliti wa aina yoyote, hata kama italazimu Zutafindaki ifungwe miaka ishirini ndipo usaliti huo uamgamizwe. Sisi tuko tayari. Tuko tayari hata kumwaga damu ikiwa ndiyo njia pekee ya kuwafyeka vibaraka na wafuasi wao.’’ (uk 15-16).

Mwandishi amemsawiri mhusika Munga kama mwanamaendeleo na mkombozi. Anafahamu mambo kitaaluma na anaamini kujikomboa kwa njia ya elimu. Kupitia kwake mwandishi anaonyesha kuwa vijana katika bara la Afrika watalikomboa bara lao. Kwa mujibu wa Kipiyo (2000), makundi yasiyo ya kiserikali yakiungwa mkono na wahadhiri wa vyuo vikuu ya umma, waandishi wa habari, mawakili walichangia pakubwa sana katika kuleta mfumo wa vyama vingi nchini Kenya. Aidha, taasisi za elimu ya juu zilihusika pakubwa.

Amutabi (2002) anasema kwamba, migomo ya wanafunzi ilisababishwa kwa sababu ya kupigania mahitaji ya kibinafsi na ya jamii kwa jumla. Kwa mujibu wa Hornsby (2012) viongozi wengi wa wanafunzi katika vyuo vikuu walifungwa jela

na wengine wakapotelea katika harakati za kupigania Demokrasia. Maoni haya ya Amutabi na Hornsby yanashabihiana na tajriba anayopitia Munga. Kupitia kwa barua ya Munga ni wazi kuwa kulikuwa na kikundi cha wasaliti. Munga anadai kuwa walikuwa tayari kukabiliana na wasaliti kwa vyovyote vile.

> ‘‘Tuko tayari hata kumwaga damu ikiwa ndiyo njia pekee ya kuwafyeka vibaraka na wafuasi wao.’’ (uk 16).

Kwa mujibu wa Klopp na Orina (2002), Rais Moi na wafuasi wake walitegemea kwa kiwango kikubwa mfumo wa gawa-utawale kuthibiti wanafunzi na wahadhiri vyuoni. Waliopinga utawala wa Rais Moi walinyimwa nafasi za masomo na kazi. Ni mbinu iliyotumika wazi mnamo mwaka wa 1985. Aidha, kupitia kwa msimamizi wa chuo, askari walivamia mkutano wa maombi katika chuo kikuu cha Nairobi, wakawachapa na kuwaua wanafunzi.

Kwa mujibu wa Ukkan (2004), wanahistoria mpya wanadai kuwepo kwa uhusiano wa karibu sana kati ya kazi za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Aidha, kazi ya fasihi sio matokeo ya ubunifu wa mwandishi pekee bali pia kazi zingine. Aidha, fasihi huhusishwa na kipindi maalum cha wakati; mfumo wa utawala husika katika, kipindi kile ambacho kazi ile inapoandikwa na huhusisha fasihi na jamiii kwa jumla. Rocha Chimerah, amemtumia mhusika Munga katika kuyasawiri maswala yaliyokuwa yakitendeka katika kipindi cha harakati za kupigania mfumo wa vyama vingi vya kiutawala nchini Kenya.

### 3.1.7 Bwana Khalifa

Mhusika Bwana Khalifa amebuniwa na mwandishi ili kuwa kiwakilishi cha watu walioshi na walioko sasa kwenye jamii. Ni tajiri mwenye mali na ushawishi mkubwa. Ni Mkurugenzi anayesimamia kampuni yao na Amu Zaidi. Kupitia kwa njia za kijanja anampindua Amu zaidi na kujinufaisha na urithi wa wazazi wake. Aidha, ni laghai anayewahini watu fedha zao na kuwafyonza maskini licha ya kuwa mhusika mwenye bidii katika kutafuta mali.

> ‘‘Tuliafikiana juu ya mambo fulani tukaweka mkataba. Kila mmoja akatia sahihi kuwa yeye akifika hapa atafanya biashara ya pembe za ndovu. Tuliafikiana kuwa mali yote atakayopata ni yetu ya shirika. Mimi, kwa upande wangu, chochote nitakachorithi kwa wale walezi wangu ni chetu sote wawili. Tukakubaliana na kuweka pesa zote katika benki ya shirika isipokuwa zile nitakazopatikana kutokana na uganga wangu; na zile atakazopata kutokana na kazi yake ya miti shamba, ambayo ndiyo hiyo aliyoifungulia ofisi. Kazi yenyewe nilimfunza mimi ili naya apate senti za kutupatupa hapa na pale… ’’ (uk 55).

Mwandishi ametumia mhusika Bwana Khalifa kuwakilisha tabaka la juu. Amesawiriwa kama mhusika fisadi na mwenye kugandamiza wanyonge. Bwana Khalifu amewajiri vijana ili kutekeleza maovu kutokana na usemi huu wa Mumanyi kuwa;

> ‘‘Nilishangazwa na Omari na Obote. Sote tuliajiriwa na mtu mmoja, katika ofisi moja. Ajabu ni kuwa sijawaona ofisini minghairi ya siku ya kwanza ya kufahamiana na Bwana Khalifu. Nilitaka kujua kazi yao haswa ni kazi gani. Mimi yangu siifichi; ni utaarishi. Je, wao waifanya wapi? Au ofisi hii ina tawi jingine mahali pengine? Basi mbona sijadokezewa…?’’ (uk 90).

Kupitia kwa uzungumzaji nafsia wa Mumanyi, inabainika kuwa vijana wenzake ambao ni Omari na Obote wanahusika na kazi na biashara za kisirisiri ambazo

yeye licha ya kuwajiriwa pamoja hajazielewa. Kati ya kazi vijana wanazopewa ni kuhusishwa na biashara haramu ya uuzaji wa pembe za ndovu. Aidha, wanahusisha pia katika kutekeleza mauaji.

> ‘‘Palipiga zii kitambo kikubwa. Nilipofunua kinywa, nikamwuliza Omari taratibu, Omari?
> Naam.
> Ulimwua Alii…?
> Sikumuua…si mimi! Yote ni mpango ya ‘halifu’. Khalifu aliyetokwa na utu toka siku ya kuzaliwa… Uvumi wote mliosikia ni kweli…Lakini sikudhamiria. Alinilazimisha…!’’ (uk 112).

Inabainika kuwa katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* watu wa tabaka la juu wanawanyanyasa watu na hata kuwaua kwa kutumia vibaraka. Aidha, kupitia kwa mazungumzo baina ya Obote, Warega na Mumanyi, vijana wanalazimishwa na watu wenye nguvu zaidi kuua. Baada ya kutekeleza uhalifu huu hatima yao inakuwa kifo.

> ‘‘Obote aliondoka kitandani pole pole, akaketi kochini. Akanena, Kibibi… na Mumanyi…Yafaa mjue kuwa sikumwua mimi Omari. Najua mtu yeyote aliyekuwa pamoja nasi jana usiku, moja kwa moja, atatuhumu kuwa ndimi niliyemwua kwa kuwa tulitoka sote, na mwenzake hakurudi tena, hai. Lakini simi niliyemwua. Ikizidi pia mwisho wangu hau mbali…
> Mimi sikuua…Na hata kama nilihusika, ningependa mfahamu kuwa wangine walihusika, huhusika kwa kulazimishwa na mtu mwingine mwenye nguvu na uwezo zaidi.’’ (uk 115).

Wanauhistoria mpya huiona historia sio kama tu matukio la awali bali kama maelezo ya kweli kuhusu binadamu kwa mujibu wa jamii husika (Sharma, 2014). Mwandishi Rocha Chimerah kwa kiasi kikubwa ameathiriwa na maswala yaliyokuwa yakiendelea katika jamii yake. Watu waliokuwa kwenye tabaka la juu

wanawatumia vibaya wachochole kwa kuwahusisha na nyendo mbaya za kihalifu, kuwakandamiza, kuwanyanyasa na hata kuwaua.

Rocha Chimerah ametumia mhusika Bwana Khalifa kama kielelezo cha watu walioishi wakiwa na ushawishi mkubwa wa kuwatumia vijana wachochole katika kutekeleza uovu katika jamii. Uovu huu ulihusisha biashara haramu na hata mauaji. Mambo haya yalitekelezwa Kutoka kipindi cha utawala wa Ukoloni hadi kipindi cha utawala wa Jomo Kenyatta nchini Kenya.

### 3.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Wahusika katika Riwaya ya *Mafamba* (2008)

Mwandishi Tom Olali ametumia mbinu kadhaa katika uainishaji wa wahusika kwenye riwaya ya *Mafamba*. Ametumia mbinu anagramu, majazi na mdokezo. Kwa mujibu wa Mdee na wenzake (2000), *anagramu* ni mbinu ya kuunda neno kwa kubadilisha herufi za neno hilo. Mwandishi amebadilisha herufi za majina kamili ya wahusika na kuchukua mianzo ya majina yao kamili. Kwa mfano; Daniel Toroitich Arap Moi ni Maotad, Raila Amolo Odinga ni Amrao, Emilio ni Limioe, Charity Kaluki Ngilu ni Chakangi, Simeon Nyachae Sinya na Stanley Jindo Matiba ni Manstanji miongoni mwa wengine.

Mwandishi pia, ametumia mbinu ya tafsiri katika wahusika Boyi ambaye ni Kijana na Fadhila ambaye ni Charity. Aidha ametumia mdokezo pale anaponuia kutaja mianzo ya majina ya wahusika kama vile mhusika U na mhusika Avadi.

Katika sehemu hii, mtafiti amejadili wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Mafamba* (2008). Mtafiti amefanya hivi ili kuchunguza ikiwa mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ameathiriwa na matukio ya kihistoria katika uwasilishaji wa wahusika. Wahusika walioangaziwa ni Maotad, Amrao, Limioe na Manstanji. Mwandishi kupitia kwa sifa, hulka na matendo ya wahusika hawa, ameangazia maswala ya uongozi, ufisadi, miungano ya vyama vya utawala na ukatili. Mwandishi anaeleza kuhusu utawala wa kidikteta wa Maotad ambao baada ya miongo miwili unabadilika na kuwa wa kidemokrasi. Kipindi cha kidikteta kilijawa na maonevu, ufisadi na mauaji mengi. Baadaye viongozi wengine wa kisiasa wanaungana kwa minajili ya kusitisha Mafamba ila ndoto hii haikutimia.

Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* ameathiriwa na matukio ya kihistoria wakati wa utawala wa Rais Moi na utawala wa Rais Kibaki. Baada ya kutawaliwa kwa muda mrefu na Rais Moi, wanamapinduzi walifanya juhudi ili kuweza kuleta Demokrasia nchini Kenya. Mhusika kama vile Maustanji ambaye ni Stanley Njindo Matiba alikuwa katika mstari wa mbele katika kupigania Demokrasia kiwango cha kupoteza uhai wake. Aidha Amrao, ambaye ni Raila Amolo Odinga hakuachwa nyuma katika kupigania Demokrasia.

### 3.2.1 Maotad

Mhusika Maotad ni kiongozi wa sayari ya NUKA**.** Maotad amesawiriwa kuwa na sifa ya ukatili. Mwandishi anaeleza jinsi macho yake yalivyomulika na kupenya mbaru za mwathiriwa yeyote. Aidha macho ya Maotad yaliweza kuupenya mwili wa mkazi mmoja na kisha mkaazi huyu aliyejulikana kama Rojoo kuaga dunia. (uk 7). Kwa mujibu wa Hornsby (2012), miaka ya themanini hadi tisini nchini Kenya ilizungukwa na utawala wa kidikteta na maonevu pale ambapo utawala ulijihusisha na ukandamizaji na kutojali. Mhusika Maotad amepewa sifa ya ukatili inayosadifiana na matendo maovu na ya kikatili yaliyokuwa yakiendelezwa katika utawala wake.

Aidha sifa hii inaendelea kubainika kupitia mikakati ya tafrija za baada ya miaka 500. Inasemekana kuwa yeyote ambaye angezua rabsha angekufa (uk 17). Mhusika Shanata pia anamnasihi Maotad asimuue baada ya kumpa ushauri (uk 21). Mastanji ni mhusika amabaye alithiiriwa na ukatili wa Maotad na maisha yake yakabadilika kabisa (Muraya, 2020).

Kwa mujibu wa Muraya (2020), chumba cha Nyayo kilikuwa na vyumba kumi na vinne. Vyumba hivi vilikuwa na seli ndogo nyeusi na vilikuwa na kuta sisizopitisha sauti, pia vilikuwa na vishimo  vidogo vya kutolea hewa. Mahali hapa wafungwa walipitia dhuluma kali. Wafungwa wangewekewa baridi jingi na wakati mwingine joto kali. Aidha miguu yao ingezamishwa kwenye maji. Msimulizi wa

riwaya ya *Mafamba* katika utenzi wa kazi yake aliathiriwa na maswala yaliyokuwa yakitendeka katika mazingira yake. Kiongozi Maotad ambaye ni Moi aliongoza nchi kwa mabavu na maonevu hadi kiwango cha kuwa katili na kuwadhulumu wapinzani wake. Ndiposa mhimili kuwa kazi za kubuni zina muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana una mashiko.

### 3.2.2 Amrao

Mhusika Amrao alikuwa kiongozi wa sayari iliyojulikana kama DiPieNi (NDP). Amesawiriwa kama kiongozi aliyekuwa na mamlaka makubwa katika sayari ya DiPieLi ambaye hakupata nafasi ya kuchuma matunda ya uhuru.

> ‘‘Amrao hakupata heri ya kuchuma matunda katika utawala wa enzi ya sayari ya Dunia. Alikuwa mwenyeji wa sayari ya DiPieNi ambayo ilipakana na NUKA na kuathiriwa mno na baadhi ya sera za NUKA.’’ (uk 27).

Mwandishi anamsawiri kama kiongozi mwenye athari kamili kwa hadhari yake. Yabainika kuwa sifa zake zilienea na alijulikana na watu wa sayari ya NUKA kama vile alivyojulikana Maotad;

> ‘‘Sifa za Amrao zilienea na alijulikana na watu wa sayari ya NUKA- kama vile alivyojulikana Maotad.’’ (uk 24).

Aidha, Amrao aliwahi kusukumwa ndani kwenda kula maharagwe katika kipindi kimoja kwa jumla ya miaka thelathini kwa kosa lililokuwa la kiwango cha uhaini (uk 25). Kupitia kwa wimbo wake kwenye (uk 27) ni kiongozi ambaye ana wajibu wa kuzitetea haki za wakati wa sayari zote, wajibu wa kufungua kambi za kusoma,

wajibu wa kuongeza vituo vya afya, wajibu wa kuleta usalama, wajibu wa kufufua uchumi na mwishowe wajibu wa kukomesha mafamba.

Kwa mujibu wa Onsando (2015), Raila Odinga ametekeleza jukumu la kuunda, kuelekeza, kuathiri na kuamuru siasa, nchini Kenya kwa miaka mingi. Kwa mujibu wa gazeti hili, siasa za Kenya kamwe haziwezi kusalia zilivyo endapo Raila Odinga angestaafu kutoka kwa siasa. Kwa mujibu wa Wayua (2020), Amolo Odinga alifungwa jela miaka saba kwa tuhuma za kuhusika katika majaribio ya kuipindua serikali ya Rais Daniel Arap Moi mwaka wa 1982. Asamba (2018) anahoji kuwa usawiri wa vyombo vya habari kuhusu Raila umechangia pakubwa katika jinsi wananchi wanavyoamua wakati wa uchaguzi. Raila ametekeleza jukumu kubwa miaka ya themanini katika kupigania mfumo wa vyama vingi nchini Kenya, hivyo akaweza kuibuka kuwa kiongozi wa kisiasa ambaye anaweza kuiwakilisha Kenya katika ngazi za kimataifa (Obonyo, 2017).

Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* hakuachwa nyuma katika kumsawiri mhusika Amrao kama mhusika ambaye huathiri siasa nchini Kenya pakubwa. Aidha Amrao huzipa mwelekeo siasa za Kenya. Haya yanabainisha kuwa mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika huathiri uhakiki wa ufasili wa matini ya kifasihi una mashiko. Kwani baadhi ya maswala yaliyoibua kazi hii ya kifasihi ni siasa.

### 3.2.3 Limioe

Limioe ni mhusika wa kihistoria aliyewahi kuishi, anayesawiriwa kama asiye na msimamo. Aidha amebandikwa jina Tiara. Inadaiwa kuwa alienda kinyume na kulipotokea upepo. Limioe sawia na mhusika Maotad anapenda Mafamba. Inasemekana kuwa nyendo zake na zile za Maotad zilikuwa zinafanana. Alikuwa kinara wa sayari ya PiDi (DP). Mwandishi anasimulia kuhusu mazungumzo kati ya Boyi, Limioe na Fadhila. Mazungumzo yalilenga muungano wa vyama vya kisiasa.

> ‘‘Asante Fadhila. Naam, huyu ni LiMioe. LiMioe ni huyu. Ndiye kinara wa sayari ya PiDi. Ndiyo, PiDi. Hivyo, huyu ni LiMioe kinara wa sayari ya PiDi. Fadhila, wakazi wa Kefo na Pidi wametutuma hapa. Wangetaka ushirikiano na wakazi wa sayari yako tukufu.’’ (uk 40).

Mwandishi anasimulia jinsi Limioe alivyopata ajali akielekea pande za nzambani alipokuwa katika shughuli za kutafuta chakula kutoka kwa wakazi wa Bikerani-Msiige. Aidha kulikuwa na kundi la U na kundi la Limioe. Makundi haya mawili yalihusu kura ya maoni. Kura ya maoni yaonyesha U atashinda. (uk 173). Tukio hili ni tukio la kihistoria nchini Kenya ambapo Kibaki alipata ajali mbaya sana ya barabarani alipokuwa anatoka ukambani kufanya kampeni za kura ya maoni kuhusu kubadilisha katiba.

Mwaka wa 2000, kamati ya bunge iliyoongozwa na Odinga ilikuwa imeteua Yash Pal Ghai kuongoza shughuli za kuchunguza katiba. Kwa mujibu wa kituo cha habari cha KTN (8/1/2018), baada ya muungano wa NARC, Emilio Kibaki

aliteuliwa kama kinara ambaye angewania urais, dhidi ya Uhuru Kenyatta ambaye alikuwa ameteuliwa na Moi aliyekuwa ametawala nchi ya Kenya kwa miaka ishirini na nne. Kilikuwa kinyang'anyiro dhidi ya farasi wawili.

Mnamo tarehe tatu Jumanne Desemba mwaka wa 2002, Kibaki alipata ajali mbaya ya barabarani alipokuwa akirejea mjini Nairobi kutoka Ukambani alikokuwa akifanya kampeni za Urais. Mwandishi ametumia mhusika Emilio Kibaki ili kuweza kusimulia matukio ya kihistoria yaliyotokea nchini Kenya. Kibaki alihusika katika kupokea uongozi wa nchi ya Kenya ambao ulikuwa mikononi mwa kiongozi raisi Moi kwa zaidi ya miongo miwili. Aidha, ajali mbaya ya barabarani ni tukio la kihistoria ililohusisha Mwai Kibali wiki chache pekee kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2002. Isitoshe Mwai Kibaki ni raisi aliyeapishwa akiwa mgonjwa. Mwandisi hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake (Njogu na Chimerah, 1999). Tom Olali ni mwandishi ambaye ameathiriwa na matukio ambayo yalitokea nchini Kenya. Athari hizi zimechipua kazi yake. Mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya unaosema kuwa kazi ya kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi peke yake una mashiko kwa kuwa mwandishi Olali ameshughulikia maswala mbalimbali ambayo si ya kubuniwa pekeee ila pia ya kiuhalisia.

### 3.2.4 Manstanji

Mhusika huyu alijulikana kwa jina kamili kama Stanley Jindo Matiba. Matiba alifanikiwa sana katika enzi za baada ya utawala wa wakoloni katika kupigania Demokrasia nchini Kenya. Alihukumiwa bila makosa mnamo mwaka wa 1990 wakiwa na Charles Rubia. Akiwa katika jela ya Kamiti alikatazwa kupata matibabu na hapo akapatwa na kiharusi (Walloga, 2013). Aliongoza katika uanzilishaji wa muungano wa upinzani uliojulikana kama Forum for the Restoration of Democracy (FORD). Mwandishi anasimulia chanzo cha uadui kati ya Maotad na Manstanji. Aidha anaeleza chanzo cha uhasidi huu ni kuwa Manstanji alimzaba Maotad kofi jambo lililosababisha uhasidi wao. ‘ Kuzaba kofi’ ni msemo unatumiwa kijazanda na mwandishi kumaanisha kupinga utawala wa Rais Moi. Matiba aliongoza katika harakati za kuanzisha mfumo wa vyama vingi nchini Kenya. Jambo ambalo halikupokelewa kwa mikono miwili na Rais Moi. Aidha mwandishi anasimulia mateso mhusika huyu aliyoyapata baada ya kupelekwa Mkanyageni;

> ‘‘Alitoa amri. Amri katili. Amri katili kwelikweli. Amri ambayo ilibadilisha maisha ya Manstanji milele. Amri hiyo ilisema Manstanji alishwe siafu, pilipili, shubiri, sumu ya anaconda kama kifungua kinywa. Mlo wa mchana alilishwa maji ya batari, vipande vya chupa, gundi ya viatu, samadi na moshi wa tairi ya magari. Chajio kilikuwa mseto wa vyakula mbalimbali- panya wa kuchemshwa, msongareli wa kusagwa, sindano za kusagwa, miiba ya kukaangwa, ulimi wa kinyonga, damu ya nzi na mate ya kombamwiko. Chumba alimokuwa hakukuwa na kitanda, kiti, zulia, mkeka, kitabu bali ndoo aliyotumia kutema mate. Aliyalalia maji.Usiku alitembelewa na wageni-anaconda. Chumba hicho kilikuwa ndani ya jingo mashuhuri katika sayari ya NUKA lijulikanalo kama Mkanyageni.’’ (uk 47).

Hayo yalikuwa baadhi ya mateso aliyoyapata Matiba alipofungwa mwaka wa 1990. Maisha ya Matiba yalibadilika kabisa kutokana na mateso haya jambo ambalo linadhibitishwa na mwandishi kupitia usemi huu;

> ‘‘Ulipoingia Mkanyageni, kulikuwa na matokeo matatu. Mwanzo kulikuwa kule kuingia na kutoka, pili kulikuwa kuingia na kutoka nusu binadamu. Tatu, kulikuwa kule kuingia na kutotoka. Manstanji aliingia na kutoka nusu binadamu.’’ (uk 48).

Kungu na Gichobi (2020) wanasimulia jinsi Matiba na Rubia walivyokamatwa mnamo tarehe 4 Julai mwaka 1990. Anaeleza jinsi walivyofungiwa na wakatesewa kwenye chumba cha Nyayo wakati wa msukosuko kwa wakenya. Wafula na Njogu (2007) wanahoji kuwa nadharia ni zao la utamaduni na historia ya jamii inayohusika. Kwa mujibu wa Bressler (2003), wana uhistoria mpya hujaribu kuelewa fasihi kutokana na mtazamo wa kihistoria. Kutokana na haya mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa kazi za kubuni huwa na muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana ni mwafaka kwa kuwa mwandishi Tom Olali katika kubuni kazi yake aliegemea katika muktadha wa jamii katika kuyaangazia maswala yaliyokuwa yakiendelea katika kipindi kile cha wakati ambacho viongozi waliopinga uongozi wa Moi walidhulumiwa.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imeangazia uwasilishaji wa wahusika katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba*. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995), mtafiti ameangazia wahusika kama vile Mumanyi, Munga, Warega, Omari, Obote, Khalifu na Amu zaidi.

Kupitia kwa wahusika hawa mtafiti ameweza kuangazia maudhui ya ufisadi, elimu, unyanyasaji, utabaka, ukombozi na ukabila. Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ni riwaya inayoangazia mambo ya kihalisia. Ni riwaya inayosimulia uhusiano baina ya viongozi na wanaongozwa.

## SURA YA NNE

## ATHARI ZA MATUKIO YA KIHISTORIA KATIKA KUWASILISHA MTINDO NA LUGHA KATIKA RIWAYA TEULE

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameangazia mtindo na lugha kama ilivyotumiwa katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995) ya *Rocha Chimerah* na *Mafamba* (2008) ya Tom Olali. Mtafiti ametaka kuchunguza athari za matukio ya kihistoria kwa mtindo na lugha. Mtafiti amefanya hivi akiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya inayotambua umuhimu wa muktadha wa kihistoria katika uteuzi, usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi.

### 4.1 Dhana ya Mtindo

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwingine.

Naye Wollheim (1995) anatofautisha kati ya mtindo wa jumla na mtindo binafsi. Anasema kuwa mtindo wa kijumla hulenga historia na wakati. Mtindo wa kibinafsi ni upendeleo mahsusi katika swala nzima. Mtindo huu hata hivyo, ni kitu ambacho hakiwezi kufunzwa lakini hutokana na ubunifu wa mwandishi. Wollheim (Keshatajwa) anaendelea kusema kuwa, mtindo binafsi una uhalisia wa kisaikolojia. Kutokana na maoni haya mtafiti ameweza kuchanganua mitindo tofautitofauti.

Mwandishi Rocha Chimerah katika riwaya ya *Nyongo Mkali Ini*, amedhihirisha upekee katika kazi yake pale ambapo ametumia lugha kiubunifu. Ametumia taswira, usimulizi, jazanda, hadithi na barua. Aidha, Tom Olali katika riwaya ya *Mafamba* pia amedhihirisha upekee kwa kutumia lugha kujieleza na kuwasilisha maudhui. Ametumia usimulizi, taashira, mafumbo, kinaya, visasili, nyimbo, ndoto, jazanda, na hotuba.

## 4.2 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Kuwasilisha Mtindo na Lugha katika Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995)

Mwandishi wa *Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini*, ametumia mtindo na lugha kwa namna ya kipekee katika kuwasilisha kazi yake. Mwandishi Chimerah, ametumia taashira na jazanda katika kazi yake.

### 4.2.1 Matumizi ya Taashira

Kwa mujibu wa TUKI English- Swahili Dictionary (2006), taashira ni matumizi ya tamathali za usemi katika mazungumzo au maandishi. Kwa mfano sanamu, picha na michoro. Taashira zilizotumiwa katika kazi hii ya kifasihi ni pamoja na damu, jipu. Mizoga, pembe za ndovu, picha na sanamu, gari la moshi na mzinga wa nyuki.

#### 4.2.1.1 Matumizi ya Taashira ya Jipu

Jipu ni mkusanyiko wa usaha katika sehemu yoyote ya mwili ambao mara nyingi husababisha uvimbe (TUKI, 2011). Dalili za kawaida za jipu ni maumivu kwenye eneo hilo, baridi, homa, kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi katika eneo lililoathirika, kuvimba kwa sehemu hiyo, kupoteza hamu ya kula, miongoni mwa mengine. Majipu hutokea wakati tishu za eneo fulani la mwili zinapopata maambukizi na mfumo wa kinga ya mwili ukijaribu kupigana nayo. Majipu yanaweza kusababishwa na bakteria, kimelea na kitu kigeni ndani ya mwili. Majipu kwenye ngozi ni rahisi kuonekana. Ni mekundu, yanavimba na kuuma.

Mumanyi alikuwa akiota jipu mara kwa mara. Anasimulia namna alivyoshuhudia jipu kubwa likitobolewa na kutoa mijisaha nyingi na baadaye mijidamu. Kutokana na masimulizi, inabainika kuwa mwenye jipu lile ni jamaa yake anayehisi uchungu na kisha akapona. Mumanyi anaendelae kueleza kuwa baada ya jamaa yake kupona hakupata jipu tena hadi alipoaga dunia.

> ‘‘Hebu tumrudie mgonjwa wetu. Kama mjuavyo, lisilo na budi halina budi. Hufika wakati jipu hilo likapasuka; likatoka mijisaha na mijidamu. Yakafika hapo, watu hao hao walikuwa wakikupapasa papasa, hushafukwa na moyo wakafanya kujikaza wasitapike. Kisha hujikaza sana. Maanake sasa una donda ati na jipu la kupasuka lenyewe donda lake ni ziwa zima. Unafiki nao hujiahiri hadi donda limepoa…’’ (uk 47).

Mumanyi anakiri kuwa palipomwaika usaha palikuwa na chungu wengi lakini baadaye wakafa. Aidha, vijana wengi wana majipu kwenye sehemu zao za siri na majipu haya husababisha vifo vyao wakati mwingine. Mwandishi ametumia

taashira ya jipu kuashiria uozo katika jamii. Uozo huu umesambaa kwa watu wote katika jamii, wazee kwa vijana. Mumanyi anaeleza jinsi jipu linavyoguswaguswa na kupapaswa. Msimulizi anaarifu kuwa vijana wengi, wavulana kwa wasichana, wana majipu katika sehemu zao za siri, na kwamba wakati mwingine majipu haya husababisha vifo vyao. Aidha, kutokana na mwandishi, ndoto za jipu humjia Mumanyi katika muktadha mahsusi. Baada ya mjadala, sentensi ya mwisho ilikaririwa akilini mwa Mumanyi hadi alipoenda kitandani na mwishowe akaota. Aliota kuhusu jipu.

> ‘‘Nilifikiria; jipu la namna ile nililiona wapi! Nikafikirii… nikafikiri wee… nikakumbuka. Mama mkubwa. Sasa ni marehemu…Mungu amweke mahali pema peponi. Alikuwa nalo, kubwa la pajani. Siku lilipotobolewa nilikuwapo. Naikumbuka kama mchana.’’ (uk 7).

Mumanyi anasimulia namna mama yake mkubwa alivyotobolewa jipu ambalo alikuwa nalo pajani. Mama yake alikuwa na uchungu ajabu. Baada ya kutobolewa na mijidamu kutoka ngozi ilishikana tena na nyama na mama akapona. Mijidamu na mijisaha iliyotoka kutoka kwa jipu lile iliwaua chungu wote waliokuwa mchangani. Mumanyi anasema kuwa hapana haja ya ugonjwa wa mtu mmoja kuwa kururi kwa chungu wasio na hatia, kisha yeye mwenyewe asife papo hapo.

Maelezo ya Mumanyi kuhusu jipu yanaibua swala la uozo uliokithiri katika jamii. Kupitia jipu la mama, msimulizi anaonyesha namna uozo wa viongozi huathiri watawaliwa. Viongozi hutengenezewa asali na wananchi walio katika tabaka la chini na kisha huila asali ile pasipo kujali maslahi yao. Kupitia dhana ya kutoboa

jipu na athari za mijidamu na mijisaha za kuua chungu, viongozi wanapojihusisha na uovu kama vile, ubinafsi, ufisadi, mauaji miongoni mwa mengine, wananchi huathiriwa moja kwa moja kwa kutozwa kodi za juu, kukosa baadhi ya mahitaji ya kimsingi miongoni mwa mengine. Mwandishi katika riwaya hii ameangazia namna wananchi riwayani walivyokosa mahitaji ya kimsingi kama vile maji na barabara kupitia kwa barua ya Chipuli Dzuya ifuatayo;

> ‘‘Sehemu kubwa za Uziwani hazina maji, hazina barabara za lami, hazina viwanda na kadhalika. Wajumbe wetu wanajaribu wawezavyo kuanzisha mipango kadha wa kadha kujisaidia wenyewe. ’’(uk 78)

Abdalla (1972) ameangazia shairi lenye anwani ‘Jipu’ katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Anasema kuwa moyo wake hauna furaha kwa ajili ya kuwa na jipu. Aidha, jipu linamkosesha usingizi kwa kuwa linachoma kama sindano. Isitoshe, anasema ya kwamba limemwathiri miaka mingi na kufanya akonde kama uzi. Jipu hili pia, linamfanya asiweze kuketi kwa hivyo, analazimika kusimama kutwa nzima. Jipu linamfanya akeshe kucha nzima. Mwandishi ana matumaini makuu na anasubiri kwa hamu siku ambayo jipu litatobolewa. Anaamini kuwa siku hiyo itakuwa siku ya furaha. Siku hiyo afya yake itamrudia. Kwa kurejelea shairi hili la Abdalla (2012), inabainika kuwa jipu linaweza kusitisha shughuli zote. Hivyo mgonjwa wa jipu akawa hawezi kufanya lolote.

Chimerah katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* alilenga kuangazia ufisadi, uongozi mbaya, mauaji, biashara haramu miongoni mwa mengine. Mwandishi anasawiri mgonjwa wa jipu kama Nchi. Atakapopona kwa kuchujuka, utakuwa mwanzo

mpya wa kuishi bila usaha ambao ni uozo mwilini. Kwa hivyo ni jukumu la wananchi kufanya juhudi zote ili kupambana na ufisadi na maovu mengine katika jamii ili taifa liendelee. Watawaliwa wanaweza kutekeleza hili kwa kuwachagua viongozi wanaofaa.

Mwandishi Rocha Chimerah aliathiriwa na uozo uliokuwa ukitendeka katika kipindi kile cha wakati. Kipindi hiki kilijawa na umwagikaji wa damu wakati wa harakati za ukombozi, ukabila, mizozo ya ardhi, ufisadi miongoni mwa mengine. Mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kuwa muktadha wa chimbuko la kazi ya fasihi husika huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi unafaa kwa kuwa umewezesha uchanganuzi maswala yaliyokuwa yakitendeka katika kipindi kile cha wakati ambayo yalihusu, mizozo ya ardhi, vita vya ukombozi, mauaji ya kisiasa, ufisadi na ukabila.

#### 4.2.1.2 Matumizi ya Taashira ya Damu

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa katika jamii zote ulimwenguni, rangi nyekundu ni ishara ya hatari. Wanaendelea kusema kuwa damu ikimwagika ni dalili iliyo wazi ya maonevu na ukandamizaji wa raia. Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* imejaa na habari za maafa. Watu wanakufa katika ajali za barabara ambazo hazijulikani jinsi zinavyotokea. Aidha, katika vita vya Maji Maji, mhusika Warega anatoa taswira inayoogofya ya damu nyingi kumwagika. Kisha Warega anasema kuwa;

> ‘‘Asubuhi hakuna kupumzika! Mtakuja chungwa kama mbuzi. Mpelekwe majiani kuchimba mahandaki ili MajiMaji wakija kutafuta vyakula majumbani waangukie humo. Na hii ilikuwa ni kazi ya kitumwa! Usiniinue mgongo; ukifanya hivyo ni mashaka. Utapigwa mpaka mwili mzima michirizichirizi ya damu. Wanawake wenye mimba uliweza kuwakuta wamelala, maiti (!) njiani, wamepasuliwa na kutolewa watoto. Isitoshe, watoto hao waliotolewa mimbani mwa mama zao walikatwakatwa vipande vipande... ’’(uk 58).

Isitoshe, ofisini mwa bwana Khalifu ukutani kuna ishara ya rangi nyekundu iliyochorewa mzinga wa nyuki na kuandikwa amri kumi za Mungu.

> Nilistaajabishwa na maandishi yaliyokuwa yameandikwa ukutani kwa rangi nyekundu juu ya kichwa cha Khalifu vile walivyoketi…. Amri zote kumi za Mungu, toka ya kwanza hadi ya mwisho. (uk 33).

Wenye kutekeleza maonevu katika riwaya hawajulikani kwa kuwa kuna siri kubwa kati ya wale wenye uwezo hivyo basi ushahidi haupatikani na umwagikaji wa damu unaendelea. Mumanyi anadhihirisha jambo hili anapokiri ya kuwa ingawa walipata kazi siku moja na Omari na Obote katika ofisi ya Bwana Khalifa, hakuelewa kazi waliofanya hasa.

> ‘‘…Ni Amu Zaid; na tulikuwa pamoja na Omari na Obote!. Hivyo wao hufanya kazi gani; mbona siwaoni ofisini…? Naam! Amu Zaid aligusia biashara ya pembe za ndovu…na hawa askari je…?’’(uk. 119)

Siku inawadia pale ambapo genge la wagandamizaji linaloongozwa na Khalifa litapatikana. Mwandishi Rocha Chimerah alifanikiwa kutumia taashira ya damu ili kubainisha maonevu na ugandamizaji uliokuwepo katika kipindi cha wakati alipoiandika kazi hii. Jamii katika riwaya hii imesawiriwa kuwa na maonevu na ugandamizaji ulioendelea kwa muda mrefu. Kipindi hiki ni cha uongozi wa

kikoloni na uongozi wa Kenyatta. Umwagikaji wa damu uliotokana na vita vya Mau Mau, siasa, ukabila, uongozi mbaya miongoni mwa mengine. Mhimili wa nadharia ya uhistoria mpya kwamba kazi za kubuni zina muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana unafaa kwa kuwa mwandishi kupitia taashira ya damu amelenga kuangazia maudhui ya dhuluma, mauaji, na ukandamizaji uliokuwa ukitendeka katika kipindi hicho maalum cha kiwakati.

#### 4.2.1.3 Taashira ya Pembe za Ndovu

Biashara ya pembe za ndovu ni biashara iliyopigwa marufuku. Kwa mujibu wa Kipengele Nambari 376 Cha Sheria Kinachohusu Utunzaji Na Uhifadhi Wa Viumbe Wa Pori. Atakayepatikana akiwinda ama akiwa na mnyama Pori atahukumiwa na kufungwa Jela. Wangomb'e (2019) anasema kuwa biashara haramu ya wanyama Pori huhusisha njia zisizofaa za uwakala, usafirishaji, uuzaji na ugawaji wa bidhaa za Porini. Mwandishi ametumia taashira ya pembe za ndovu kurejelea biashara haramu. Biashara haramu huendeshwa kisirisiri. Watu wanaoendesha biashara hizi hutajirika sana pamoja na wanaoshikiana nao. Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, mwandishi anabainisha namna biashara hii iliopigwa marafuku inavyoendeshwa kisirisiri kwa ushirikiano wa moja kwa moja wa wale wenye mamlaka ya sheria na matajiri. Kupitia kwa mhusika Mumanyi, inabainika kuwa Amu Zaid alishirikiana na mkuu wa Wilaya katika biashara ya kuuza pembe za ndovu. Aidha, vijana wachochole Omari na Obote walihusishwa kutokana na usemi huu wa Mumanyi;

> ‘‘Zilizokitwa upande huu na huu wa barabara_zinapogusana. Moja kwa moja akili yangu ilirukia biashara ya pembe za ndovu. Ni nani aliyetaja pembe za ndovu vile…? Na tuliokuwa pamoja ni kina nani alipotaja hivyo…? Aaaah…! Nishakumbuka sasa… Ni Amu Zaid; na tulikuwa pamoja na Omari na Obote! Hivyo wao hufanya kazi gani; mbona huwa siwaoni ofisini…? Naam! Amu Zaid aligusia biashara ya pembe za ndovu…na hawa askari je…? ’’(uk 93)

Hii ni biashara inayoendelezwa kwa siri. Kupitia kwa usimulizi wa mhusika Mumanyi inabainika kwamba biashara hii haramu inawahusisha wenye nguvu katika jamii, askari na vijana katika jamii. Anasimulia jinsi bwana Khalifu alivyosaidiwa na mkuu wa wilaya kuendesha biashara hii haramu. Aidha ,anaeleza namna Omari na Obote walivyohusishwa katika biashara hii haramu.

Mwandishi alilenga kuangazia taashira ya pembe za ndovu kuangazia hatari na uozo unaowakabili vijana. Biashara haramu ndizo zinazowasababishia majipu vijana. Biashara hizi ni pamoja na uhalifu, na uuzaji wa dawa za kulevya. Mwandishi amelenga kuonya vijana dhidi ya kujihusisha na biashara haramu. Kupitia kwa wahusika Alii wa Bokole, Omari na Obote mwandishi anaonyesha kuwa hatima ya ushirikiano kati ya matajiri na vijana katika biashara haramu huwa kuangamia kwa vijana.

Uhalifu wa vijana kwa jumla umekuwa ukipanda Afrika, hasa katika miji ambapo kuna vijana wenye umri kati ya miaka 12 hadi 25. (UN-Habitat, 2011). Aidha, tatizo la uhalifu wa vijana nchini Kenya lina asili yake katika nyakati za ukoloni pale ambapo wakoloni walipata upinzani mkubwa kutoka kwa jamii nyingi vijana

wakiwa kwenye mstari wa kwanza katika kupinga kuwepo kwao (Kyamana, 2015).

Isitoshe, kulingana na ripoti ya UN Habitat (2011) kuhusu vijana na uhalifu mjini Nairobi, vijana wengi wamepatikana na makosa ya wizi ambao ni asilimia 23, waliopatikana na dawa za kulevya ni asilimia 10, ujambazi asilimia 10 na mauaji asilimia 7. Aidha, vijana hutumia bunduki, panga na visu kutekeleza uhalifu. Lengo la uhalifu huu ni kutafuta pesa (UN Habitat report, 2011).

Rocha Chimerah, amesawiri jamii yake ikiwa na vijana waliosoma kwa mfano Mumanyi lakini hawana kazi. Aidha, Omari, Obote na Alii wa Bakole ni vijana wanaotumiwa na wakwasi kama vile Bwana Khalifu katika kutekeleza uovu hasa ule wa kujihusisha na biashara haramu ya uuzaji wa pembe za ndovu. Mhimili kuwa kazi ya kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee unafaa kwa kuwa mwandishi wa riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ameshughulikia swala la biashara haramu kupitia kwa uuzaji wa pembe za ndovu ambayo ni taashira ya jumla ya uhalifu uliotendeka nchini Kenya katika kipindi cha wakati ambapo mwandishi Rocha Chimerah alitunga riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini.*

#### 4.2.1.4 Taashira ya Sanamu na Picha

Kuna sanamu za watu ambao walipigania vita vya pili vya dunia katika riwaya. Sanamu ya Mfalme Joji wa Sita inatajwa. Aidha, kuna picha ya Malkia Elizabeth wa Uingereza ambayo imo chumbani mwa Mzee wa Mji. Mzee huyu ni mhudumu wa serikali. Vilevile kuna picha ya Rowland Vidzo. Picha na Sanamu ya Malkia Elizabeth na Mfalme Joji ni ishara ya Ukoloni Mamboleo. Ingawa viongozi hawa hawakutawala nchi moja kwa moja, athari za uongozi wao bado zingalipo. Kupitia kwa Mumanyi, inabainika kuwa sanamu ya mpiganaji ambaye ni Jenerali Marisheli haikuwepo. Jambo hili linaonyesha namna Mwafrika anavyodhalilisha mwafrika mwenzake na kumsifia au hata kutambua Mzungu;

> ‘‘Kwa upande mwingine, juu ya kitanda cha babake Omari, zipo picha mbili zivutazo nathari ya wale waonao aibu kujiangalia pale kiooni. Picha zenyewe ni za mtu na mkewe. Mkono wa kushoto ni ya prince Philip, Duke of Edinburg na mkono wa kulia ni ya Elizabeth wa pili ambaye ni Malkia wa Uingereza. ’’(Uk 2)

Segell (2019) anasema ya kwamba bara la Afrika limeathiriwa na Ukoloni Mamboleo. Ukoloni huu Mamboleo ulirudisha nyuma Bara la Afrika. Ukoloni Mamboleo huhusisha mikopo ambayo haijadhibitiwa, biashara, uekezaji wa moja kwa moja na ushirikiano kati ya viongozi wa Kiafrika na viongozi wa Kigeni, ili kuhakikisha kwamba maslahi ya wakoloni yameangaziwa bila kujali sana suala la maendeleo, uhimili, umaskini na ustawi wa nchi za Kiafrika.

Rocha Chimerah ameangazia suala la elimu ambayo inapatikana kwenye riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Elimu hii inabainika kuwa elimu isiyofaa kwa msingi kuwa

vijana wengi wamesoma ila hawana kazi. Inabanika kuwa sera kuhusu elimu ni suala ambalo halijazingatiwa vyema. Mfumo wa elimu unaofuatwa nchini Kenya ulianzishwa na Mwingereza. Mfumo wa elimu nchini Kenya ni ishara ya ukoloni mamboleo kwa kuwa, ingawa haina manufaa kwa vijana hasa katika kupata kazi, bado inaendelezwa. Mwandishi kupitia kwa wahusika Mumanyi, Obote na Munga unausawiri mfumo na sera ya elimu kama ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Kwa mujibu wa Maloba (2017), baada ya wakoloni kuondoka, usimamizi wa wananchi uliwachwa mikononi mwa tabaka la wasomi na wenye uwezo. Aidha, viongozi hawa walikuwa wale ambao walielewa mienendo ya wakoloni na wakaanza kuendeleza. Uchumi wa nchi ya Kenya unaendelea kutegemea teknologia, fedha, kibiashara, Uingereza, Marekani, Japani na Uchina. (Ndege, 2009).

Mhimili wa nadharia ya uhistoria kuwa kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano na kimwingiliano matini na wala sio kazi zinazotakana na ubunifu wa mwandishi pekee yake una mashiko.

### 4.3 Matumizi ya Jazanda

Kwa mujibu wa Okwena (2013), jazanda ni taswira au picha ambayo hujirudia katika kazi ya fasihi na ambayo ndani yake maana ya kitu imefichama. Jazanda

zilizotumika katika riwaya ya *Nyongo Mkali Ini* ni pamoja na Nyongo, Ini, Nyuki, mikebe ya asali na mti ambao ni makao ya nyuki. Kwa mujibu wa Okwena (2013), jazanda hutumiwa katika kazi za fasihi ili kusawiri mawazo ya mtunzi kwa undani na kumpa msomaji uwezo wa kufahamu zaidi.

### 4.3.1 Matumizi ya Jazanda katika *Nyongo na Ini*

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) nyongo ni majimaji machungu yanayotengenezwa na Ini kwa ajili ya kuyeyusha na kusaidia katika usagaji wa chakula tumboni. Ini ni kiungo ambacho hutoa nyongo na hubadilisha glukosi kuwa glukojeni, kiungo kinachopima kiwango cha sukari katika damu. Nyongo hutengenezwa na kuhamishwa kutoka ndani ya ini hadi kongosho, Baadaye, nyongo huvutwa tena na ini kwa kipimo ili kusaidia na kurahisisha shughuli za kusagia chakula.

Katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*, viongozi wanalinganishwa na Nyongo. Mwandishi ametumia jazanda ya Nyongo ili kuonyesha jinsi viongozi wanavyochaguliwa na wananchi ili watimize ahadi wanazotoa wakati wa kampeni. Kwa kutumia jazanda hii, viongozi wanapaswa kurahisisha maishi ya wananchi ambao ni Ini kama namna nyongo na ini mwilini wanavyohusiana kama viungo vya mwili. Inabainika kuwa nyongo huhitaji sana ini. Mwandishi kupitia kwa riwaya hii, anaonyesha namna viongozi hujitakia makuu baada ya kuchaguliwa. Pia huwanyanyasa na kuwagandamiza watawaliwa. Ili Taifa liweze kustawi na

kuendelea kiuchumi, ini ambalo ni jazanda ya wananchi wana jukumu la kuwachagua viongozi ambao wanaajibika. La sivyo Taifa litazorota kimaendeleo. Mwandishi anaonyesha kuwa hatari inaweza kutokea iwapo ini litaondolewa pasi kuwa makini. Anasema kuwa nyongo inaweza kumwagika na kuharibu ini kwa maana kwamba kuwaondoa viongozi kwa mabavu kunaweza kuleta michafuko ambayo inaweza kuwa na athari za mauaji na kuzorota kwa uchumi. Kupitia kwa masimulizi ya Mumanyi, ini lina jukumu la kuichuja nyongo. Hivyo ni jukumu la wananchi kuwachagua viongozi ambao wana sifa za uajibikaji. Ikiwa wananchi wanaongozwa vizuri, watapata maendeleo na uchumi wa nchi utastawi. Hapo nyongo itakuwa imefanya kazi pamoja na ini ipasavyo.

Aidha, wananchi wanapotawaliwa vibaya, nyongo kwa kuwa inapatikana juu ya ini haipati madhara lakini ini hupata madhara hasa ya kisukari. Hii ina maana kuwa nchi huzorota kimaendeleo na suluhisho huwa ni kuondoa nyongo. Yaani kuwachagua viongozi wengine ambao wataajibika.

Kwenye riwaya hii, mwandishi ameangazia swala la ugandamizwaji. Wananchi wanaishi kama maskwota katika nchi yao kwa kuwa mashamba yote yamemilikiwa na wageni. Mwandishi anathibitisha swala hili kupitia kwa usemi huu;

> ‘‘Mimi naona mwandishi amefanya utafiti wa kutosha na kutoa ukweli wote kuhusu hali ilivyo… Tazama hapa mikadini. Sote ni wapangaji katika mashamba ya Wahindi na Waarabu. Wenyewe

> wakiamua kutufukuza wakati wo wote watafanya hivyo hata kama ni usiku.'' (uk 79).

Kupitia kwa barua ya Dzuya, inabainika kuwa mahitaji ya kimsingi kama vile maji na barabara hayapatikani. Isitoshe, viongozi wanashughulikia mahitaji yao binafsi baada ya kuchaguliwa.

> ''Sehemu kubwa za uziwani hazina maji. Hazina barabara za lami, hazina viwanda na kadhalika. Wajumbe wetu wanajaribu wawezavyo kuanzisha mipango kadha wa kadha ya kujisaidia wenyewe.'' (uk 78).

Mwandishi anaangazia namna nyongo (viongozi) walivyotelekeza majukumu yao isivyofaa hivi kwamba baadhi ya mahitaji ya kimsingi kama vile maji, barabara na mahala pa kujisetiri hayapatikani. Mwandishi Rocha Chimerah ameyasawiri maswala yaliyokuwa yakitendeka katika kipindi cha kiwakati cha utawala wa ukoloni hadi kipindi cha utawala wa Rais Kenyatta. Kupitia kwa jazanda ya Ini, inabainika kuwa wananchi hawakupata huduma walizostahili kupata kutoka kwa viongozi wao. Pia wahusika Mumanyi, Munga na Obote, ni kiwakilishi cha vijana wasomi ambao hawana kazi. Isitoshe kisa cha nyuki kinadhihirisha namna tabaka la chini linavyofanya kazi lakini nyenzo zote za kuzalisha mali zinamilikiwa na tabaka la juu. Mhusika Omari anasema;

> ''La hasha. Sikusema hivyo. Nimesema ndio hao nyuki wanaotaka kula asali peke yao. Ni lazima ufahamu kuwa ikiwa pana nyuki watakao wale asali peke yao, lazima wapo wengine wanaonyimwa asali; kama kina Omari hapa.'' (uk. 40).

### 4.4 Athari za Matukio ya Kihistoria katika Uwasilishaji wa Mtindo na Lugha katika Riwaya ya *Mafamba* (2008)

Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba*, Tom Olali ametumia mtindo na lugha kwa namna ya kipekee katika kuwasilisha kazi yake. Njogu na Chimerah (2008) wanasema ya kwamba mbinu ya usimulizi hutumiwa kwa lengo la kurahisisha uelewa wa maudhui. Mwandishi Olali ametumia mbinu za maelezo, utambaji, mjadala, nyimbo na mdokezo.

#### 4.4.1 Matumizi ya Maelezo

Maelezo ni mbinu ya kufafanua jambo au maneno kwa kueleza kwa kina (TUKI, 2006). Mwandishi ametumia mbinu ya maelezo kwa lengo la kuwasilisha maudhui na pia kusawiri sifa za wahusika wake. Mwandishi kupitia kwa maelezo, anaelezea jinsi Maotad alivyotawala sayari ya NUKA kwa muda mrefu. Aidha, anasema kuwa Maotad alikatalia kwenye kiti cha enzi ambacho ni Ikulu. Isitoshe, anaeleza namna alivyokorofishana na Amrao. Kupitia kwa mbinu hii pia, Maotad anasimuliwa kama mhusika hatari aliyetisha na hata kuwaua wapinzani wake kama vile Rojoo.

> ‘‘Maotad alikataa katakata kutoka chumbani_chumba maalum. Chumba ambacho Amrao na LiMioe walikitaka. Muda ulipita na alianza kukorofishana na Amrao.’’ (uk 6).

Msimulizi pia anasema hivi,

> ‘‘Halijulikani jina hilo Maotad lilitoka wapi ama kutokana na nini. Macho yake yalikuwa makali, meusi na yangeenda sawia na miale ya jua kwa uangavu. Iliaminika macho ya Maotad yangalimulika, yangalipenya mbavu za mwathiriwa yeyote. Iliaminika miongoni

> mwa wakazi wa Bikerani-Msiige kuwa macho haya ya Maotad yaliweza kuupenya mwili wa mkazi mmoja wa sayari ya NUKA aliyeitwa Rojoo. Miale mikali kutoka macho ya Maotad ilipompenya maskini ,alikata roho.'' (uk 7).

Mwandishi kupitia kwa maelezo anatoa habari kuhusu Amrao. Anaonyesha namna Amrao alivyokuwa mtu mwenye mamlaka makubwa katika sayari ya DiPieLi. Anaeleza namna Amrao alivyotoa maneno yenye athari kamili kwa hadhira. Msimulizi kupitia mbinu hii anamsawiri mhusika Amrao kama kiongozi mwenye umaarufu na mwenye wafuasi wengi sawia na Maotad. Umaarufu wake uliwatia wengi tumbo joto akiwemo Maotad. Isitoshe, msimulizi anaeleza namna Amrao alivyofungwa jela kwa kutofautiana na uongozi wa Maotad;

> ''AMRAO alikuwa na mamlaka makubwa katika sayari ya DiPieLi. Kila alipozungumza watu wa sayari ya DiPieLi walimsikiliza kwa wingi wa makini. Sifa zake Amrao zilienea na alijulikana na watu wa sayari ya NUKA kama vile alivyojulikana Maotad. Yeye Amrao alisukumwa ndani kwenda kula maharagwe katika kipindi kimoja cha jumla ya miaka thelathini.'' (uk 24).

Mwandishi anaendelea kusimulia kwa kueleza sababu za tofauti kati ya Maotad na Amrao. Anasema kuwa tofauti hizi zilitokana na falsafa zao mbalimbali kuhusu MAFAMBA. Msimulizi anasema kuwa Amrao alikashifu Mafamba naye Maotad alisifia;

> ''Tofauti kati ya Maotad na Amrao zilisababishwa na falsafa zao mbalimbali kuhusu MAFAMBA. Mafamba tu. Basi. Hakukuwa na jingine. Na kwa sababu ya tofauti hizo, Amrao alisukumwa ndani. Maotad alimtukuza mafamba naye Amrao alimkashifu mafamba. Wote wawili waliyatathmini maneno kutoka wa kila mmoja na kuyachuja. Amrao alilichuja hili naye Maotad akalichuja neno lile.'' (uk 31)

### 4.4.2 Matumizi ya Mjadala

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja* (2011) mjadala ni kuzungumzia jambo kwa kushirikisha mtu au watu ili kuweza kuelewa vyema au kulipatia ufumbuzi. Kupitia kwa mjadala kati ya Maotad na Shanata, inadhihirika kuwa Maotad ni katili na yeyote ambaye hujaribu kumpinga Maotad hufa. Aidha, ni kupitia kwa mjadala huu ambapo Shanata alipendekeza muungano kati ya Sayari ya NUKA na DiPieNi;

> ‘‘Mh. Endelea, Maotad alimhimiza Shanata aendelee Ninakupa nafasi nyingine, Maotad alimhakikishia Shanata.
> Naomba mambo mawili, aliuliza Shanata huku akiwa sasa ametulia.
> Nayo ni? Alitaka kujua Maotad.
> Mosi, naomba kusimama kukupa ushauri wangu.
> Pili, naomba kutokufa baada ya kukupa ushauri huo, Shanata alimaliza maombi yake yakipenya mboni za macho ya Shanata. Walitazamana kwa muda. Muda ukapita.
> Sawa, Maotad alimhakikishia Shanata shingo upande.
> Sayari ya NUKA itakuja pamoja na ile ya DiPieNi. Tutakuwa kitu kimoja na ile ya DiPieNi. Tutakuwa kitu kimoja. Lakini alama zetu na rangi zetu zinazoitetea sera ya mafamba zitabakia vile vile. Watu wetu tutawakanya wasiingiliane sana na wakazi wa DiPieNi kwa vile hawaaminiki. Tutawahadaa tu. Tuna uwezo huo…alianza Shanata huku akionyesha dalili za kutaka kujua zaidi. Aliendelea Shanata. ’’(uk 22).

Kupitia kwa mjadala kati ya LiMioe, Fadhila na Boyi, mwandishi anaonyesha namna wahusika hawa walivyokutana ili kujadili jinsi ya kuwa na muungano wa vyama vya kisiasa. Walikuwa na nia ya kuondoa mafamba. Kupitia kwa mazungumzo kati yao, walionelea kuwa, ikiwa wangeungana wangemshinda Maotad na chama chake cha NUKA. Inabainika kupitia kwa mjadala huu kuwa Boyi ni Kinara wa KEFO naye LiMioe alikuwa kinara wa PiDi.

> ‘‘Asante Fadhila. Umetujua sisi. Hata hivyo tutajifahamisha tu. Mimi ninazungumza kwa niaba ya mwenzangu hapa…alimeza mate machungu Boyi na kuendelea. Naam, mimi ni Boyi. Boyi ni mimi. Ndimi kinara wa sayari ya KEFO. Endelea Boyi, alihimiza Fadhila.
> Asante Fadhila. Naam, huyu ni LiMioe. LiMioe ni huyu. Ndiye kinara wa sayari ya PiDi. Ndiyo, PiDi. Hivyo huyu ni LiMioe kinara wa sayari ya PiDi. Ndiyo, PiDi. ’’(uk 39-40).

### 4.4.3 Matumizi ya Utambaji

Kutamba ni kusimulia au kuhadithia. Mwandishi Tom Olali ametumia mbinu ya utambaji katika kazi yake kwa kutaka kusisimua, kuteka makini ya msomaji, kuwasilisha maudhui na kusawiri sifa za wahusika (TUKI, 2000).

Mwandishi anatamba kuhusu kiongozi wa sayari ya NUKA. Anasimulia namna wakazi wa Bikerani-Msiige walivyotaka aondoke mamlakani lakini kiongozi huyo hakuwa tayari kuondoka mamlakani. Anaeleza kuwa wafuasi wake walitaka asalie uongozini. Kiongozi Amrao alikuwa hasidi wa Maotad kwa kuwa alitaka kurithi uongozi. Kupitia kwa mbinu ya utambaji, mwandishi ameonyesha namna kiongozi wa sayari ya NUKA alivyotawala kwa muda mrefu na hakuwa tayari kuondoka mamlakani;

> ‘‘Mtu yule aliyekemewa na Arijojo aliitwa Maotad. Jina lake maarufu lilikuwa Aende. Kila mara wakazi wa Bikerani- Msiige walimwambia aende! Maotad alikuwa kiongozi wa sayari iliyoitwa NUKA. Alikuwa maarufu na kupendwa na wale ambao haja zao zilikidhiwa na kutimizwa. Wale ambao haja zao zilinyimwa kama Arijojo walimwita Aende. Arijojo aliamua kukabiliana na Aende. Kwa ghadhabu kuu, Arijojo alitupa tusi ambalo halichapiki. Wewe mtu nenda zako, alifoka Arijojo Aende! Aende! alipata shime kutoka kwa Amrao na wakazi wengine wa Bikerani-Msiige.

Amrao alikuwa ni mwandani wake Arijojo – waliletwa pamoja na dhiki waliyoamini ilisababishwa na Maotad, na azma yao ilikuwa ni ile ile moja_maji matamu.'' (uk 4).

Mwandishi anasimulia kuhusu asili ya NUKA. Anaeleza kuwa sayari hii iliumbwa yapata miaka arobaini iliyopita. Anasema ya kuwa sayari hii ilinukia zamani lakini baada ya Arijojo na wakazi wa Bikerani-Msiige kuudhika na Maotad ikabatizwa NUKA. Kupitia kwa utambaji wa mwandishi inabainika kuwa sayari hii ilinuka kutokana na mafamba au uozo uliokuwepo chini ya uongozi wa Maotad. Msimulizi anasema kuwa uozo huu ulichafua viatu vya wageni. Hili ni suala linaloonyesha athari za mafamba kwa jamii nzima na hata kwa Mataifa ya kigeni;

> ''NUKA ilikuwa sayari ya zamani sana. Muumba alipoiumba KARIFA, sayari ya NUKA iliumbwa yapata miaka 4000 iliyopita. Sayari nyingi ziliundwa kama vile NUZAPIFU, NUTA na ELIMO-FR. Katika sayari zote hizi, iliyojulikana sana ni NUKA. Zamani sana ilijulikana kama NUKIA. Arijojo na wakazi wa Bikerani-Msiige, waliibatiza jina jipya-NUKA baada ya kuudhika na Maotad. Sasa sayari hii iliitwa NUKA- sayari maarufu kupita zote. Ndiyo, sayari ya NUKA. Sayari ambayo ilipata umaarufu wake kutokana na vitu vyenye kuvutia-matapishi, hewa mbaya, mbwedu, dondandugu, uvimbe na kuliko yote, mafamba. Maotad kwa niaba ya wenyeji wa NUKA alicheka kirefu na wakajitapikia ovyo. Matapishi yao yalivichafua viatu vya wageni waliozuru NUKA!'' (uk 8).

Aidha, mwandishi anasimulia kuhusu asili ya sayari ya KEFO. Anaeleza kuwa ilizaliwa kutoka kwa EF na kuwa kinara wake ni Boyi. Anasema ya kuwa Boyi ni kinara ambaye hakushiriki wala hakupenda mafamba;

> ''Shanata alianza kusimulia asilia ya sayari ya KEFO; Zamani sana palikuwa na sayari kubwa sana ilijulikana kama EF. EF waikumbuka nusra isababishe vifo vyetu. Hakika tulikufa kisha tukafufuka baada ya wewe kufanya maarifa. Sayari hii iligongwa na mwamba mkubwa kutoka nyota kubwa ya angani. Shanata alifikia glasi ya maji iliyokuwa kando yake na kuimimina maji

> kinywani mwake. Kisha aliendelea. Mwamba huo uliteremka kwa kasi ya kilomita takriban milioni 70 kwa sekunde na ulipogonga EF, tokeo lilikuwa ni kuzaliwa kwa vijisayari vingine vidogo ambavyo vyote vilibeba visifa vidogovidogo vya sayari ya EF. Kimojawapo cha vijisayari hivyo ni KEFO. Kinara wa KEFO ni Boyi. ’’ (uk 23).

### 4.4.4 Matumizi ya Nyimbo

Kulingana na Matei (2011) anasema ya kwamba fasihi simulizi imeathiri fasihi andishi kwa kuzingatia mbinu za uwasilishaji na kimaudhui. Aidha, anasema kuwa msimulizi wa hadithi anaweza kutumia nyimbo kufanikisha usimulizi wa hadithi yake. Katika riwaya ya *Mafamba*, Tom Olali ametumia nyimbo kuwasilisha maudhui yake.

Aidha, Matei (2011) anaongezea kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti, muwala na mapigo ya kimuziki na huwasilishwa kwa kuimbwa. Anaendelea kusema kuwa nyimbo hutumia lugha nzito yenye kuibua taswira na hisia nzito kama mapenzi, huzuni na furaha. Aidha, nyimbo hutumiwa kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo Fulani. Isitoshe, nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni za jamii. Matei (2011) anaendelea kusema kuwa nyimbo za kisiasa zina majukumu mengi katika jamii yakiwemo kuzindua na kuhamasisha watu, kusawiri mfumo wa kisiasa katika jamii, kusawiri migogoro iliopo katika jamii, kueneza propaganda, kurekodi matukio ya kihistoria, kukashifu uongozi mbaya, kuwasifu viongozi waadilifu miongoni mwa mengine.

Wamitila (2003) anasema ya kwamba nyimbo huwa na mawazo mazito na hupaniwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha.

Baada ya kiongozi wa NUKA kutawala nchi kwa muda mrefu, aliibadilisha nchi kutoka kwa hali ya KUNUKIA na kuwa NUKA. Hili lilisababishwa na hali ya mafamba ambayo ni hali ya uozo ulioshamiri katika jamii. Wapinzani wa Maotad pamoja na wananchi wa Bikerani-Msiige walichoshwa na hali hii na kupendekeza Maotad aende. Walikuwa wamechoshwa na utawala wake. Maotad kupitia kwa wimbo uliotungwa na wakereketwa wake aliwajibu wapinzani kwa kuyasifia mafamba;

NUKA ikipenda huna budi kupenda
NUKA ikichukia huna budi kuchukia
Ikiwa hupendi NUKA pia yumkini haitapenda
Mafamba, Mafamba ni hali ya maisha
Maisha ya binadamu
Mafaaaaaamba!!

Na hali ya maisha ni Mafamba,
Nani anayedhulumiwa na Mafamba?
Ni nani?
Maisha ya binadamu
Mafaaaaamba!!

Mafamba mtu safi sana
Mafamba mtu safi sana
Mafamba mtu safi sana
Maisha ya binadamu
Mafaaaaamba!!
Na kama si dhehebu ni sera
Kwa sababu Mafamba ina wafuasi wake

Wafuasi wakeeee
Maisha ya binadamu
Mafaaaaamba!!

Maendeleo ya sayari ya NUKA
Barabara za sayari ya NUKA
Ni kutokana na Mafamba
Maisha ya binadamu
Mafaaaaamba!! (uk 36-37)

Mwandishi kupitia kwa wimbo huu amefanikiwa kukejeli uongozi wa Maotad uliojaa mafamba ambayo ni maovu. Wimbo huu umetekeleza jukumu la kusawiri jamii inayotawaliwa na Maotad. Kupitia kwa wimbo huu, mwandishi amebainisha ya kwamba mafamba ni hali ya kawaida, hali ya maisha na kuwa lolote linalofanywa katika sayari ya NUKA linatokana na mafamba. Mwandishi amefaulu katika kutumia mbinu ya wimbo kuwasilisha mengi yanayohusiana na uongozi mbaya wa kiongozi Maotad. Wimbo huu pia unabainisha ya kwamba kuna watu halisi au wafuasi wa mafamba. Hawa ni wakereketwa wa Maotad. Wafuasi hawa hujihusisha na nyendo chafu ambazo zinarejelewa kama mafamba.

Aidha, kupitia kwa wimbo mwingine kwenye riwaya, inabainika kuwa Amrao ni kiongozi ambaye alichukia mafamba. Hili ni jambo ambalo lilileta tofauti kati yake na Maotad. Mwandishi anaeleza kuwa wawili hawa walikuwa mahasidi ambao waliwindana. Inabainika ya kwamba tofauti zao za kisiasa zilisababisha Amrao alifungwa jela. Akiwa gerezani alitunga wimbo ufuatao:

Mimi Amrao nina wajibu
Mimi Amrao nina wajibu
Mimi Amrao nina jibu

Mimi Amrao nina jibu
Wajibu wa kuzitetea haki za wakazi wa sayari zote

Jibu la kuzitetea haki za wakazi wa sayari zote
DiPieNi, PiDi, NUKA, MARS
Wajibu wangu
Wajibu wangu
Wajibu wangu
Ni kufungua kambi za kusoma
Wajibu wangu
Ni kuongeza vituo vya afya
Wajibu wangu
Ni kujenga barabara
Wajibu wangu
Ni kuleta usalama
Wajibu wangu
Ni kuufufua uchumi
Wajibu wangu kamili
Wajibu wangu kamili
NI KUKOMESHA MAFAMBA
NI KUKOMESHA MAFAMBA
NI KUKOMESHA MAFAMBA (uk 27-28)

Mwandishi kupitia kwa wimbo wa Amrao analenga kuonyesha namna kiongozi Amrao alivyokuwa tayari kuzindua na kuhamasisha jamii katika kuondoa mafamba. Kupitia kwa wimbo huu yuko tayari kuajibikia jamii kwa kutetea haki zao. Aidha, yuko tayari kutumikia jamii kwa kufungua kambi za kusoma, kuongeza vituo vya afya, kujenga barabara, kuleta usalama na kufufua uchumi. Kupitia kwa mbinu ya takriri kwenye wimbo huu, wajibu wake kamili ni kukomesha mafamba. Mwandishi ametumia mbinu ya uradidi ili kusisitiza wajibu wa Amrao hasa ni kukomesha mafamba.

Matei (Keshatajwa) anasema ya kwamba nyimbo za kisiasa huzindua na kuhamasisha watu. Vile vile, nyimbo hizi huwatanabahisha watu kuhusu haki zao

na kuwahimiza kupigana dhidi ya unyanyasaji. Licha ya Amrao kuwa ndani wakati wa kutunga na kuimba wimbo huu, mwandishi Olali analenga kuonyesha kuwa Amrao ni kiongozi ambaye ni mkakamavu na mtetezi wa haki za wanyonge.
Mwandishi Olali (2008) ametumia mbinu za usimulizi kuyasawiri matukio halisi ya kihistoria yaliyotokea nchini Kenya. Njogu na Chimerah (2008) wanahoji kuwa fasihi ni sanaa inayowasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Aidha, msomaji na msikilizaji wa kazi ya fasihi huingiliana na tajiriba za hali iliyowasilishwa na wahusika wa kazi hiyo kama walivyosawiriwa, na huku akikata kauli kuhusu ukweli, uhalisi, na ubora wa yale anayokumbana nayo.

**4.4.5 Matumizi ya Anagramu**

Anagramu ni mbinu ya kuunda neno kwa kubadilisha herufi za neno hilo (TUKI-*English-Swahili Dictionary*, 2000). Mwandishi Tom Olali amefanikiwa kutumia mbinu hii katika kuviangazia vyama tawala vilivyokuwepo katika kipindi cha kihistoria cha kuanzia utawala wa Moi hadi utawala wa Kibaki. Aidha ni kupitia mbinu hii ambapo ameweza kuangazia miungano ya vyama hivi. Vyama alivyovitaja ni kama vile NUKA, Dipieli, PIDI, NUTA, KEFO, ASIFO, PIDIELI.

Mwandishi Olali (Keshatajwa) ametumia mbinu ya Anagramu ili kuficha hali halisi ya kihistoria kama ilivyojitokeza nchini Kenya. Wahusika wake wakuu ni viongozi wa kisiasa ambao waliwahi kuishi katika kipindi cha utawala wa Rais

Moi na Rais Kibaki. Wahusika hawa ni Maotad ambaye ni Daniel Toroitich Arap Moi, Amrao ambaye ni Raila Amolo Odinga, LiMioe ambaye ni Emilio Mwai Kibaki, Rojoo ambaye ni John Robert Ouko, Sinya ambaye ni Simeon Nyachae, Manstanji ambaye ni Stanley Jindo Matiba miongoni mwa wengine. Aidha, kupitia kwa mbinu hii amefanikiwa kuficha vyama halisi vya kisiasa vilivyokuwepo katika kipindi hicho maalum cha kiutawala. Vyama hivyo ni NUKA-KANU, DiPieLi-LDP, DiPieNi- NDP, PiDi-DP, NUTA- TANU, miongoni mwa vingine.

Kwa mujibu wa Mink (1974), fasihi si masuala ya kidhahania. Uhalisia unatokana na historia. Olali (2008) ameyaangazia maswala yaliwahi kutokea katika kipindi cha wakati cha utawala wa Rais Moi na Rais Kibaki. Ni kipindi kilichoshuhudia mabadiliko mengi ya vyama vya utawala. Kupitia kwa mbinu ya anagramu, mwandishi amebainisha vyama vya utawala vilivyokuwepo katika kipindi kile cha kiwakati. Matumizi ya anagramu yanashajiisha ubunifu wa majina wa masimulizi.

### 4.4.6 Matumizi ya Mdokezo

Kwa mujibu wa *Kamusi Ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) kudokeza ni kumpa mtu fununu kuhusu jambo fulani. Mwandishi Tom Olali (Keshatajwa) amefanikiwa katika kutumia mbinu hii ili kuficha hali halisi ya kihistoria kama ilivyojitokeza na pia kuonyesha umaarufu wake wa kuboronga lugha.

Mwandishi anasimulia kuhusu ajali mbaya ya barabarani. Anadokeza kuwa ilitokea pande za Nzambani. Anasimulia namna siasa zilivyokuwa zimeshika kasi wakati ambapo LiMioe pamoja na wafuasi wake walipokuwa wanatoka Ukambani na gari likapata ajali mbaya ya barabarani. Mwandishi kupitia kwa mbinu ya mdokezo anasimulia kuhusu tukio la kihistoria lililohusisha aliyekuwa rais wa nchi ya Kenya kwenye ajali mbaya ya barabarani. Mink (1974) anasema ya kwamba fasihi haitokani na ombwe tupu bali hutokana na mazingira halisi ya watu. Katika riwaya ya *Mafamba*, hoja hii kupitia kwa mbinu ya mdokezo ni dhahiri kwa kuwa msimulizi amefafanua kisa halisi kilichotokea katika mazingira halisi. Msimulizi amezitaja sehemu halisi, tukio halisi na watu halisi waliowahi kuishi. Ni tukio lililohusisha Rais Kibaki kwenye ajali mbaya ya barabarani wakati wa kampeni za kura ya maoni nchini Kenya alipokuwa akitoka kufanya kampeni za kura ya maona na kuhusika katika ajali mbaya ya barabarani huko Ukambani. Mwandishi anadokeza sehemu ya kampeni na kutokea kwa ajali kama Nzambani.

### 4.5 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti umebainisha jinsi mtindo na lugha umetumiwa vilivyo na wasanii kuwasilisha matukio ya kihistoria. Imebainika kuwa, mwandishi Rocha Chimerah ametumia jazanda na taashira kwa wingi ili kuficha matukio aliokuwa akiangazia kwa kuwa aliandika kazi yake katika kipindi cha wakati ambao hakukuwa na uhuru wa kujieleza nchini Kenya. Kipindi hiki kilikuwa kipindi cha utawala wa wakoloni na utawala wa Rais Moi. Aidha, utafiti umebaini kuwa, Tom

Olali ametumia mbinu mbalimbali ambazo zina uwazi zaidi, katika kuangazia matukio yaliyotukia katika kipindi cha wakati ambamo mlikuwa na uhuru wa kujieleza. Kipindi hiki ni kipindi cha kidemokrasia nchini Kenya. Mbinu za uwasilishaji alizotumia ni pamoja na maelezo, mjadala, utambaji, mdokezo na nyimbo.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Lengo kuu la sura hii lilikuwa kutoa muhtasari, mchango na mapendekezo ya utafiti huu. Utafiti huu umeshughulikia riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008). Utafiti huu ulibaini namna matukio ya kihistoria yalivyoathiri waandishi wa riwaya teule katika uwasilishaji wa maudhui, wahusika na mtindo na lugha.

Uteuzi wa riwaya hizi *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008), ulichochewa na wazo kuwa riwaya hizi zina tofauti ya mwongo mmoja katika kuandikwa kwake. Aidha, kila riwaya iliandikwa katika nyakati tofauti za kiutawala nchini Kenya. Hivyo, waandishi hawa wameathiriwa na yale yaliyokuwa yakitendeka katika vipindi hivyo maalum vya kiutawala.

### 5.1 Muhtasari

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya Kwanza imezungumzia maudhui kwa mujibu wa matukio ya kihistoria. Sura hii imeangazia vipengele vya kimsingi vinavyohusiana na utafiti. Aidha, sehemu hii imebainisha sababu za kuchagua mada pamoja na nadharia ambayo imeongoza utafiti huu ambayo ni nadharia ya uhistoria mpya. Pia, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada yamefafanuliwa. Mbinu za

ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo umeshughulikiwa.

Sura ya Pili iliangazia uwasilishaji wa maudhui yaliyochipuzwa na matukio ya kihistoria. Maudhui haya ni mizozo ya ardhi, vita vya uhuru, siasa, elimu, usaliti, vita vya uchaguzi na ukombozi. Aidha, maudhui haya yamejadiliwa kwa namna ya kudhihirisha kuwa yameathiriwa na matukio ya kihistoria katika vipindi maalum vya kiwakati ambavyo ni kipindi cha utawala wa ukoloni, kipindi cha utawala wa Rais Kenyatta, kipindi cha utawala wa Rais Moi na kipindi cha utawala wa Rais Kenyatta.

Sura ya Tatu imejadili wahusika wa kihistoria katika riwaya teule. Katika sura hii wahusika wamechorwa na kuwasilishwa kwa kuhamasishwa na wahusika halisi wa kihistoria katika riwaya za Rocha Chimerah na Tom Olali. Waandishi wametumia mbinu tofauti katika uainishaji wa wahusika. Rocha Chimerah kwa mfano, ameainisha wahusika kwa kutumia kigezo cha umri na utabaka. Aidha, Tom Olali ametumia mbinu ya maelezo, mjadala, utambaji, nyimbo, anagram, na mdokezo na katika kuwasilisha mtindo na lugha.

Sura ya Nne imechunguza namna matukio ya kihistoria yameathiri uwasilishaji wa mtindo na lugha katika riwaya teule. Rocha Chimerah amefanikiwa katika matumizi ya taashira katika kuangazia maswala mbalimbali kama vile ufisadi,

mauaji, biashara haramu na elimu. Aidha, ametumia jazanda ya nyongo na ini kuangazia uhusiano wa watawala na watawaliwa mtawalia. Mwandishi Tom Olali aidha, ametumia mbinu ya masimulizi, hadithi ndani ya hadithi, nyimbo na anagramu katika kuangazia maswala mbalimbali nchini Kenya katika kipindi cha utawala wa Rais Moi hadi utawala wa Rais Kibaki.

Sura ya Tano ni hitimisho la tasnifu. Hitimisho hili la tasnifu limedokeza utangulizi na muhtasari wa kila sura. Aidha, maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Pia, sura hii imeeleza matokeo na mapendekezo ya utafiti.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu umebaini kuwa, waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008) wameathiriwa na matukio ya kihistoria katika kazi zao. Malengo ya utafiti huu yalikuwa, kubaini iwapo matukio ya kihistoria huathiri jinsi waandishi wanavyowasilisha maudhui yao, kuchunguza jinsi matukio ya kihistoria huathiri uwasilishaji wa wahusika na kuchunguza namna matukio ya kihistoria huathiri mtindo na lugha ambayo wandishi hutumia kuwasilisha kazi za kifasihi.

Lengo la kwanza, lilikuwa kubaini iwapo matukio ya kihistoria huathiri jinsi waandishi wanavyowasilisha maudhui yao. Utafiti ulipata kwamba, maudhui yaliyoshughulikiwa katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* ni mizozo ya ardhi, vita vya uhuru, siasa, elimu na utabaka. Kuhusu maudhui ya ardhi, utafiti ulionyesha

ya kwamba serikali iligawanya mashamba baina ya Waafrika, Kugawanya huku kuliibua migogoro miongoni mwa makabila mbalimbali ya Kiafrika. Aidha, umiliki wa ardhi ulibadilika kutoka kwa asasi za kijamii na kumilikiwa na mtu binafsi.

Mtafiti alipata kwamba, vita vya mau mau vilipangwa msituni na walioshukiwa kushirikiana na mau mau waliuawa kinyama. Aidha, Wachovya walidhaniwa kuwa ndio waliopigania uhuru.

Vilevile, utafiti ulibaini kuwa siasa ni sanaa ya kuongoza na kutawala nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali. Kuna mauaji ya kisiasa. Aidha, kupitia kwa matukio ya kihistoria kuna baadhi ya viongozi waliodhulumiwa kisiasa kwa mfano, Abdilatif Abdalla kwa sababu ya msimamo wake wa kisiasa.

Aidha, awali wanajamii walielimisha wana wao. Baada ya kuja kwa Wakoloni mfumo wa elimu ulibadilishwa. Mfumo huu mpya ulikumbwa na upinzani kutoka kwa wenyeji. Sababu kuu ya upinzani huu ilikuwa ni mila na dini. Utafiti pia uliangazia migomo na maandamano katika vyuo vikuu, shule za upili na shule za msingi.

Isitoshe, jamii inayopatikana katika riwaya iligawika kwenye tabaka la juu na tabaka la chini. Kwa kutumia mfano wa nyuki na asali, kuna wale waliofanya kazi

kwa bidii na wakati huo huo wale waliojifaidi kutokana na bidii hiyo. Mwandishi kama macho ya jamii, anasawiri watu wa tabaka la chini kama wanaonyanyaswa na wale wa tabaka la juu. Kupitia kwa barua ya Dzuya, inabainika kuwa watu wa tabaka la juu waliwanyanyasa wale wa tabaka la chini. Watu wa Uziwani wamekuwa kama wapangaji na walinyang'anywa mashamba yao.

Aidha, maudhui ya ufisadi yamesheheni katika riwaya ya *Mafamba.* Kuna sakata mbalimbali riwayani kama vile Anglolasting na Goldenberg. Ni sakata zilizohusisha viongozi waliokuwa katika serikali ya Moi. Utafiti ulipata ya kwamba licha ya tume mbalimbali kubuniwa ili kuchunguza kashfa hizi hakuna aliyehukumiwa.

Vilevile, maudhui ya siasa yanajitokeza katika riwaya ya *Mafamba*. Kupitia kwa maelezo ya mwandishi, kuna mbinu mbalimbali zilizotumiwa na wanasiasa kushinda uchaguzi. Mbinu hizi ni pamoja na kuwaua wapinzani, kuungana kwa vyama mbalimbali vya kisiasa, propaganda, ahadi za uongo na pia kuwapa wananchi pesa ili wawachague.

Isitoshe, maudhui ya elimu yanajitokeza katika riwaya ya *Mafamba.* Kuna elimu ya kisiasa na elimu ya shuleni. Kupitia kwa utawala wa BORA elimu ya bure ilipatikana na watoto wengi wakaweza kujiunga na shule ya msingi. Kuhusu elimu

ya siasa, wanasiasa wengi walifunzwa siasa na Maotad. Ndiposa hawaoni tofauti kati ya utawala wa Maotad na Bora.

Pia, vita vya uchaguzi vilitokea kwa sababu ya tamaa ya uongozi hasa kati ya Limioe na Amrao. Mwaka wa 2700 kulikuwa na patashika kati ya Limioe na Amrao kila mmoja akishikilia kuwa alishinda uchaguzi. Utafiti ulibaini ya kuwa jambo hili lilipelekea kuwepo kwa vita kati ya wafuasi wao. Kulishuhudiwa uharibifu wa mali. Mwandishi anatumia wakati ujao yaani 2700 kusawiri matukio ya historia.

Licha ya hayo, wanajamii wa riwaya ya *Mafamba* wanatafuta njia za kujikomboa kutokana na wanasiasa wanaovuja mali. Kupitia kwa kupiga kura waliamua kuwangoa mamlakani wanasiasa wanaoendeleza sera ya ‘mafamba’. Viongozi wanaohusishwa na sera ya mafamba kama vile Damisi wanang’olewa mamlakani. Aidha, utafiti ulipata kuwa wakati wa vita hivi vya uchaguzi, kulikuwa na harakati ya ukombozi. Harakati hii ilihusu ugavi wa mamlaka kati ya Limioe na Amrao.

Mbali na hayo, kulikuwa na usaliti wa kisiasa. Ilibainika kuwa Amrao, Saigeo na Kamu waliungana na kundi Limioe kwa sababu walihisi ya kwamba walikuwa wamesalitiwa na Maotad. Hii ni kwa sababu Maotad aliwaahidi uongozi lakini hatimaye Maotad aliamua uongozi wa sayari ya NUKA ungechukuliwa na U. Aidha, Limioe aliwahidi kuwatengea nafasi Fadhila, Amrao na Kamu baada ya

kuchukua uongozi. Hata hivyo, Limioe anaenda kinyume na mkataba huo. Hali kadhalika utafiti ulibaini kuwa wanasiasa huwasaliti wananchi. Kupitia kwa hotuba ya Limioe, ahadi nyingi zinaonekana zikiwemo kuteua viongozi wasiohusishwa na mafamba. Kiongozi huyu hakuweza kutimiza ahadi hizo. Utawala wake unageuka na kuwa utawala wa mafamba. Rais Kibaki aliwasaliti Ngilu, Kalonzo na Odinga kwa kuvunja mkataba waliokuwa nao wa kuwatengea nyadhifa za juu uongozini baada ya kura ya mwaka wa 2002. Hili ni jambo ambalo hakutimiza. Licha ya kuwaahidi wananchi kuwa utawala wake ungekabiliana na ufisadi, utafiti ulipata kuwa utawala wake ulikumbwa na kashfa mbalimbali ikiwemo ile ya angloleasing.

Aidha, kupitia kwa wahusika, mwandishi aliangazia maudhui ya ufisadi, elimu, dhuluma, utabaka, ukombozi na ukabila kwenye riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini.* Aidha, utafiti ulipata kuwa mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* aliangazia maswala ya ufisadi, siasa, miungano ya vyama vya kisiasa, mauaji miongoni mwa mengine. Kupitia kwa sifa, hulka, matendo ya wahusika na uhusiano miongoni mwao.

Pamoja na hayo, mhusika Omari alitumiwa na mwandishi Chimerah ili kuangazia maswala ya uozo katika jamii. Mhusika Omari alitumiwa vibaya na bwana khalifa ambaye alikuwa mkwasi. Aidha,anabainisha uwezo wa matajiri juu ya maskini. Anatumiwa kutekeleza mauaji ya wote walioshuku na kupinga nyendo za bwana Khalifa.

Isitoshe, mhusika Mumanyi ni mhusika mwenye kisomo cha kutosha ila hana kazi. Alisawiriwa kuakisi wasomi wa kihistoria wa miaka ya themanini na tisini waliokuwa na kisomo lakini hawakuwa na kazi. Isitoshe, mhusika huyu alikuwa na utambuzi wa mambo. Aliweza kutafiti kuhusu fumbo la nyuki. Utafiti ulibaini ya kuwa Mumanyi ni kielelezo cha wasomi wengi wa miaka ya 1980 na 1990 waliokuwa wafikirivu.

Aidha, mhusika Munga ni mwanamaendeleo  na mwanamapinduzi. Alifahamu mambo kitaaluma. Alijiamini sana kujikomboa kwa njia za elimu na utafiti. Mhusika huyu alitetea haki za wanyonge na kupingana na udhalimu unaoendeshwa na wenye mamlaka.

Vilevile, Bwana Khalifu ni mhusika wa kubuni anayeakisi jamii ya kihistoria na kisasa. Mwandishi alimsawiri kama tajiri mwenye mali na ushawishi mkubwa. Utafiti ulibaini kuwa, bwana Khalifa  alikuwa mfisadi na mgandamizaji. Mhusika huyu anawaajiri vijana ili kutekeleza maovu riwayani.

Aidha, katika riwaya ya *Mafamba*, mhusika Maotad ni mhusika wa kihistoria ambaye amewahi kuishi. Utafiti ulibaini kuwa kiongozi huyu alikuwa na sifa ya ukatili. Ilidhihirika ya kuwa aliwaua wapinzani wake kwa mfano Rojoo. Utafiti ulibaini kuwa hili ni tukio la kihistoria ambapo John Robert Ouko aliuawa kwa sababu za kisiasa.

Isitoshe, utafiti ulibaini ya kuwa mhusika Amrao ambaye ni Raila Odinga ametekeleza jukuma la kuunda, kuelekeza, kuathiri na kuamuru siasa nchini Kenya kwa miaka mingi. Aidha, Raila ametekeleza jukumu kubwa miaka ya themanini katika kupigania mfumo wa vyama vingi nchini Kenya.

Utafiti ulibaini kuwa Limioe ni mhusika wa kihistoria. Mwai Kibaki alihusika katika kuchukua uongozi nchini Kenya uiokuwa mikononi mwa rais Moi kwa zaidi ya miongo miwili. Aidha ajali mbaya ya barabarani ni tukio la kihistoria lililohusisha Rais Mwai kibaki wiki chache kabla ya uchaguzi wa mwaka wa 2002. Utafiti pia ulibaini kuwa Rais Kibaki aliapishwa akiwa mgonjwa.

Vilevile, utafiti ulibaini kuwa mhusika Manstanji ni Stanley Jindo Matiba. Utafiti ulibaini kuwa Matiba na Moi hawakuwa na uhusiano mwema. Aidha sababu kuu ya uhasidi ni kwamba Matiba aliongoza katika harakati za kuanzisha mfumo wa vyama vingi nchini Kenya jambo ambalo halikupokelewa kwa mikono miwili na Moi. Utafiti ulibaini kuwa jambo jambo hili lilifanya afungwe jela na maisha yake yakabadilika kutokana na mateso aliyoyapata.

Kupitia kwa kipengele cha wahusika, inabainika kuwa mwandishi Rocha Chimerah ameathiriwa na matukio ya wakati wa ukoloni na utawala wa Rais Jomo Kenyatta nchini Kenya katika kuwasawiri wahusika wake. Aidha, Tom Olali amewatumia wahusika wake katika kuangazia yale yaliyokuwa yakiendelea katika

nchi ya Kenya kuanzia kipindi cha kiwakati ambapo rais Moi alikuwa akitawala katika mfumo wa chama kimoja hadi pale nchi ilipopata demokrasia. Aidha, kupitia kwa sifa, matendo na mahusiano ya wahusika, utafiti ulibaini yale yaliyokuwa yakiendelea katika kipindi hicho cha kiwakati.

Kuhusu mtindo na lugha, utafiti ulipata ya kwamba, mbinu mbalimbali zilitumiwa ili kuangazia maswala tofauti kwenye jamii. Kwa mfano, taashira ya jipu ilitumika kuashiria uozo kwenye jamii. Taashira ya damu aidha, ilitumika kuashiria mauaji yaliyosheheni kwenye jamii. Taashira ya pembe za ndovu iliashiria biashara haramu. Utafiti pia ulipata kuwa kulikuwa na taashira ya sanamu na picha. Isitoshe, mwandishi alitumia jazanda ya nyongo na ini kuonyesha watawala na watawaliwa mtawalia.

Kwenye riwaya ya *Mafamba*, utafiti ulipata ya kwamba mbinu ya masimulizi, hadithi ndani ya hadithi, nyimbo na anagramu zilitumika. Ulinganishi wa vipindi hivi tofauti vya kiutawala katika historia ya nchi ya Kenya ulituwezesha kuonyesha kuwa matukio ya kihistoria yaliathiri waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* katika kuwasilisha maudhui, wahusika na mtindo na lugha.

Isitoshe, mihimili ya nadharia ya uhistoria mpya ilikuwa mwafaka katika kuongoza utafiti huu. Aidha, fasihi sio matokeo ya ubunifu pekee bali huhusisha

kazi zingine. Mihimili ya nadharia hii ilituwezesha kuelewa matukio ya kihistoria katika nchi ya Kenya kutokea kipindi cha utawala cha wakoloni, kipindi cha utawala cha Kenyatta, kipindi cha utawala cha Moi na kipindi cha utawala cha Kibaki. Aidha, vipindi hivi maalum vya tawala mbalimbali za kisiasa vimesaidia katika kuelewa athari za matukio ya kihistoria katika uwasilishaji wa maudhui, wahusika na mtindo na lugha katika riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba.*

## 5.3 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa matini za kutosha kuhusu nadharia ya uhistoria mpya katika lugha ya Kiswahili. Hivyo data nyingi ilitokana na tafsiri kutoka kwa matini za kiingereza.

## 5.4 Mchango wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu utawafaa wasomi, kwa kuwa utaonyesha mtagusano kati historia na fasihi. Mtafiti anatarajia kuwa wasomi wengine watanufaika kwa kuwa utafiti huu utahifadhiwa katika makataba. Aidha, mitindo imewekwa wazi katika kuwasawiri wahusika kwenye riwaya. Mwandishi Olali ametumia mtindo wa kipekee katika kubainisha wahusika. Kwa kuchanganua maudhui, wahusika na mtindo, utafiti huu umechangia katika kuonyesha mtagusano kati ya historia na fasihi.

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu umelenga kuchunguza athari za matukio ya kihistoria katika uwasilishaji wa maudhui, wahusika na mtindo na lugha katika riwaya za Nyongo *Mkalia Ini* (1995) na *Mafamba* (2008). Utafiti huu ulijikita katika riwaya ambazo zina tofauti ya zaidi ya mwongo mmoja. Utafiti zaidi wa aina hii unaweza kufanywa kwa kuzingatia kipindi tofauti cha kiwakati. Aidha, usomi wa baadaye unaweza kuzingatia nadharia ya uhistoria mpya katika ushairi au tamthilia.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (2012). *Sauti ya Dhiki*. Oxford University Press. East Africa Ltd.

Abdulaziz, M. H. (1979). *Diwani ya Mashairi ya Muyaka*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abubakar, M. (mh) *Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara (mtu ni kwao japo chini mwa irara).*

Adero, C. M. (2005). *Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya kuanzia Mwaka wa 2002 hadi 2005*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi.

Africa confidential (2002). Mwai's moment: the Rainbow Coalition looks like the People's Choice ahead of President Moi's retirement: *Africa confidential* 43(24), 6 December.

Amutabi, N.M. (2002). *Crisis and student protest in universities in Kenya*, examining the role of students in National Leadership and Democratization Process. Cambridge university presss.

Asamba, M. (2018, March 27). Raila vows to sue Cambridge Analytical, facebook for running devilish propaganda. *The Standard. https://www.standardmedia.co.ke/kenya/article/2001274653/raila-vows-to-sue-cambridge-analytica-facebook-for-running. Retrieved 24th June 2019.*

Balkaya, A.M. (2014). Basic Principles of New Historicism in the light of Stephen Greenblatt's *Resonance and Wonder and Invisible Bullets*. Aksray University. Turkey.

Bennet, N. R. (1978). *A History of the Arab State of Zanzibar.* London: Methuen Co. Ltd II New Fetter Lane London EC4P4EE.

Boone, C. (2011). "Politically Allocated Land Rights and Geography of Electoral Violence: The Case of Kenya in the 1990s.'' Katika *Comparative Political Studies.* 44 (10), 1311-1342.

Boone, C. (2012). “Land Conflict and Distributive Politics in Kenya.’’ Katika *African Studies Review*, 75-103.

Branch, D. (2011). *Kenya: Between Hope and Despair, 1963-2011*. Yale University Press.

Bressler, C.E (2003). *Literary criticism. An introduction to theory and practice.* New Jersey: Pearson Education, Inc.

Butler, M. (1984). History in Literature. The Renaissance-Theatre and Crisis. 1632-1642. Cambridge University Press. Cambridge.

Chimerah, R. (1995). *Nyongo Mkalia Ini.* Nairobi: Oxford University Press.

Craig  D. (1975). *Marxists on Literature. anAnthology*. Hadmordswoth: Penguin.

Crystal, D and Davy, D. (1969). Investigating English style; London: Longman group ltd.

Foucault, M. (1972). *The Archaeology of Knowledge and the Discourse of Language.* New York: Routledge Publishers.

Frye, N. Baker S. na Perkins, G. (1985). *The harper Handbook of literature.* New York: the Harper Collins. College publishers.

Greenblatt, S.J. (1980). *Renaissance Self- Fashioning, from more to Shakespeare*. Chicago and London: UCP, Print.

Greiner, C. (2013). “Guns, Land and Votes: Cattle Rustling and the Politics of Boundary Making in Northern Kenya.’’ Katika *African Affairs*, 112 (447), 216-237.

Holman, C.H (1976). A handbook of literature. Indianpolis, the Odyssey press.

Hornsby (2012). *Kenya, A History since independence*. Bloomsbury Academic.

K'okul, F. (2010). *Perception of Students on Status of Guidance and Counselling in Selected Universities in Kenya for Minimising Student Riots*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

*Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011). Longhorn Publishers. Nairobi. Kenya.

Kanyinga, K. (1998). Politics and Struggles for Access to Land: 'Grants from Above' and 'Squatters' in Coastal Kenya. Katika *The European Journal of Development Research*, 10 (2), 50-69.

Kapiyo, N.W, Kiruthi, F. M, and Kimori (2000). *The Evolving World*. A History and Government course, Form Four. Oxford University Press. Nairobi.

Kapiyo, N. W (2011). *The Evolving World, a History and Government Course Book.* Oxford University Press East Africa.

Keesey, D. (2003). *Historical Criticism*, Context for Criticism. Mayfield Publishing Company. London.

Kezilahabi, E (1972). *The Development of Swahili Poetry*: 18th – 20th C in Kiswahili. Chuo Kikuucha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Kimeu, A. N. (2016). Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti. (Haijachapishwa).Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi.

King'ei, G. K. na Kisovi, M. (2005). *Misingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kingei, G. K. (1999*)*. Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili. *Journal of the Faculty of Arts Kenyatta University.uk 48*

Kinoti, T.M. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi. Kenya.

Kivuva, J. (2015). Kenya's benefit less democratization. GREAT insights magazine, volume 4, issue 3, April/ May 2015.

Klopp, J.M. and Orina J.R. (2002). University crisis activism and Contemporary Struggle of Democracy in Kenya in African Studies. Review, vol. 45, no 1. Cambridge.org. uk 43-76.

Klopp, J. M. (2001). "Ethnic Clashes" and Winning Elections: The Case of Kenya's Electoral Despotism. Katika *Canadian Journal of African Studies*, 35 (3), 473-517.

Kombo, K. na Tromp, A. (2006*). Proposal and Thesis Writing*. An Introduction. Nairobi: Pauline Publishers.

Kyamana, S. (2015). Factors contributing to crime among male urban youth: A case of pumwani-majengo ward, Nairobi. Nairobi: University of Nairobi.

Kyle, K. (1999). The Politics of The Independence of Kenya, London: Macmillan Press

Madumulla, J. (1998*). Riwaya ya Kiswahili Tanzania, Mulika 20*: Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mahoney, J. (2010). The Sino-Kenyan Relationship: An Analysis of African Motivation for Engaging with China. B.A.Thesis, Massachussets. Williams College.

Maloba, O.W. (2017). *The anatomy of neo-colonialism in Kenya: British imperialism and Kenyatta, 1963-1978:* Switzerland; springer science and business media: Palgrave Macmillan.

Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Shule Za Upili. Oxford University Press. Nairobi, Kenya.

Materu, F. (2015). *The post-election violence in Kenya. Domestic, and international legal responses.* Dar es Salam. T.M.C.Asser Press.

Mbatiah, A. M. (1995). *Mapitio ya Riwaya ya Walenisi. Kioo Cha Lugha:* University of Dar es Salaam.

Mbatiah, A. M. (1998). *Mienendo Mipya Katika Uandishi wa Kezilahabi*: Nagona Na Mzingile. *Mulika*: University of Dar es Salaam.

Mbatiah, A.M. (1999). “The Origin and the Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania” Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mbatiah, A.M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*; Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbatiah, A.M. (2003). “*A Critical Approach to Wamitila’s Nguvu ya Sala*”: *Hekima*, Journalof the Humanities and Social Sciences, University of Nairobi.

Mbatiah, A.M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili:* Chimbuko na Maendeleo yake. J. K. F: Nairobi.

Mdee, J.S. Njogu, K. na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya karne ya 21*. Longhorn publishers, Nairobi Kenya.

Mink, L. O. (1970). *History and Fiction as Modes of Comprehension: New Directions in Literary History* (Ed Ralph Cohen) Baltimore: The John Hopkins University Press.

Mlacha, S. (1984). ‘*Riwaya za Visiwani (1970-1980) na ujenzi wa jamii mpya’ katika Mulika no. 16*. Uk 84. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mlaga, W. (2017). *Uhistoria katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano katika Riwaya za ‘Ndoto ya Ndaria’, ‘Gamba la Nyoka’ na ‘Miradi ya Wazalendo’*. Kiswahili 78, no. 1 (2017).

Mlaga, W.(2015). *Uhistoria Katika Riwaya ya Kiswahili;* https://www. Researchgate. net/publication/321309790. Ilipakuliwa tarehe 20/10/2020

Mligo, E. J. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki.* Dar-es-Salaam Ecunemical Gathering.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.

Muhammed, K. (1988). *Utenzi Wa Ukombozi Wa Zanzibar*.Oxford University Press.

Munyao, R. (2017). Mwingiliano Wa Fasihi na Historia Katika *Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara*. *Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuuu Cha Nairobi.

Munyole, S. D. (2017). *Usomaji na Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwanakupona*. (Haijachapishwa). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi,

Muraya, J. (2020, February 19). I will never forgive Moi, Torture Victim Says On Visting Nyayo House. *Capital News*. https://www.capitalfm.co.ke/news/2020/02/i-will-never-forgive-moi-torture-victim-says-on-visiting-nyayo-house/ Retrieved on 24th Octomber 2020

Mwirabua, A.K. (2009). "Ukoloni Mamboleo na Utandawazi Katika Tamthilia Teule.'' *Tasnifu ya Uzamili.* Chuo Kikuu Cha Kenyatta.(Haijachapishwa).

Nasimiyu, C. (2008). Athari za mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Kenyatta. (haijachapishwa).

National Crime Research Centre (2018 a). *Borderland-related crimes and security threats in Kenya.* Nairobi, Kenya: The Jomo Kenyatta Foundation publishers.

National Crime Research Centre (2018). *Perspectives of youth criminality in Kenya*.from the findings of both Natonal Crime Mapping (2016) and Probation Orders report (2018).

Ndege, P.O, (2009). *Colonialism and its legacies in Kenya;* lecture delivered during Fulbright – Hays Group Project Abroad Program: July 5th to August 6th 2009 at the Moi University main campus.

Ndonga, A. na Carranza, R. (2019). Can Buiding Bridges Break the Cycles of Corruption and Political Violence in Kenya? Nairobi: *ICTJ Briefing*.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*: University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2016). *Ufundishaji wa Fasihi*. *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, A. W. (2014). Viongozi kama Visababishi vya Mabadiliko katika za Riwaya za Mwenda Mbatiah: *Vipanya vya Maabara na Majira ya Tufani*. (Haijachapishwa). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi.

Nkinyangi, J. A. (1981). The Origins of Student Disturbances: The Kenyan Case. Working Paper No. 378. Nairobi Institute of Development Studies, University of Nairobi.

Nthenya E. S. (2007). *Haini;* Kama Riwaya ya Kihistoria. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Obonyo, O. (2017, May 28). A journey through raila Odinga's politics. *Daily Nation.* Retrieved from http://www.nation.co.ke/news/raila-odinga-politics-kenya/1056-3945030-3vnfthz/index.html. Retrieved on 27th November 2020.

Okoth-Ogendo, H. W. O. (1989). Some Issues of Theory in the Study of Tenure Relations in African Agriculture. *Africa: Journal of the International African Institute. Cambridge University Press*, 6-17.

Okwena S. (2013). *Matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu za Timothy Arege* (haijachapishwa).tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Olali T. M. (2008). *Mafamba*; Nairobi; Jomo Kenyatta Foundation.

Omary, M. (2011). *Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008).* (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.

Onoma, A. K. (2010). “The Contradictory Potential of Institutions.’’ In Mahoney, J. & Thelen, K. (Eds.) *Explaining Institutional Change*, 63-93.

Onsando, E. (2015, October 8). Raila’s role in Kenyan politics unrivalled. *The Standard.* https://www.standardmedia.co.ke/ureport/article/2000178967/railas-role-in-kenyan-politics-unrivalled. Retrieved on 24th August 2020.

Orwa, D.K. (1992). Independent Kenya External Economic Relations In Ochieng, R. W and Maxon, R. M. (Ed) An Economic History of Kenya. Nairobi. East Africa Education Publishers.

Otinga, Rene (15 April 2018). Veteran politician Kenneth Matiba is dead” *TUKO.co.ke*. Retrieved 15 April 2018.

Owallah, K. (2013). Uhakiki wa maudhui Teule katika utenzi wa Nabii Isa. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Oyugi,W., Wanyande, P. na Mbai, C. O. (2003). The politics of transition in Kenya. From KANU to NARC. *Heinrich Boll Foundation.* Nairobi.

Rajmund, O. (2005). Historical Approach to Swahili Literature: As Here to fore an open Question. *Kiswahili Juzuu la 68 Dar es Salaam*; TUKI 2005.

Rollins, J. D (1983). A History of Swahili Prose. From earliest times to the end of the nineteenth century. Brill. Leiden.

Segell, G. (2019). Neo-Colonialism in Africa and two Cases of Turkey and Iran. Insight on Africa, 2019. Journals. Sagepub.com.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi Na Jamii;* Dares-Salaam; Tanzania Publishing House.

Sharma, R. (2014). *New historicism: an intensive analysis and appRaisal in India.* Review of World Literature in English, 10 (2), 1-11.

Southall, R. (2005). The Ndungu report: land & graft in Kenya. *Review of African Political Economy*, 32(103), 142-151.

Standa, E. M. (2000). Report of the Vice-Chancellor's Committee on the causes of Disturbance/Riots in Public Universities. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Steeves, J. (2006). Presidential Succession in Kenya: The Transition from Moi to Kibaki. *Commonwealth & Comparative Politics,* 44 (2), 211-233.

TUKI English- Swahili Dictionary (2006). Book Printing Services Ltd. Dar es Salaam.

Ukkan, R. P. (2004). *Approaching New Historicism*. Critical Practice.

UN Habitat (2011). *Youth and Crime in Nairobi*. Nairobi: UN.

Wa Kinyatti, M. (2008). *History of Resistance in Kenya*. Nairobi: Mau Mau Research Centre.

Wafula, R. M na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi Jomo Kenyatta Foundation.

Walloga, L. (5 June 2013). "Detention saved Matiba from the sword of KANU killers, says, Edith" *Nation Media Group*. Retrieved 10 July 2019.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele vyake*: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*; Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi* : *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide- Muwa Publishers.

Wang'ombe (2019). Assessment of the Factors That Have Led To Increased Poaching Activities. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Wayua (2020). Raila Odinga's framed political brand image and the voters reasoned actions. In presidential elections. *Tasnifu ya Uzamili*. Daystar University.

Wellek, R na Warren, A. (1994). *Theory of Literature*. London: Penguin Books, Harmondsworth.

Wollheim, R. (1995). Style in Painting in the Question of Style in *Philosophy and the Arts*, edited by Caroline Van Eck, James McAllister, and Renee van de vall, 37-49. Cambridge: Cambridge Universtiy Press.

Zaja, J. O. (1986). *Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*, Matatizo na Athari zake (Haijachapishwa) chuo Kikuu cha Nairobi.